# Nipashe

Jumanne Januari 28, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580139

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



**TAARIFA KWA UMMA**

**Regency Medical Centre** tunatangaza kuanzia leo na kuendelea usambazaji wa madawa utakua unafanyika kupitia mfumo wa mitandao. Wasambazaji wetu wote na wauzaji wanaweza kufikia mfumo wa zabuni kupitia tender.regencymedicalcentre.com.

Kama ukihitaji kujisajili wasiliana nasi kupitia +255 784417500/ +2221050500 au barua pepe kutoka anuani ya barua pepe iliyopendekezwa pamoja na jina la muhusika, namba ya simu kwenda appointments@regencymedicalcentre.com. Mtu wa kuwasiliana nae atakuwa msimamizi wa duka la dawa

115602402




## Lipumba afunguka sakata la kukamatwa, hatima upinzani

UKURASA 3

# MSAKO KABAMBE

**TCRA** yatangaza uhakiki laini za simu zilizosajiliwa kwa majina ya wengine, watakaofumwa...*Endelea ukurasa wa 2*


## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**


**600 WALIOZINGIRWA NA MAFURIKO WAOKOLEWA**
WAKAZI zaidi ya 600 kutoka vijiji vitano wilayani Kilwa mkoani Lindi waliokuwa wamezingirwa na mafuriko...

**UKURASA WA 4**

**WAZIRI AWAPANGUA WATUMISHI HOSPITALI**
SERIKALI imemwondoa Mfamasia wa Wilaya ya Mkuranga, Dk. Elly Mende, katika nafasi yake pamoja...


## MGANGA AFUNGWA MAISHA UBAKAJI

UKURASA 3



Mshtakiwa ambaye ni mganga wa kienyeji, Venas Edward (48), mkazi wa Ujiji, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, akiangua kilio, huku akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi katika Mahakama ya Wilaya ya Kigoma, jana, baada ya kuhukumiwa kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kosa la kumbaka mtoto. **PICHA: JOCTAN NGELLY**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


# Magufuli ampa kibarua kizito Simbachawene

**AMTAKA** asiingiwe na 'pepo' kama wenzake, amtahadharisha watendaji wabovu ndani ya wizara...*Endelea ukurasa wa 2*


**MICHEZO** KOBE BRYANT, GIANNA WALIVYOACHA MAJONZI UK. 32 | MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Msako waliosajilia wengine laini waja

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na watoa huduma, imetangaza kufanya uhakiki wa laini zote za simu zilizosajiliwa ili kuondoa wale waliosajili kwa kutumia kitambulisho cha mtu mwingine.

Pia uhakiki huo utawahusu wale waliosajili laini zao kwa kutumia kitambulisho tofauti ambao wote watachukuliwa hatua za kisheria.

Kwa mujibu wa tangazo la mamlaka hiyo lililochapishwa na gazeti hili juzi, TCRA imeamua kufikia uamuzi huo ili kujiridhisha waliosajili laini zao za simu kwa kutumia kitambulisho sahihi.

Ofisa mwandamizi wa TCRA, alipoulizwa kuhusu lini uhakiki huo utaanza, alisema hawajasema wataanza lini, huku akiendelea kusisitiza uzimaji wa laini ambazo hazijasajiliwa linaendelea.

Katika tangazo hilo, TCRA ilisema kuwa kwa kushirikiana na watoa huduma itafanya uhakiki huo.

"Kusajili laini ya simu kwa kutumia kitambulisho cha mtu mwingine ni kosa sanjari na kupewa laini iliyojasiliwa na mtu mwingine."

Tangazo hilo limesema kuwa onyo na tahadhari zitaendelea kutolewa kwa makundi yote yanayohusika na usajili wa laini hizo.

"Kwa waliositishiwa huduma za laini zao za simu kuanzia Januari 20, wanaweza kuendelea na utaratibu wa usajili kwa lengo la ama kurudisha laini hizo zilizofungwa kama zitakuwa bado zipo au kupata mpya, mchakato huu ni endelevu," sehemu ya tangazo hilo ilisema.

Pia tangazo hilo linasema watumiaji au waombaji wapya wa laini za simu wataendelea kusajiliwa muda wowote kwa kutumia kitambulisho cha Taifa na kuhakikiwa kwa alama za vidole.

Uzimaji wa laini za simu ambazo hazijasajiliwa ulikuwa ufanyike Desemba 31, mwaka jana, lakini Rais John Magufuli aliongeza siku 20 na mchakato huo ulikamilika Januari 20, mwaka huu.

Akitoa taarifa za uzimaji laini za simu ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, alisema linafanyika kwa awamu ili kuondoa usumbufu na kwamba walikuwa wamezima laini 975,041.

Alisema kundi la kwanza waliozimiwa laini zao ni watu 656,091 ambao wana vitambulisho vya Taifa au Namba lakini hawajasajili laini zao.

Alisema kundi la pili la watu 318,950 waliosajili laini zao kwa kitambulisho cha Taifa kabla ya kuanza mfumo wa kusajili kwa alama za vidole.



Upanuzi wa barabara ya Morogoro kwa njia sita ukiendelea vizuri, huku kukiwa na mabadiliko kwa baadhi ya maeneo ikiwamo ujenzi wa daraja eneo la Kibamba, wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. Daraja hilo litatumiwa na watembea kwa miguu. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Wakazi 600 waliozingirwa na mafuriko waokolewa

**Na Said Hamdani, LINDI**

WAKAZI zaidi ya 600 kutoka vijiji vitano Wilayani Kilwa mkoani Lindi waliokuwa wamezingirwa na mafuriko, wameokolewa.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilwa, Renatus Mchau, alisema waliokolewa baada ya kupelekewa boti tano.

"Wananchi hao ni kutoka vijiji vya Makangasa, Kipindimbi, Njinjo, Kikole na Mitole," alisema Mchau.

Aliongeza kuwa kazi ya uokoaji ilifanywa na wavuvi kutoka miji midogo ya Kivinje, Masoko kwa kushirikiana na watu wenye uzoefu wa kuogelea.

Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, wamelazimika kupeleka boti tano aina ya 'faiba' kutoka Kivinje.

Alisema mafuriko hayo yamesababisha mashamba na vitu mbalimbali yakiwamo magodolo, vitanda na mifugo kama mbuzi, vimesombwa na maji yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Lindi.

Alisema kutokana na tatizo hilo, uongozi wa serikali Wilaya ya Kilwa na Mkoa wamelazimika kuomba msaada wa watendaji kutoka Dar es Salaam kwenda kusaidia kazi ya uokoaji.

Aliongeza kuwa wameshawapeleka kiasi kidogo cha chakula kwa ajili ya kuwasaidia waathirika hao.

# Magufuli ampa kibarua Simbachawene

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli amempa kibarua kizito Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, huku akimtaka asiingie katika mkumbo wa waliomtangulia kwa kufanya mambo ya ovyo.

Akizungumza jana katika hafla ya kuwaapisha mawaziri wapya aliowateua wiki iliyopita pamoja na mabalozi watatu aliloteuliwa kuwakilisha Tanzania nje ya nchi, Rais pia alimtaka Simbachawene kushughulikia dosari zilizoko katika hiyo ikiwamo kuwaondoa viongozi na watendaji ambao ni kikwazo katika ufanisi wa wizara .

Sambamba na hilo, alimtaka kushughulikia makubaliano yaliyotiwa saini na viongozi wakuu wa wizara waliopita kuhusu mkataba wa ununuzi wa vifaa vya zimamoto vyenye thamani ya zaidi ya Sh. Trilioni moja katika mazingira yasiyo na uadilifu na bila kujali maslahi ya taifa.

Unakwenda kwenye wizara yenye mapepo. "Sasa hayo mapepo yasikuingie. Kawe mkali, kasimamie na mimi najua utaweza na saa nyingine ukamtangulize Mungu. Lakini ukifika pale yale yanayohitaji kubadilishwa, yabadilishe, kama kuna watendaji ukiona hawafai, watoe. Wanaohitaji kuwa 'demoted' (kushushwa cheo) wa-'demote' ili utendaji kazi wa wizara hii uende vizuri," alisema Rais Magufuli.

Pamoja na kumpa tahadhari hiyo, Rais Magufuli alisema anampeleka Simbachawene katika wizara ambayo ni ngumu lakini anaamini atafanya vizuri.

"Lakini ugumu utauleta wewe au utarahisisha wewe. Narudia kusema kwamba (Wizara ya) Mambo ya Ndani (ya Nchi) imehusika kwenye kashfa nyingi na wamekuwa wakiambiwa wajirekebishe. Mawaziri wote huwa nawaeleza, lakini sifahamu huwa pana mdudu gani pale. Nimeona nikupeleke wewe, nenda kayasimamie haya," alisisitiza.

Rais alisema watendaji katika wizara hiyo walikuwa na taarifa juu ya kile kilichokuwa kinaendelea kuhusu mkataba mbovu uliongiwa na Wizara hiyo lakini walinyamaza.

"Hili suala la kampuni waliloingia Memorandom of Understanding (makubaliano), tena haya ma-Document (nyaraka) nakupa wewe ukayasome. Nenda ukaanze na hili," alisema na kuongeza:

"Na nataka nikupe tu tahadhari, watendaji wako utakaowakuta si kwamba hawayajui, Naibu Waziri anayajua ingawaje hakuhusishwa sana. Alikuwa anapewa tu madokezo, na alipokuwa anayapata alinyamaza wakati angeweza hata akaja mapema serikalini akaeleza. Sasa sijui kwa nini alikaa kimya lakini hakuhusika sana."

"Naibu Katibu Mkuu alihusika sana, tangu kuanza kwake mpaka mwisho na una watendaji wengine kwenye Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wamehusika na ndio hao wengine walikuwa wakikaa kwenye vikao wanalipwa dola 500 ya kikao, dola 300 ya safari na wanapewa 'Laptop'. Sasa unaweza kujiuliza huyo mtu unaye-negotioate (anaye-

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Lipumba afunguka Polisi kumtia mbaroni

**Na Boniface Gideon, TANGA**



SIKU moja baada ya Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, kukamatwa na kuachiwa huru bila ya masharti yoyote, kiongozi huyo wa upinzani ameeleza na kufunguka mazito juu ya hatima ya siasa kwa vyama vya upinzani nchini.

Akizungumza na Nipashe, Prof. Lipumba alisema katika ziara yake aliyoifanya mkoani Tanga imepitia katika misukosuko mingi hususani vyombo vya dola ambavyo vilikuwa vinachagizwa na makada wa chama tawala na maofisa wa serikali.

Prof. Lipumba alisema amezunguka wilaya zote za Mkoa wa Tanga, na kuwa hakuna wilaya ambayo alifanya kikao cha ndani kwa uhuru.

"Polisi wanatumia nguvu kubwa kutudhibiti tusifanye vikao vya ndani, wanakuja na magari mengi na silaha za moto utadhani wanakwenda kukabiliana na majambazi, kumbe ni raia wema," alisema Lipumba.

Aliongeza: "Shughuli za kisiasa zipo kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi, lakini walituambia vikao vya ndani vifanyike...sisi tumekubali kutokufanya mikutano, lakini mbona wanatuzuia na kutumia nguvu kubwa kutudhibiti?" Alihoji Lipumba.

**AZUNGUMZIA SAKATA LA KUTIWA MBARONI HANDENI**

Akizungumzia suala la kukamatwa na kuachiwa huru huko wilayani Handeni Prof. Lipumba alisema alikuwa kwenye kikao cha ndani katika moja ya nyumba ya mwanachama wake ghafla walishangaa maofisa wa polisi wakiingia na kuwapeleka kituo cha polisi Wilaya ya Handeni.

Aliongeza kuwa baada ya kupelekwa kituo cha polisi kwa ajili ya taratibu nyingine za kisheria alimwita mwanasheria ;"Baada yakuja mwanasheria wangu alikaa na Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Handeni na baada ya kupitia taratibu zote za kisheria wakabaini kuwa sijakiuka taratibu za vikao na mikutano ndipo waliponiachia huru bila masharti ya dhamana," alisema Lipumba.

Akielezea mikakati ya chama chake Prof. Lipumba alisema ataendelea na harakati za siasa kwani wanazuiwa ili kukatishwa tamaa kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika baadaye mwaka huu.

"Sisi tunafahamu hizi zote ni juhudi za kukatishana tamaa, lakini mwaka huu tutapambana nao mpaka nafasi ya Rais," alisema Lipumba.

Lipumba alisema nchi inapitia wakati mgumu katika mfumo wa demokrasia wa vyama vingi. "Tusikate tamaa hasa wanachama wangu tuendelee kupambana japo tunapitia katika wakati mgumu na wanasiasa wa vyama vya upinzani nchini nao wasikate tamaa," alisema Lipumba.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe, alisema sababu za kumkamata Prof. Lipumba ilikuwa ni kumkumbusha kuwa mikutano hairuhusiwi. "Tumemkumbusha tu kuwa mikutano hairuhusiwi mpaka muda utakapofika na tumekubaliana aendelee na vikao vya ndani na sio nje kwa hiyo anaendelea na shughuli zake kama kawaida," alisema Gondwe.

# Mganga wa kienyeji jela maisha kisa kubaka mtoto

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya Kigoma Mkoa wa Kigoma imemhukumu mganga wa kienyeji, Venas Edward (48), mkazi wa Ujiji Manispaa ya Kigoma/Ujiji kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kosa la kumnajisi mtoto wa kike mwenye umri wa miaka minane.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Katoki Mwakitalu, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Mwakitalu alisema katika kesi hiyo upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Raymond Kimbe, na ulipeleka mashahidi wanne na kielelezo kimoja ambacho ni PF3.

Alisema mama wa mtoto huyo alimpeleka mtoto wake nyumbani kwa mshtakiwa kwa ajili ya kutibiwa, na baada ya kumfikisha, mganga alimtuma mama huyo aende dukani kununua wembe.

Alisema baada ya mama kwenda dukani, mshtakiwa alimfanyia mtoto huyo kitendo hucho cha kikatili.

Alieleza kuwa baadaye mama wa mtoto huyo alifika kutoka dukani na kumchukua mtoto wake na kurudi nyumbani kwake.

Alieleza zaidi kuwa baada ya muda mama alisikia mtoto wake analalamika kusikia maumivu sehemu zake za siri, ndipo mama alipomkagua na kugundua kuwa mtoto wake alikuwa amenajisiwa.

Aliendelea kueleza kuwa mama wa mtoto huyo alimbana mtoto wake kwa kumuuliza ni nani aliyekufanyia kitendo hicho ndipo alimjibu kuwa ni mshtakiwa.

Mshtakiwa huyo baada ya kuhukumiwa kwenda jela maisha, aliangua kilio hadharani na kusababisha ndugu zake nao kuanza kuangua vilio mahakamani mbele ya umati uliofika mahakamani kwa ajili ya kusikiliza hukumu hiyo.

Awali akisoma hati ya mashtaka Wakili Kimbe alidai kuwa Aprili 23, mwaka 2019 majira ya asubuhi eneo la Kasoko Ujiji, mshtakiwa alinajisi mtoto huyo na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri.


## Blue Nile International Limited

BNIL

P.O.BOX: 11007,
Dar Es Salaam, Tanzania,
East Africa,
Ph: +255686312801
Email: info@trinity.ac.tz

## VACANCY ANNOUNCEMENT

An upcoming college in Arusha invites applications from suitable candidates with relevant qualifications and experience to apply for the following vacant positions to its Diploma and Certificate programmes in **CLINICAL MEDICINE, NURSING AND MIDWIFERY, MEDICAL LABOROTORY SCIENCE, PHARMACY and COMPUTER SCIENCE**.

**1. Tutors (16 Posts)**

**Qualifications:**

(i) Doctor of Medicine degree (4 posts)
(ii) Bachelor degree in Nursing and Midwifery (4 posts)
(iii) Bachelor degree in Medical Laboratory Sciences (4 posts)
(iv) Bachelor degree in Pharmaceutical Sciences (4 posts)

**Other conditions:**

(v) Successful candidates will join our new institute in Arusha (Kisongo) where they will be engaged with teaching Certificate and Diploma level courses;
(vi) The above positions are for qualified Tanzanian, registered and recognized by relevant professional bodies;
(vii) Candidates who previously underwent Diploma studies are highly encouraged to apply;
(viii) The Employer is equal opportunity sensitive and hence women are also encouraged to apply;
(ix) Senior applicants with leadership experience may be considered for managerial positions.

**2. Assistant Tutors (20 Posts)**

**Qualifications:**

(i) Diploma in Clinical Medicine (4 posts)
(ii) Diploma in Nursing and Midwifery (4 posts)
(iii) Diploma in Medical Laboratory Sciences (4 posts)
(iv) Diploma in Pharmaceutical Sciences (4 posts)
(v) Diploma in Computer Sciences or Computer Engineering or ICT(4 posts)

**Other conditions:**

(i) Successful candidates will join our new institute in Arusha (Kisongo) where they will be engaged with assisting in teaching Certificate and Diploma level courses;
(ii) The above positions are for qualified Tanzanian, registered and recognized by relevant professional bodies;
(iii) The Employer is equal opportunity sensitive and hence women are also encouraged to apply;

**Mode of applications:**

Qualifying candidates should to submit their applications accompanied with most recent passport sized-photograph, curriculum vitae, academic transcripts and copies of academic certificates with names of three referees together with their contact address and any other relevant document portraying their competence in the field. Interviews for shortlisted applicants will be arranged and the dates will be communicated to them

**Apply before 15th February 2020 by sending an email with relevant attachments to info@trinity.ac.tz**

215602702

# Viongozi wapya ACT-Wazalendo Machi

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kinatarajia kupata viongozi wapya ifikapo Machi, mwaka huu, baada ya jana kutangaza kuanza mchakato wa kutoa fomu kwa wanachama wake kuwania nafasi mbalimbali.

Akitangaza mchakato huo jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Katibu Mkuu wa chama hicho, Dorothy Semu, alisema uongozi uliopo sasa madarakani unamaliza muda wake Machi na kwamba nafasi zitakazogombewa ni Kiongozi wa Chama, Naibu Kiongozi na Mwenyekiti wa Chama Taifa.

Zingine ni Makamu Mwenyekiti-Tanzania Bara, Makamu Mwenyekiti-Zanzibar, Katibu Mkuu, wajumbe wa Halmashauri Kuu na wajumbe wa Kamati Kuu.

Semu alisema uchaguzi huo utahusisha pia nafasi za Ngome ya Wanawake ambazo ni Mwenyekiti wa Ngome, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Naibu Katibu, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa.

Alisema uchaguzi huo utahusu ngome ya vijana na nafasi zitakazogombewa ni Mwenyekiti wa Ngome, Makamu Mwenyekiti wa Ngome- Tanzania Bara, Makamu Mwenyekiti wa Ngome-Zanzibar, Katibu wa Ngome, Naibu Katibu wa Ngome, Wajumbe wa Halmashauri Kuu Taifa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa. Kadhalika, Semu alisema uchaguzi utahusu pia viongozi katika ngome ya wazee na nafasi zitakazogombewa ni Mwenyekiti wa Ngome, Makamu Mwenyekiti wa Ngome-Tanzania Bara, Makamu Mwenyekiti wa Ngome-Tanzania Bara, Makamu Mwenyekiti wa Ngome-Zanzibar, Katibu wa Ngome, Naibu Katibu wa Ngome, Wajumbe wa Halamashauri kuu Taifa, Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa.

"Kuchukua na kurejesha fomu kuanzia leo, uchaguzi wa ngome ya wazee utafanyika Machi 7, uchaguzi wa ngome ya vijana ni Machi 8, uchaguzi wa ngome ya wanawake ni Machi 9, na uchaguzi wa chama ni Machi 14," alisema Semu.

Alisema fomu zinapatikana ofisi ya Makao Makuu, Kijitonyama jijini Dar es Salaam, ofisi kuu iliyoko Vuga Zanzibar, Ofisi za ACT-Wazalendo katika mikoa yote.

Semu aliongeza kuwa fomu zitakazorejeshwa zinapaswa kuambatanishwa na stakabadhi ya malipo inayoonyesha namna yalivyofanyika.



Mkufunzi Mkuu kitengo cha huduma za viwanja vya ndege kutoka Chuo cha Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) Dar es Salaam, Thamarat Abeid, akitoa ufafanuzi wa fursa za kimasomo katika chuo hicho, kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Rugambwa na Ihungo za mkoani Kagera juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri apangua watumishi hospitali

**Na Futuna Seleman, MKURANGA**

SERIKALI imemwondoa Mfamasia wa Wilaya ya Mkuranga, Dk. Elly Mende, katika nafasi yake pamoja na Mfamasia wa Hospitali, Erdwin Clement kubaki kwenye nafasi zao za kawaida, baada ya kubainika kuna wizi mkubwa kwenye mfumo wa utoaji dawa za serikali.

Aidha, imewahamisha watumishi wengine akiwamo Katibu wa Hospitali hiyo, Money Goodluck, ili kuinusuru hospitali hiyo inayolalamikiwa na wananchi wengi wa Mkuranga katika utoaji wa baadhi ya huduma ikiwamo upatikanaji wa dawa.

Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndungulile, alitoa maamuzi na maelekezo hayo wilayani Mkuranga mkoani Pwani alipotembelea hospitali ya wilaya hiyo na kupata maelezo kwa wagonjwa namna wanavyohudumiwa na kutembelea wodi mbalimbali na chumba cha kuhifadhia dawa ambacho hakikuwa na kiyoyozi (AC).

Aidha, aliigiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo na Mkurugenzi Mtendaji, Mhandisi Mshamu Munde, kufuatilia kwa kina mfumo wa utoaji dawa na ikithibitika waliokuwa wanauhujumu mfumo huo kwa kuuchezea, wachukuliwe hatua za kisheria.

"Mkuranga mnatuangusha timu ya hospitali jitafakarini, naagiza mfamasia wa wilaya aondolewe kwenye nafasi yake abaki ya kawaida, mfamasia wa hospitali aondolewe... natoa onyo kwa mganga mkuu wa wilaya ajirekebishe, asiingilie majukumu ya mganga mkuu wa hospitali ya wilaya kila mtendaji awe na mipaka yake, katibu wa hospitali aondolewe," alisema Dk. Ndugulile.

Alitaja duka moja kubwa la dawa lililopo wilayani Mkuranga kuwa linahusika na wizi wa dawa za serikali, na kusisitiza kuwa mfumo unaotumika kuiba dawa serikali anaujua.

Pia alisema amebaini watumishi wote wa hospitali hiyo hawana vitambulisho na kwamba hilo nalo ni tatizo, hivyo, alitoa mwezi mmoja kwa mkurugenzi na watumishi wote wawe wamevaa vitambulisho kama ilivyo katika hospitali nyingine za serikali nchini.

Alishangazwa na kutokuwapo kwa huduma ya maabara na nyingine muhimu kwa afya za wananchi kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, wakati hospitali ikikusanya fedha za malipo ya papo kwa papo kutoka kwa wananchi na bima ya afya.

## Serikali yawatoa hofu Watanzania kuhusu ugonjwa wa corona

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imewataka Watanzania kuwa watulivu kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa homa ya corona uliotokea China, na kueleza kuwa hadi sasa hakuna Mtanzania yoyote aliyeathiriwa na maradhi hayo.

Hadi sasa ugonjwa huo ambao ulianzika katika Jiji la Wuhan nchini China umeshaua watu zaidi ya watu 80 na zaidi ya 2,000 wakiwa wameambukizwa.

Tangu kugundulika kwa ugonjwa huo, mamlaka ya China imesitisha safari za ndege kwa raia wake wanaotoa na kuingia nchini humo.

Akitoa ufafanuzi kuhusu Watanzania waishio nchini China, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliwataka wawe watulivu, makini na kupenda kuwa na subira ya kupata maelezo au maelekezo na ufafanuzi rasmi wa serikali.

"Watanzania tunaomba muwe na subira ya kupata maelezo au maelekezo na ufafanuzi rasmi wa serikali pale kunakotokea jambo badala ya kukimbilia kwenye mitandao na uvumi ili kuondoa kueneza hali ya taharuki kwa wananchi bila ya kuwa na uhakika," alisema Prof. Kabudi.

Alisema Tanzania ina wanafunzi takribani 4,000, na kwamba katika mji wa Wuhan wapo 400.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, amehakikishia serikali kuwa mpaka sasa hakuna Mtanzania yoyote aliyeathiriwa ama kukumbwa na maradhi hayo.

Alisema Tanzania inaendelea kufuatilia kwa ukaribu kujua maendeleo na hali za Watanzania wanaoishi jimboni Wuhan na China kwa ujumla.

Prof. Kabudi aliwataka Watanzania kuwa makini na suala la kutoa taarifa zisizo rasmi au za uvumi kwa sababu kwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

**WATALII 500 WAKWAMA KUJA**

Wakati huohuo, mlipuko wa ugonjwa huo umesababisha kusitishwa kwa safari ya watalii zaidi ya 500 waliotarajiwa kuja nchini katika kipindi cha Februari na Machi mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania(TTB), Jaji mstaafu, Thomas Mihayo, alisema watalii hao walitarajiwa kuingia nchini Februari 24 na Machi 2 mwaka huu na ndege za Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL).

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075 ,

Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12.2019

**Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 12/31/2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka iliopita |
|---|---|---|---|
| | | 31/12/2019 | 30/9/2019 |
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 485 | 606 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 224 | 202 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 1 539 | 2 500 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 10 419 | 9 419 |
| 12 | Mali nyingine | 2 316 | 1 785 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 425 | 457 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **15 409** | **14 969** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 14 185 | 13 432 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 3 | 205 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 78 | 95 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Ba | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 65 | 375 |
| 28 | Madeni | 3 128 | 3 125 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **17 462** | **17 235** |
| 30 | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **(2 053)** | **(2 266)** |
| | | | |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 3 164 | 3 162 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5 831) | (5 831) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 504 | 292 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 111 | 111 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **(2 053)** | **(2 266)** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 0 | 0 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1017 | 1265 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2382 | 3221 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | -13.32% | -13.15% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 7.94% | 10.01% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 73.45% | 70.13% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 67.62% | 62.93% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 77.61% | 79.63% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 5.61% | 8.50% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.94% | -23.12% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZ KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) | Limbikizo lamwaka sasa | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 12/31/19 | 12/31/18 | 12/31/19 | 12/31/18 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1 002 | 304 | 3 331 | 3 342 |
| 2 | Gharama za Riba | 168 | 50 | 699 | 752 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 834 | 254 | 2 632 | 2 589 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 10 | 20 | 99 | 513 |
| | | | | | |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **209** | **103** | **880** | **1 147** |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 147 | 32 | 543 | 471 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 63 | 71 | 337 | 676 |
| 7 | **Gharma Zisizo za Riba:** | **822** | **260** | **2 909** | **3 223** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 306 | 38 | 1 133 | 1 493 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 110 | 4 | 283 | 225 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 407 | 217 | 1 493 | 1 505 |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **211** | **77** | **504** | **1** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **211** | **77** | **504** | **1** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **211** | **77** | **504** | **1** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 60 | 53 | 60 | 53 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 26 | 9 | 62 | 55 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 1.39% | 0.40% | 3.32% | 0.00% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | -9.79% | 26.05% | -23.32% | 0.01% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 67.87% | 63.84% | 69.09% | 71.80% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 4.66% | 1.23% | 14.69% | 5.37% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho**

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2019

| | Mtaji wa hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la zaidi ya jumla | Mengineyo Bainisha | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **3 164** | **-** | **(5 619)** | **2 363** | **68** | **(6)** | **(30)** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 504 | - | - | - | **504** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | (2 363) | - | - | **(2 363)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | 19 | (206) | **(187)** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 24 | **24** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **3 164** | **-** | **(5 115)** | **-** | **87** | **(188)** | **(2 053)** |

| | Mtaji wa hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la zaidi ya jumla | Mengineyo Bainisha | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **2 039** | **623** | **706** | **505** | **88** | **22** | **3 983** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 1 | - | - | - | **1** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1 858) | 1 858 | - | - | **-** |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (4 120) | - | (20) | - | **(4 140)** |
| Mengineyo | - | - | (348) | - | - | (28) | **(376)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **2 039** | **623** | **(5 619)** | **2 363** | **68** | **(6)** | **(532)** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 .12. 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka yasasa | Robo ya Mwaka iliyopita |
|---|---|---|---|
| | | 31/12/2019 | 30/9/2019 |
| | | | |
| | | | |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 211 | 128 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | Hasara Katika Mali | 57 | 61 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1 000) | 2 656 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 551 | 1 053 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (327) | 104 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (531) | 2 010 |
| | Kodi Iliyolipwa | (25) | (8) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli** | **(1 064)** | **6 004** |
| | **Zauendeshaji** | | |
| | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana** | | |
| | **na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | 0 | -9 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | 0 | 0 |
| | Mengineyo ( bainisha) | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa** | **-** | **(9)** |
| | **(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | | |
| | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 3 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 2 | 0 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | (5 264) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | **5** | **(5 264)** |
| | **Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | | |
| | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | 0 | 0 |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | (1 059) | 192 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 3 308 | 3 116 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **2 249** | **3 308** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 12/31/19**

Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina Na Cheo* | | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| **Philipo Raymond** ……………………… **Meneja mkuu** | **(Imesainiwa)** | | **1/28/20** |
| **Kelvin Mushi** ……………………………… **Mkuu wa kitengo cha fedha na utawala** | **(Imesainiwa)** | | **1/28/20** |
| **Hilda Valerian**…………………………… **Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | **(Imesainiwa)** | | **1/28/20** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi

| **Jina** | | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Pro. Dominicus Kasilo ……………………… Mkurugenzi | (Imesainiwa) | **28/1/2020** |
| Ernest Usangira …………………………….. Mkurugenzi | (Imesainiwa) | **28/1/2020** |

### MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Savings Account** | | | |
| | | **Companies, Institutions etc.** | **Private Individuals** | **Employees** |
| | | **TZS** | **TZS** | **TZS** |
| | **Bank Statement** | 1 500.00 | 1 500.00 | 1 500.00 |
| | **Opening Account** | 50 000.00 | 5 000.00 | 5 000.00 |
| | **Dormant Account** | 3 000.00 | 3 000.00 | 3 000.00 |
| | **Closing Account** | 2 000.00 | 2 000.00 | 2 000.00 |
| | **Certicate of Balance** | 10 000.00 | 10 000.00 | 10 000.00 |
| | **Interest Rate** | 4% | 4% | 4% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | **Loans** | | |
| | **Loan Product** | **Interest Rate** | **Remarks** |
| | Individual business Loan | 2.0% | Per Month |
| | Group Loans | 2.5% | Per Month |
| | Employees loans (Full guarantee) | 1.2% | Per Month |
| | Employees loans (Partial guarantee) | 2.0% | Per Month |
| | Saccos Loan | 1.2% | Per Month |
| | Loan Administration fee | 2.0% | |
| | Loan Application Fee | TZS 10000 | |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | **General** | **TZS** |
| | ATM Cards | 15 000.00 |
| | Replacement of lost Bank Card/ATM | 15 000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | **Payment Services** | |
| | **Cheque clearing charges (Processing)** | **Amount/%** |
| | NMB (Mafinga branch) | 1 000.00 |
| | Cheque of other banks | 15 000.00 |
| | Cash Withdraw above 5,000,000. | 0.05% |
| | Cash Withdraw | 500.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | **Money Transfers** | **Rate** |
| | To and From Dsm | 0.3% |
| | Western Union Local | 2.0% |

215601202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hujuma machinjio Dodoma inawanyong'onyeza wafugaji

**HATUA** iliyotangazwa na Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ya kuagiza kukamatwa na kuchunguzwa pamoja na kuchukuliwa hatua dhidi ya wahusika waliochelewesha na kukwamisha ujenzi wa machinjio na viwanda vya kuzalisha nyama imeonyesha kwa mara nyingine jinsi ambavyo ubadhirifu ulivyoumiza uchumi wa nchi.

Agizo hilo japo linakuja baada ya kuchelewa kwa karibu miaka 10 lakini ukweli ni kwamba kukwamisha ujenzi wa machinjio na mipango ya uzalishaji wa nyama ni tatizo linalowaachia makovu Watanzania hata leo.

Ikumbukwe kuwa ukosefu wa machinjio umeligharimu taifa hasa kudhuru afya za wateja wa nyama kutokana na kula nyama za viwango duni zenye madhara, magonjwa kama kifua kikuu (TB), homa ya matumbo na hata kimeta.

Pamoja na magonjwa hayo ukosefu wa machinjio umeuangusha uchumi wa nchi kutokana na kukosekana kwa mapato yanayotokana na sekta ya nyama kwa vile kitoweo hakikuwa na viwango kutokana na kukosa machinjio ya kisasa na pia kuandaliwa katika mazingira mabovu yanayowafanya wateja wa kimataifa kukimbia soko la Tanzania.

Yote hayo yaliwapeleka wanunuzi wa kimataifa na hoteli za kitalii kukimbilia mataifa jirani na kuneemesha uchumi wake huko soko la nyama la Tanzania likihudumia wateja wa ndani pekee na kuendelea kulaumiwa kuwa lilikuwa na nyama 'chafu'.

Viongozi hao wanaotakiwa kuchunguzwa ni watendaji wa Wizara ya Kilimo na Mifugo waliokuwapo madarakani kati ya mwaka 2008 na 2015 kwa madai ya kushirikiana na kampuni ya nyama ya Nicol na Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) na kudaiwa kuwa walichota takribani Sh. bilioni 15 zilizokuwa zimelengwa kuboresha machinjio ya Dodoma .

Haipendezi kuendelea kusikia kashfa kama hizo , kwani madai ya uhujumu wa fedha za umma na ufujaji mali za Watanzania umesababisha mkwamo wa uchumi na umaskini unaotokana na kufungwa kwa viwanda na kuchangia ukosefu mkubwa wa ajira.

Lakini, ni jambo linalowaumiza Watanzania wengi kuona kuwa ni taifa la pili kwa idadi kubwa ya mifugo Afrika hasa ng'ombe ambao wanakaribia milioni 30 sasa, lakini hakuna manufaa makubwa yanayoonekana.

Aidha, inasikitisha kwamba sekta ya mifugo imeshindwa kuwainua Watanzania na kuwaweka kwenye ramani ya dunia kutokana na ukweli kuwa baada ya Ethiopia nchi yenye mifugo mingi ni taifa hili.

Hivyo, tunaendelea kuungana na Kamati ya Bunge kutaka uchunguzi ufanyike kwa sababu ukosefu wa machinjio bora na ya kisasa umesababisha uchinjaji nyama kiholela mitaani na hata wizi wa mifugo iliyochinjwa na kuuzwa kinyemela kwenye baa, hotelini na hata machinjioni.


Inasikitisha kuona kuwa pamoja na kwamba serikali imetenga fedha na kuweka mikakati ya kusimamia sekta hiyo ili inufaishe nchi, lakini hakuna kilichofanyika hasa kwenye sekta ya nyama.

Tunashauri kuwa kilichofanywa na Kamati ya Bunge, kimulike pia miradi ya ujenzi wa machinjio katika jiji la Dar es Salaam na miji mingine ambayo kwa miaka mingi umekwama.

Miradi hiyo ni pamoja na ile inayoelezwa kuwa ililenga kujenga machinjio na viwanda vya nyama vya kisasa ambayo yatabadilisha sura ya kile kinachoendelea huko Vingunguti na Ukonga ili kuwalisha wananchi nyama safi na salama.

Lakini pia uchunguzi huo ulete ari mpya ya viongozi wa sekta ya mifugo na uvuvi kujitathmini na kujiangalia kwenye utendaji wao ili kuwa na sekta inayohudumia badala ya kuumiza Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mtindo huu nao ni moja ya maadui elimu ubora nchini

Na Sabato Kasika

**UTORO** shuleni kwa baadhi ya walimu, unachangia kukwamisha lengo namba nne la maendeleo endelevu linalohusu elimu. Hivyo, ni vyema kuendelea kudhibitiwa kwa nguvu zote.

Hadi ifakapo mwaka 2030, kunatakiwa kuwapo elimu bora, usawa na fursa kwa wote kujiendeleza zaidi. Ni vyema kusema, kuna haja ya walimu kujituma zaidi katika ufundishaji na wazazi kutoa ushirikiano.

Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), linasema elimu ni kati ya haki msingi za binadamu. Ni sehemu ya mafao ya wengi na inawajibisha jamii nzima.

Kutokana na umuhimu wa elimu katika jamii, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, liliazimia kuanzishwa Siku ya Elimu Duniani, inayosherehekewa kila Januari 24 ya kila mwaka.

Lengo la Umoja wa Mataifa ni kubainisha na kuendeleza dhamana ya elimu kama sehemu ya mchakato wa maendeleo endelevu na fungamani ya binadamu, kiutu na kijamii.

Nchini Tanzania, serikali imeamua kuvalia njuga suala la elimu kwa kuanzisha kampeni za kuhamasisha jamii kuelewa umuhimu wa elimu kwa kuacha kuwatumikisha watoto, badala yake wapelekwe shule.

Hata hivyo, kampeni hizo zinaweza zisizae matunda kama mtindo wa utoro wa walimu hautapatiwa dawa ya kudumu, kutokana na ukweli kwamba baadhi yao wanatuhumiwa kwa utoro.

Haishii katika utoro tu, bali hata mtindo wa wanafunzi kujihusisha na mapenzi, hali ambayo kwa namna moja au nyingine inashusha kiwango cha elimu kwa wanafunzi.

Kwa mfano miezi, ni kadhaa iliyopita walimu 4,046 wa shule za msingi na sekondari wamefukuzwa kazi kutokana na makosa mbalimbali, yakiwamo utoro kazini, kukiuka maadili na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi.

Ni tamko la Katibu Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Winifrida Rutaindurwa, katika mkutano wa kuwajengea uwezo Makatibu Wasaidizi wa TSC toka wilaya zote za Tanzania Bara.

Anasema, walimu wengi walikutwa na makosa ya utoro wakati wa kuhakiki watumishi, kwanini waliondoka katika vituo vya kazi bila yaa kufuata taratibu na kuruhusiwa na waajiri wao, hivyo walichukuliwa hatua za kinidhamu.

Lakini pamoja na hayo, itoshe kusema utoro na mambo mengine yasiyo na maadili, ni moja wa maadui wakubwa wa maendeleo ya elimu kwa wanafunzi, hivyo walimu watimize wajibu wao.

Ikumbukwe kuwa, bado kuna uhaba mkubwa walimu kwenye shule za umma, sasa baadhi yao wanapojihusisha na vitendo vinavyosababisha wafukuzwe kazi, maana yake wanazidi kuongeza uhaba wa walimu.

Serikali inakiri kwamba, haijivunii kuwafukuza kazi walimu wake iliyowaajiri yenyewe ikizingatiwa kuwa, bado kuna upungufu wa walimu katika maeneo mbalimbali nchini.

Sasa kuna masikitiko ya kuwafukuza kazi idadi kubwa ya walimu, pia inakumbusha kuwa haina huruma na watumishi wazembe wasiozingatia maadili na miiko ya kazi yao.

Ni vyema kukumbushana, kwamba ualimu ni wito na mhusika anatakiwa kujituma. Bila ya kuwapo wito wa kazi hiyo, mara nyingi ufanisi wake unakuwa ni mdogo.

Inawezekana wapo baadhi ya watu wanafanya kazi ya ualimu ambayo siyo wito wao, bali kwa sababu tu wameajiriwa katika eneo hilo, hiyo, mwisho wake wanaangukia kushindwa kutumiza wajibu inavyotakiwa.

Huenda ndiyo hao ambao miaka ya nyuma walikuwa hawafundishi na kubaki wakifanya biashara ndogo, wakiacha vipindi na kusababisha wanafunzi wakose masomo.

Serikali imefanikiwa kudhibiti hilo kwa kupiga marufuku walimu kufanya biashara hiyo shuleni, lakini likaibuka tatizo lingine la utoro na mahusiano ya kimapenzi kati ya walimu na wanafunzi wao.

Yote ni hatari kwa maendeleo ya elimu kwa mwanafunzi. Ni vyema walimu wakatimiza wajibu wao inavyotakiwa kwa kuzingatia maadili ya kazi, badala ya kuchanganya na mengine ya ovyo.

Walimu ni walezi, wana jukumu la kuwalea wanafunzi, katika maadili mema yatakayowajenga vyema kwa kushirikiana na wazazi, lakini yanapojitokeza mambo ya utoro na kushiriki mapenzi na wanafunzi, ni tatizo katika elimu.

# Mgogoro kiwanda, hifadhi kufikia tamati

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imeahidi kuutafutia ufumbuzi mgogoro baina ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani na Kiwanda cha Chumvi cha Seasalt Ltd kilichoko ndani ya hifadhi hiyo, Bagamoyo mkoani Pwani.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alipokuwa akizungumza na mwekezaji wa kiwanda hicho pamoja na menejimenti ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan, katika kikao kilichofanyika kwenye hifadhi hiyo.

Awali mwekezaji wa kiwanda hicho, Ajar Sengar, alisema chanzo cha mgogoro huo ni tozo ya magari yanafika katika kiwanda hicho kubeba chumvi.

Kwa mujibu wa mwekezaji huyo, kiwanda hicho kiko ndani ya hifadhi, hivyo magari makubwa yanayokwenda kubeba chumvi hulazimika kulipia tozo ya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) za Sh. 200,000 kwa kila gari ili kuingia katika hifadhi hiyo.

Alisema hali hiyo inasababisha chumvi inayozalishwa katika kiwanda hicho kuuzwa kwa bei ya juu kulinganisha na inayozalishwa katika maeneo mengine, hivyo amekuwa hapati faida.

Mmiliki huyo alisema akiwa mwekezaji anayelipa kodi serikalini, anaona kuwa tozo hiyo si sawa kwa vile kiwanda hicho alibinafsishiwa na serikali, hivyo wateja wake hawatakiwi kulipa tozo hiyo.

Mbali ya tozo hiyo, alisema mgogoro wa mpaka kati ya hifadhi na kiwanda umekuwa ukiongezeka kwa kuwa kila akitaka kujitanua anakutana na vigingi (beacons) vilivyowekwa na Tanapa, hali inayosababisha kushindwa kuzalisha zaidi.

Kwa mujibu wa ramani, kiwanda hicho kiko ndani ya hifadhi, huku wawekezaji wake akidai hakiko ndani ya hifadhi.

Pia alisema tatizo lingine ni wakati wa kuomba vibali vya watumishi wakiwamo watumishi wa kigeni ambapo kila anapotuma maombi, majibu yake yamekuwa yakichelewa kutolewa hivyo kulazimika kuingia ndani ya hifadhi.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Kanyasu alisema kuna haja ya kulifanyia kazi jambo hilo kwa vile kiwanda hicho kimeajiri watumishi 2,000.

Alisema wawekezaji wanahitajika na uhifadhi unahitajika pia kwa ajili ya maendeleo ya taifa, hivyo lazima serikali ije na suluhu huku akisema busara haina budi kutawala katika kufikia mwisho wa suala hilo.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa mwekezaji wa kiwanda cha chumvi cha Seasalt Ltd, Ajar Sengar (kulia), kuhusu mpaka kati ya kiwanda hicho na Hifadhi ya Taifa ya Saadani, katika Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani jana, baada ya kutembelea mashamba ya chumvi ya kiwanda hicho, ambacho kwa mujibu wa ramani kinaonekana chote kipo ndani ya hifadhi hiyo. Wengine ni wajumbe wa menejimenti ya hifadhi hiyo. **PICHA: WMU**

# Kesi ya Kabendera yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

KESI ya uhujumu uchumi inayomkabili Mwandishi wa Habari za Uchunguzi, Erick Kabendera, imepigwa kalenda mpaka Februari 10, mwaka huu itakapotajwa baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa upelelezi bado haujakamilika.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali, Gloria Mwenda, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi bado haujakamilika na mchakato bado unaendelea.

Kutokana na madai hayo, Hakimu Mtega alisema kesi hiyo itatajwa Februari 10, mwaka huu, itakapotajwa na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Kabendera anadaiwa kupanga na kushirikiana na genge la uhalifu na shtaka la tatu ni la kukwepa kodi zaidi ya Sh. milioni 173.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa siku na mahali pasipofahamika mshtakiwa alijihusisha na genge la uhalifu.

Alidai kuwa katika tarehe tofauti tofauti kati ya Januari, 2015 na Julai, mwaka jana, alitenda kosa la kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia maslahi.

Katika shtaka la pili, Kabendera anadaiwa kuwa anakabiliwa na shtaka la ukwepaji kodi zaidi ya Sh. 173,247,047.02.

Kabendera anadaiwa kuwa katika tarehe tofauti tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 19, mwaka jana, alishindwa kulipa kodi kiasi cha Sh. 173,247,047,02.

Katika shtaka la tatu, Kabendera anadaiwa, kati ya Januari 2015 na Julai 2019, katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, mshtakiwa alitakatisha fedha Sh. 173,247,047.02.

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAHADHARI KWA UMMA

NDUGU WATANZANIA;

KAMA MNAVYOFAHAMU, LAINI ZA SIMU AMBAZO HAZIJASAJILIWA KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA **(NIN)** NA KUTHIBITISHWA KWA ALAMA ZA VIDOLE ZILIANZA KUZIMWA TAREHE 20 JANUARI, 2020 USIKU NA **ZOEZI LINAENDELEA.**

**HAKIKI TENA USAJILI WA LAINI ZAKO KWA KUPIGA NAMBA *106# NA UCHUKUE HATUA STAHIKI SASA.**

1.0 KWA WALIOSITISHIWA HUDUMA ZA LAINI ZAO ZA SIMU KUANZIA TAREHE 20.01.2020 WANAWEZA PIA KUENDELEA NA UTARATIBU WA USAJILI KWA LENGO LA AMA KURUDISHA LAINI ZAO ZILIZOFUNGWA KAMA ZITAKUWA BADO ZIPO AU KUPATA LAINI MPYA. **ZOEZI HILI NI ENDELEVU.**

2.0 KWA WATUMIAJI/WAOMBAJI **(WATANZANIA)** WAPYA WA LAINI ZA SIMU WATAENDELEA KUSAJILIWA MUDA WOTE KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA NA KUTHIBITISHA KWA ALAMA ZA VIDOLE. **HUDUMA HIYO NI ENDELEVU PIA.**

3.0 MATUMIZI SAHIHI YA VITAMBULISHO WAKATI WA USAJILI WA LAINI ZA SIMU(ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE)UKO KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO: -

3.1 Sisi wa-**Tanzania** kitambulisho chetu ni kile cha Taifa kitolewacho na NIDA kwa vigezo vyao;

3.2 Kwa wageni wanaokaa hapa nchini **chini ya miezi sita** wanasajili laini za simu kwa kutumia namba za Hati zao za kusafiria na kuthibitisha kwa alama za vidole;

3.3 Kwa wageni wanaokaa **zaidi miezi sita** wanatumia vitambulisho ***(Legal Resident ID)*** ambavyo hupewa na NIDA (Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa idara ya Uhamiaji na NIDA);

3.4 Kwa wanadiplomasia wanatumia Hati zao za kusafiria pamoja na vitambulisho vyao vinavyotolewa na Wizara ya Mambo ya nje; na

3.5 Kwa wakimbizi wanatumia vitambulisho vyao ambavyo hutolewa na NIDA ***(Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa idara ya Uhamiaji na NIDA),***

4.0 KATIKA KUJIRIDHISHA KUWA WALIOSAJILI LAINI ZAO ZA SIMU WAMETUMIA VITAMBULISHO SAHIHI, TCRA KWA KUSHIRIKIANA NA WATOA HUDUMA ITAFANYA ZOEZI LA KUHAKIKI LAINI ZOTE ZITAKAZOKUWA ZIMESAJILIWA ILI KUWAONDOA WALE WALIOSAJILI LAINI ZAO AMA KWA KUTUMIA VITAMBULISHO VYA WATU WENGINE AU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO TOFAUTI SAMBAMBA NA KUWACHUKULIA HATUA ZA KISHERIA.

5.0 IKUMBUKWE PIA KWAMBA KUSAJILI LAINI YA SIMU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA MTU MWINGINE NI KOSA SANJARI NA KUPEWA LAINI ILIYOSAJILIWA NA MTU MWINGINE.

6.0 **ONYO NA TAHADHARI ZINAENDELEA KUTOLEWA KWA MAKUNDI YOTE YALIYOORODHESHWA KWENYE KIPENGELE CHA 3.0 HAPO JUU, KUTOTUMIA KITAMBULISHO KISICHOKUHUSU WAKATI UNASAJILI LAINI ZAKO ZA SIMU** (ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE).

**ImetolewanaMkurugenziMkuu**
**MamlakayaMawasiliano Tanzania (TCRA)**
**24Januari, 2020**

215600102

# Bunge kujadili taarifa za kamati za kudumu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MKUTANO wa 18 wa Bunge unaanza leo ukiwa ni mahsusi kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za mwaka za Kamati za Kudumu za Bunge.

Sambamba na hilo, Bunge leo litakabidhi majoho kwa maspika wastaafu ikiwa ni kutambua utendaji kazi wao walipokuwa wakiendesha shughuli za bunge.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema Kamati hizo 15 zitawasilisha taarifa za Mwaka za kazi kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge.

Alitaja Kamati hizo kuwa ni ya Hesabu za Serikali(PAC), Hesabu za Serikali za Mitaa(LAAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Pia, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii,Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Nyingine ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Kuhusu kukabidhi majoho, alisema kutakuwa na shughuli ya kukabidhi majoho kwa Maspika Wastaafu ambao ni Pius Msekwa, Marehemu Samuel Sitta ambapo Joho alilotumia litapokelewa na Mke wake Margaret Simwanza Sitta kwa niaba ya familia na Anne Makinda.

"Shughuli hii itafanyika katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa 18 wa Bunge tarehe 28 Januari, 2020 mara baada ya Kipindi cha Maswali,"alisema

Ndugai pia alisema katika mkutano huo wastani wa maswali 125 ya kawaida yanatarajiwa kuulizwa na wabunge na maswali 16 ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Kadhalika, alisema Bunge pia linatarajia kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa Mwaka 2019 na Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020.



Mmoja wa wavuvi wa mwalo wa Butuja, wilayani Ilemela, mkoani Mwanza, akivusha samaki katika mazingira yasiyo salama, jana, baada ya miundombinu ya mwalo huo, kuharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha. **HABARI UK. 9. PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## Magufuli ampa kibarua Simbachawene

INATOKA UK 2

fanya makubaliano) naye kwa nini akulipe, leo anakulipa, kesho hivyo hivyo na kesho kutwa anakulipa," alisema.

"Kwa akili za kawaida unaweza kuelewa hapa kuna kitu cha ajabu kinafanyika. Kama mnazungumza kwa nini akulipe, lakini watendaji wako hawakuliona hili mpaka ukatiwa saini mkataba, wakapelekwa nje, wakalipwa, vifaa vyenyewe vinavyohitajika ni vya ovyo. wanakwenda kununua drones (ndege zisizo na rubani), sasa sijui kama zitahusika kuzima moto, kwenye mkataba huo palikuwa na vitu vya ovyo".

Rais Magufuli alimtaka Simbachawene kutumia taaluma yake kutatua mkataba huo ambao ni mbovu. Kitaaluma, Simbachawene (pichani) ni mwanasheria.

Vilevile, Rais Magufuli alimhusia Simbachawene kutumia mbinu na siri iliyosababisha Naibu Waziri wa Wizara hiyo kufanya kazi kwa kipindi kirefu katika wizara hiyo.

Kadhalika, Rais Magufuli alimuagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu, kwenda kusimamia kwa usawa masuala ya muungano pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zinazohusu sekta hiyo.

Mbali na Simbachawene na Zungu, mabalozi walioapishwa ni Maimuna Tarishi ambaye anakuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Ofisi za Umoja wa Mataifa Geneva, Uswisi na Hussein Kattanga, Tokyo nchini Japan. Mwingine ni Profesa Kennedy Gastorn anayekuwa Mwakilishi wa Kudumu Ofisi za Umoja wa Mataifa, New York, Marekani.



# Upelelezi kesi ya kina Papa Msofe bado

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayowakabili wafanyabiashara wanne akiwamo Marijan Msofe (53) maarufu kama 'Papa Msofe' na Wakili wa Kujitegemea Mwesigwa Mhingo (36) dhidi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuratibu genge la uhalifu na kutakatisha Dola za Marekani 410,000 (sawa na Sh. milioni 943), umedai haujakamilika.

Mbali na Papa Msofe, Mhingo, washtakiwa wengine ni Wenceslaus Mtui (49), Josephine Haule (38) na Fadhili Mganga (61).

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi anayesikiliza usikilizwaji wa awali katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Elia Athanas, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa.

"Mheshimiwa sina taarifa halisi ya jalada la kesi tunaomba tarehe nyingine ili niweze kwenda kufuatilie limefikia wapi," alidai Athanas.

Upande wa utetezi uliomba mahakama ipange tarehe fupi kwa ajili ya kupata taarifa ya Jamhuri.

Hakimu Shaidi alisema kesi itatajwa tena baada ya siku 14, washtakiwa warudishwe mahabusu mpaka Februari 11, mwaka huu.

Awali Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya, aliwasomea washtakiwa mashtaka yao mahakamani hapo.

Komanya alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Desemba 2018 na Septemba, mwaka huu, washtakiwa wote kwa pamoja na wenzao ambao hawajakamatwa walifanya mpango wa kuongoza genge la uhalifu.

Katika shtaka la pili, kati ya Desemba 2018 na Septemba, mwaka huu, washtakiwa wote, mahali tofauti walitakatisha Dola za Marekani 300,000 (sawa na Sh. milioni 690) kutoka kwa Pascal Jean Camille.

Shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa siku ya tukio la pili, washtakiwa wakiwa na nia ovu walijipatia kwa njia ya udanganyifu Dola za Marekani 300,000 kutoka kwa Camille baada ya kumdanganya kuwa wangemuuzia kilo 200 za madini aina ya dhahabu na kuyasafirisha kwenda nchini Ureno huku wakijua si kweli.

Upande wa Jamhuri ulidai katika shtaka la nne, tarehe tofauti Desemba 2018 na Septemba, mwaka huu, washtakiwa walitakatisha Dola za Marekani 110,000 (sawa na Sh. milioni 253) kutoka kwa John Mahsson wakati wakijua ni zao la uhalifu.

Komanya alidai katika shtaka la tano, washtakiwa walijipatia Dola za Marekani 110,000 kutoka kwa Mahsson baada ya kumlaghai kwamba wangemuuzia kilo 20 za madini aina ya dhahabu na kuyasafirishа mpaka Ureno huku wakijua si kweli.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

# Wavuvi sasa waomba maboresho ya mwalo

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WAVUVI wa mwalo wa Butuja wilayani Ilemela mkoani Mwanza wameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kuwaboreshea miundombinu ya mwalo huo uliokumbwa na mafuriko tangu kuanza kwa mvua za masika.

Katibu wa BMU ya Butuja, Emmanuel Nyagwesi, alisema barabara haipitiki vizuri ya kumfikisha mtu mwaloni, maegesho ya mitumbwi yameharibika, huku mitumbwi ikipasuka na kwamba wanunuzi wa samaki wanakosa sehemu ya kukaa hivyo kuwapa wakati mgumu kutokana na kufanya kazi katika mazingira ambayo siyo rafiki.

Alisema mwalo huo usingekuwa na choo kizuri, kungekuwa na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu.

"Tulihitaji halmashauri kupitia ofisi ya mkurugenzi kuona sisi ni wadau wake, ambao ni walipakodi wazuri, kwa mwezi halmashauri inakusanya zaidi ya shilingi milioni kama mapato kutoka mwalo huu," alisema.

"Tunayo mitumbwi zaidi ya 100 na yote inalipa kodi, kuna tozo za mzani wa serikali wa kupima samaki na sisi basi tukumbukwe," alisema na kuongeza:

"Huyu mkurugenzi aje siku moja atutembelee aangalie mara moja atusaidie angalau barabara ipitike kirahisi, tujengewe sehemu ya kuuzia samaki pamoja na kuboreshewa miundombinu yote kwa ujumla."

Katibu wa Ushirika wa Butuja Saccos, Maneno Hamis na Mwenyekiti wa Mtaa wa Butuja, Kichonge Mwita, walisema changamoto walionayo ni maji ambayo yamewavamia na kuharibu miundombinu na kushusha kipato cha wananchi wanaofanya shughuli katika mwalo huo.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akipita katika madimbwi ya maji machafu yaliyopo nje ya Soko la Buguruni mwishoni mwa wiki, ambayo yamekuwa kero kwa watumiaji wa soko hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maabara upimaji wa ebola kujengwa Siha

**Na Mary Geofrey, SIHA**

HOSPITALI ya Magonjwa ya Kuambukiza ya Kibong'oto wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, imesema inajenga maabara ya kisasa ya magonjwa ambukizi, itakayofanya uchunguzi wa kina wa maambukizo ya virusi vikiwamo vya ebola.

Imeelezwa kuwa kukamalika kwa ujenzi huo kutarahisisha utoaji huduma katika Kanda ya Kaskazini na kuachana na utaratibu wa kupeleka sampuli kwenye maabara ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Donatus Tsere, aliyaeleza hayo juzi mkoani humo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mwendelezo wa ziara ya maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto walio kampeni maalum ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Lengo la kampeni hiyo ni kuangazia mafanikio ya miaka minne ya serikali ya awamu ya tano katika sekta ya afya.

Alisema ujenzi wa maabara hiyo ya daraja la tatu unatarajiwa kukamilika mwakani na kwamba itakuwa kubwa na ya kwanza kuwapo Kanda ya Kaskazini.

"Jengo la maabara hii litakuwa la ghorofa tatu na itakuwa na mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kupima virusi kwa uwezo wa daraja la tatu bila kutegemea tena kwenda kupima MNH kama tunavyofanya sasa. Pia, itakuwa na uwezo wa kupima virusi bila kuwa na tahadhari kubwa ya kupata maambukizo," alisema.

Aliongeza kuwa maabara hiyo itapima virusi vyote vya magonjwa ya kuambukiza na itakuwa na uwezo wa kubaini virusi kwa madaraja vikiwamo vya ebola ambavyo kwa sasa hawana mtambo wa kuvibaini.

Alisema gharama zote za ujenzi wa maabara hiyo ni Sh. bilioni nane na tayari awamu ya kwanza ya ujenzi huo umekamilika.

Akizungumzia kuhusu ugonjwa wa kifua kikuu (TB), kiongozi huyo wa hopsitali alisema asilimia kubwa ya wagonjwa wanatoka katika mgodi wa Mirerani mkoani Manyara.

Alisema kati ya watu 100,000 waliopo mgodini, 14,000 wanaugua TB na kwamba sababu za kuwapo kwa idadi kubwa ni mazingira ya kufanyia kazi yanayokuwa na hewa nzito na vumbi.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, alisema hospitali inatoa elimu ya kujikinga kwa wafanyakazi wa migodini na imenunua mashine za kisasa kubaini wagonjwa wakiwa katika hatua za awali na kupata majibu kwa muda mfupi.

Dk. Tsere alisema wanatoa huduma za upimaji katika mgodi huo na wagonjwa wanaobainika kuwa na maambukizo, wanawahi kuwapa matibabu ili kuepuka kuenea zaidi kwa ugonjwa huo.

Alisema wameboresha huduma za matibabu kwa wagonjwa wa TB, hivyo kufanya idadi ya wagonjwa wanaotibiwa kuongezeka kutoka 150 mwaka 2015 hadi 180 kwa sasa.

Alisifu hatua ya serikali kuhakikisha nchi inakuwa na vituo 145 vya kutolea huduma za upimaji wa TB, akieleza kuwa imesaidia kuwa na mwamko wa wagonjwa kujitokeza kupata matibabu.

# Mil. 190/- kwa mikopo vikundi 36

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Tabora imetoa mikopo ya jumla ya Sh. milioni 190 kwa vikundi 36.

Fedha hizo zimetolewa hadi kufikia Desemba mwaka jana ikiwa ni sehemu ya mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato yake ya ndani.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na mchumi wa Manispaa ya Tabora, Joseph Kashushura, wakati wa kikao maalumu cha kupitia makisio ya mapato na matumizi ya Bajeti wa Baraza la Madiwani ya Manispaa ya ya Tabora.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 115 zimetolewa kwa vikundi 23 vya kinamama, shilingi milioni 55 zimetolewa kwa vikundi tisa vya vijana na shilingi milioni 20 zimetolewa kwa vikundi vinne vya walemavu.

Katika hatua nyingine, Kashushura alisema kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imepeleka kiasi cha shilingi milioni 119.4 katika kata 19 ili kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kashushura amesema kuwa halmashauri hiyo imepokea jumla ya shilingi milioni 899.2 ambazo zimetumika katika ukarabati wa miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Kazima.

Alizitaja kazi zilizofanyika ni ukarabati wa vyumba 6 vilivyokuwa vimeungua, ukarabati wa bweni la wasichana na bweni la wavulana, ukarabati wa vyumba sita na ukarabati wa vyoo vya walimu na wanafunzi.

Kashushura aliongeza kazi nyingine ni ukarabati wa mfumo wa majitaka, ukarabati wa darasa la walemavu, ukarabati wa vyumba vya block 23, ukarabati wa maabara ya kemia, bailojia, fizikia, ukarabati wa

**Taarifa hiyo ilitolewa jana na mchumi wa Manispaa ya Tabora, Joseph Kashushura, wakati wa kikao maalumu cha kupitia makisio ya mapato na matumizi ya Bajeti wa Baraza la Madiwani ya Manispaa ya Tabora.**

# Dawa za kulevya zampeleka jela

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MAHAKAMA Kuu Zanzibar imemuhukumu mshtakiwa Anuar Maalim Said (37) mkazi wa Kipangani Wete kulipa faini ya Sh. 2,000,000 au kutumikia kifungo cha miaka miwili kwa kupatikana na makasha 42 ya dawa za kulevya.

Dawa za kulevya alizokutwa nazo ni aina ya mirungi yenye uzito wa kilo 14.76.

Jaji wa mahakama hiyo, Abdul-hakim Ameir Issa, alitoa hukumu hiyo baada ya kumaliza kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili na kuona kuwa mtuhumiwa huyo ana kesi ya kujibu.

Alisema kuwa mahakama ilisikiliza mashahidi sita akiwamo mchunguzi kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Fatma Iddi Rashid, alithibitisha baada ya uchunguzi kuwa kielelezo alichopewa ni dawa za kulevya aina ya mirungi.

Alieleza kuwa mashahidi wengine ni nahodha Abdalla Kombo na baharia Makame Faki Haji ambao waliithibitishia mahakama kuwa walimchukua mshtakiwa huyo Shimoni Kenya akiwa na boksi.

"Waliithibitishia mahakama kuwa walipokwenda kuuza pweza Shimoni Kenya, mshtakiwa huyo aliwaomba wamsaidie anakuja kwao Pemba na wakamchukua akiwa na boksi," alisema Jaji huyo.

Alieleza kuwa mashahidi wengine ni maofisa wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) Ali Seif Ali na Rajab Abdalla Suleiman ambao waliithibitishia mahakama kukabidhiwa mshtakiwa akiwa na boksi hilo kutoka kwa askari Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM).

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo, Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Ali Amour Makame, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Kabla ya mshtakiwa kusomewa hukumu, aliiomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kwani ana familia ambapo yeye ndie msimamizi.

Pamoja na maombi hayo ya mshtakiwa, Jaji alimhukumu kulipa faini ya Sh. 2,000,000 na akishindwa kulipa atatumikia kifungo cha miaka miwili jela.

Mshtakiwa alitenda kosa hilo Mei 5 mwaka 2019 katika Bandari ya Mawe Matatu Makangale Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.



Wanafunzi na baadhi ya watu wazima wakihangaikia usafiri wa kuelekea maeneo ya Mpiji Magohe, kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ambao mara nyingi huwa ni wa shida. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mawenzi wajivunia kumaliza vifo uzazi

**Na Mary Geofrey, MOSHI**

HOSPITALI ya Rufani ya mkoani Kilimanjaro, maarufu Mawenzi, inajivunia kudhibiti vifo vitokanavyo na uzazi katika kipindi cha miaka miwili iliyopita ambayo haikuwa na kifo cha mama.

Mafanikio hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Jumanne Karia, alipozungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika kampeni maalum ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Lengo la kampeni hiyo ni kuangazia mafanikio ya miaka nne ya serikali ya awamu ya tano katika sekta ya afya.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili, hakuna kifo cha mama kilichotokea kutokana na ubora wa huduma wanazotoa kuhakikisha mama na mtoto wanakuwa salama.

Alisema mwaka jana, wanawake 3,411 walijifungua na walirudi nyumbani wakiwa salama na wenye afya.

"Haya ni mafanikio tunajivunia kama hospitali kwa kuhakikisha tunapunguza na kumaliza vifo vitokanavyo na uzazi. Lengo ni kutoa huduma nzuri na kuwafanya kinamama kuona hii ni sehemu ya kuja kujifungulia," alisifu.

Alisema mafanikio hayo yametokana na kutoa huduma za mkoba katika vituo vya kutolea huduma za afya kwenye halmashauri mkoani humo.

Aliishukuru serikali kwa kuajiri watumishi wapya 40 wa kada mbalimbali kwa mwaka 2018/19 kwa ajili ya hospitali hiyo.

"Tunaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kuwaendeleza kitaaluma pamoja na kulipa stahiki mbalimbali za watumishi," alisema.

Alisema serikali pia inaendelea na ukamilishaji wa jengo jipya la mama na mtoto.

Alisema Sh. bilioni 1.7 zimetolewa na serikali kwa ajili ya hatua saba za ujenzi wake wote.

Sambamba na hilo alielezea mafanikio mengine wanayojivunia kuwa ni kufanya upasuaji wa kuondoa ukungu kwenye lenzi ya jicho kwa wagonjwa 640.

Alisema pia wamepandikiza kioo cha jicho na huduma ya mkoba kwa ajili ya kuondoa ukungu kwenye lenzi ya jicho kwa wagonjwa 430.

# NMB yapiga jeki shule, zahanati

**Na Mwandishi Wetu**

KERO ya kutembea umbali mrefu kwa wanafunzi zaidi ya 350, wakiwamo wasichana 169 wa kitongoji cha Misuna, Kijiji cha Ngimu wilayani Singida, imepatiwa ufumbuzi baada ya jamii kwa kushirikiana na benki ya NMB kujenga miundombinu ya vyumba vya madarasa.

Wananchi hao wameshirikiana na benki ya NMB kumaliza kero hiyo, kutokana na watoto wao kupata usumbufu wa kutembea mwendo mrefu kila siku kwenda shule, na kurudi nyumbani huku mchana kutwa wakilazimika kushinda na njaa.

Wakipokea msaada wa vifaa mbalimbali kutoka benki ya NMB, baadhi ya wananchi walisema kuwa kila siku watoto wao walilazimika kutembea mwendo wa kilomita tano kwenda shuleni na zingine tano kurudi nyumbani, hali iliyozorotesha taaluma yao.

Akikabidhi baadhi ya vifaa hivyo ikiwamo bati, mbao, nondo, misumari, makoa na waya kwa ajili ya ujenzi, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati yenye mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara; Nsolo Mlozi, alisema benki hiyo itaendelea kuunga mkono juhudi za wananchi.

"Benki ya NMB itaendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha changamoto zote zinazoikabili jamii zinatatuliwa, kipaumbele chetu ni kwenye sekta za elimu na afya...ombi langu ni kuwataka mfunge akaunti beki ya NMB ili baadaye turudishe faida kwenu," alisema.

Alifafanua kuwa, msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 20, kwa ajili ya shule mbili za msingi na zahanati mbili, ni mwendelezo wa benki hiyo katika kuhakikisha inarejesha faida inayopata, kwa jamii ili itumike kuleta maendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskasi Mlagiri, alisema msaada katika shule hiyo na mingine iliyotolewa kwenye Shule ya Msingi Msange, zahanati ya kijiji cha Mwakichenche na Mwachambia, ni chachu kwa jamii katika kujiletea maendeleo yao.

Hata hivyo, mkuu huyo wa wilaya aliwataka wananchi kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo yao, ikiwamo ujenzi wa matundu ya vyoo, vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, madawati na zahanati.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Eliya Dighah, kwa niaba ya wananchi wa wilaya hiyo, aliishukuru benki ya NMB kuwekeza kiwango kikubwa cha fedha za maendeleo katika halmashauri hiyo, hali inayojenga imani kwa jamii.

"Ni jambo la kuishukuru sana benki ya NMB kusaidia sekta ya elimu na afya katika wilaya yetu, hongereni sana na tunaomba msituchoke...miundombinu hii mnayotusaidia leo, imesaidia sana watoto wetu wafanye vizuri darasani," alisema.

## Mkurugenzi Jiji awafunda wafanyabiashara

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKURUGENZI wa Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, amewataka wafanyabiashara kutokubali kutumika kwa maslahi ya mtu binafsi kwa kuzusha uongo dhidi ya viongozi wa halmashauri hiyo.

Alitoa kauli hiyo jana kupitia taarifa yake kwa waandishi wa habari, iliyosomwa na Msimamizi wa Masoko wa Jiji, Mwita Nyarukururu.

Dk. Madeni alisema hivi karibuni kumezuka taarifa zinazosambaa kwa kasi kuwa jiji hilo linawatoza ushuru wajasiriamali wadogo wenye vitambulisho, kitu ambacho si kweli.

"Hatujawahi wala kuthubutu kuwatoza ushuru wafanyabiashara hawa isipokuwa wale wenye mikataba (wapangaji) na makubaliano mbalimbali kwenye miundombinu ya masoko ya jiji hili kama vizimba, vibanda, meza na maduka," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Madeni, wafanyabiashara wenye kero zao ni vyema wakaziwasilisha ofisi za jiji au ngazi ya wilaya na si vinginevyo.

Aidha, alisema maelekezo ya Rais John Magufuli aliyotoa kuwa wasiwatoze ushuru wajasiriamali, wanayazingatia na kuyaheshimu.

Dk. Madeni alisema wako baadhi yao wanaosubiri ziara za viongozi wa ngazi za juu ya wilaya, mkoa na taifa na kutoa kero zao jambo ambalo si sahihi.

**"Hatujawahi wala kuthubutu kuwatoza ushuru wafanyabiashara hawa isipokuwa wale wenye mikataba (wapangaji) na makubaliano mbalimbali kwenye miundombinu ya masoko ya jiji hili kama...**

# Watelekeza maduka kisa ukaguzi NEMC

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

BAADHI ya wafanyabiashara wa mifuko ya kubebea bidhaa katika soko la Kilombero jijini Arusha, wametelekeza maduka yao na kutokomea kusikojulikana, kukwepa msako unaoendeshwa na maofisa wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

NEMC Kanda ya Kaskazini imeanzisha operesheni ya kusaka mifuko mbadala isiyokidhi viwango.

Mkaguzi wa Mazingira wa NEMC, Kanda ya Kaskazini, Nancy Nyenga, alisema juzi kuwa wamebaini kuwapo mifuko ya plastiki na mifuko mbadala, ambayo haijathibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

"Wafanyabiashara wengi wanaendelea kuuza mifuko mbadala isiyokidhi viwango na ile ya plastiki jambo ambalo ni kinyume cha sheria," alisema.

Nyenga alisema mbali na mifuko hiyo kutothibitishwa na TBS, asilimia kubwa imeonekana haina nembo na iko chini ya viwango vinavyokubalika.

Alisema mifuko mbadala inayofaa kwa matumizi ya kubebea bidhaa, lazima iwe na uzito usiopungua gramu 70 ili kubeba bidhaa, lakini iwe imethibitishwa na TBS.

"Katika ukaguzi huu wa mifuko kwenye soko la Kilombero, tumekuta baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, wanaingiza na kuzalisha mifuko mbadala ambayo haikidhi vigezo," alisema.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Jiji la Arusha, Alani Lushokana, alisema operesheni hiyo ni endelevu na amewatahadharisha wasambazaji na wauzaji wa mifuko hiyo kufuata sheria za nchi.

Pia alisema kumekuwa na matumizi yasiokubalika ya mifuko laini inayotumika kubebea bidhaa na mifuko hiyo inapaswa kutumika kwa ajili ya vifungashio vya bidhaa maalum na si vinginevyo.

Alisema katika operesheni hiyo, ilikamatwa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na serikali ikiuzwa kinyemela na wauzaji walitoroka na kutelekeza maduka yao baada ya kuwaona maofisa hao.

"Pamoja na baadhi kutoroka lakini baadhi yao tuliwakamata wakiwa na mifuko hiyo na tuliwapiga faini kwa mujibu wa sheria," alisema.

Operesheni hiyo ilifanyika katika wilaya za Arusha na Longido katika eneo la Namanga mpakani mwa Tanzania na Kenya baada ya timu ya ukaguzi kubaini idadi kubwa ya mifuko isiofaa kwa matumizi inayotoka Kenya.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (wa pili kushoto), akizungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Maulid Madeni (kulia), alipotembelea eneo la wazi katika Mtaa wa Kaloleni jana, ambalo Mwenyekiti wa Mtaa huo, Abdallah Nasoro (wa pili kulia), aliliomba kwa ajili ya kujenga kiwanja kitakachotumika kwa kuchezea michezo zaidi ya kumi ikiwamo mpira wa kikapu na taikondo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Madiwani wakutana baada ya miezi sita

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

HATIMAYE Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, imeruhusu Baraza la Halmashauri ya Meru linaloongozwa na Mwenyekiti Willy Njau (Chadema), kuendelea na majukumu yake baada ya kusitishwa kwa miezi sita.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisitisha vikao vya baraza hilo Agosti 28, mwaka jana, kwa muda usiojulikana kutokana na kuwapo viashiria vya uvunjifu wa amani.

Ijumaa iliyopita, ikiwa ni siku ya kwanza ya kikao cha baraza hilo tangu lisitishwe, Mwenyekiti Njau alilazimika kuahirisha kikao hicho kwa saa tatu kuanzia saa sita mchana kutokana na baadhi ya madiwani kutoridhia kikao hicho kuwa cha mkutano wa mwaka.

Madiwani hao walidai kuwa tangu kusitishwa kwa vikao hivyo, vikao vinne vya baraza havikuwahi kufanyika.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Nelson Mafie, alisema wafanye vikao vya nyuma vilivyopita kwa ajili ya kupitia hoja mbalimbali zikiwamo za mapato na matumizi.

Hata hivyo, hoja hiyo ilipingwa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Emmanuel Mkongo, kwa madai kuwa kikao hicho ni cha mwaka na kwamba makabrasha yana taarifa za mapato na matumizi.

"Nikiwa mkurugenzi, ninachojua kikao cha leo ni cha kujadili taarifa ya mwaka kwa sababu kamati zilikuwa zinaendelea na majukumu kama kawaida kwa muda wote. Baraza lilipositishwa kamati zilijadili taarifa ya robo ya nne ya mwaka na kama hamataki, naomba niondoke niwaache mlumbane kwanza mkishamaliza nitarejea," alisema.

Mkongo alisema alipokea barua kutoka serikalini (hakutaja ni ngazi gani) Januari 13, mwaka huu, kuruhusu vikao vya baraza kuendelea kufanyika na kwamba madiwani hao hawatalipwa posho za vikao vya nyuma kwa muda wote baraza lilipokuwa limesitishwa.

Baada ya majibu hayo ya mkurugenzi, baadhi ya madiwani walianza kuonyesha vidole, wakitaka kujua hatima ya posho zao za vikao vilivyopita ambavyo havikufanyika.

Baada ya baraza kurejea saa tisa alasiri, hoja ya posho iliibuka tena na Mafie alidai kuwa Agosti 28, mwaka jana, walifika halmashauri na kutia saini daftari la mahudhurio kisha kikao kikaanza na baadaye kusitishwa, lakini hawakulipwa stahiki zao na kutaka kujua ni ngazi ipi ya serikali ilisitisha posho zao.

Pia aliomba baraza hilo kupatiwa taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi chote ambacho vikao vya baraza havikufanyika.

Akijibu hoja hiyo, Mkongo alisema licha ya madiwani hao kutokuwapo, ofisi yake kwa kushirikiana na watumishi wa halmashauri wametekeleza majukumu yote muhimu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanafunzi wote wa kidato cha kwanza wanaanza masomo kwa wakati.

"Naomba niwatoe hofu halmashauri yenu iko salama na Rais John Magufuli hakuniteua kwa makosa kuja kufanya kazi katika halmashauri hii. Nitaendelea kusimamia sheria na kanuni muda wote wa utendaji wangu nitakapokua hapa kumsaidia Rais," alisema.

Alisema muda umeshapita na wanatakiwa kuendelea na vikao vya bajeti ya halmashauri ya mwaka 2020/21 na kwamba hoja yao ya kutaka kufanya vikao vya nyuma kwa sasa haina mashiko.

Baada ya maelezo hayo ya mkurugenzi, Mwenyekiti Njau aliridhia hoja ya awali ya mkurugenzi ya kikao hicho kuwa cha mwaka na walikubali kupokea taarifa ya mwaka na kujidaili.





# Tanzania yapewa 5 uzalishaji mchele

**Na Mary Mosha, MOSHI**

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha mchele mzuri na msafi na ambao una thamani ukilinganisha na unaozalishwa Msumbiji, Kenya, Rwanda na Burundi.

Sambamba na hilo imetajwa kuwa nchi yenye idadi kubwa ya wanawake wanaozalisha kwa wingi zao hilo, ambapo huzalisha tani 5-8 kwa hekta ukilinganisha na nchi ya Msumbiji na Kenya.

Hayo yalibainishwa na mtaalamu wa kilimo kutoka Jimbo la Zambezia nchini Msumbiji, Jaime Gado, alipotembelea nchini akiwa na timu ya wataalamu saba wa zao la mpunga na mtaalamu mmoja kutoka Japan kwa lengo la kubadilishana ujuzi na kujifunza kutoka kwa wakulima wa Tanzania kuhusu namna ya kuzalisha mpunga bora.

Gado alisema mbali na changamoto ya kuwa na mashine zilizochakaa na ubovu wa miundombinu ikiwamo barabara, bado mkulima wa Tanzania amekuwa na ari ya kuzalisha mpunga ulio bora ukilinganisha na nchi nyingine.

"Tumeona changamoto kadha wa kadha, lakini bado mkulima huyu amekuwa akizalisha kilicho bora, tatizo ni uhakika wa soko...naishauri mamlaka husika kuangalia namna ya kumsaidia mkulima huyu ili pia aweze kuuza kwa wingi katika nchi zinazozunguka Bara la Afrika," alisema.

Aliongeza kuwa: "Nipende pia kuwapongeza Jica kwa kuweka utaratibu wa kuongeza thamani ya zao hili kwa kusaidia kusimamia makubaliano kati ya wanunuzi na wakulima wa Tanzania kupitia kwenye mradi wa Tanrice 2, kwani umekuwa mkombozi kwa wakulima wengi hususani waliopo kwenye skimu ya Lower Moshi."

Awali akizungumza wakati wa mafunzo hayo ambayo yalilenga kubadilishana uzoefu na wataalamu wa kilimo nchini, mshauri mkuu wa kiufundi katika mradi wa maendeleo ya uzalishaji wa mpunga wa Tanrice 2, Monitori Tomitaka, alisema idadi kubwa ya wazalishaji wa mpunga ni wanawake.

JICA linatekeleza mradi wa Tanrice 2 nchini na Proapa nchini Msumbiji, na wataalamu wamekuwa wakibadilishana ujuzi kwa lengo la kusaidia kuongeza uzalishaji.

**"Tumeona changamoto kadha wa kadha, lakini bado mkulima huyu amekuwa akizalisha kilicho bora, tatizo ni uhakika wa soko...naishauri mamlaka husika...**

# Mwakyembe avitaka vyuo habari kufundisha historia

**Na Mary Mosha, MOSHI**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amesema ipo haja ya vyuo vyote vinavyofundisha taaluma ya habari nchini kufundisha somo la histori ya ukombozi wa nchi na Bara la Afrika, lengo likiwa kuzalisha wanahabari wenye uelewa mpana juu ya masuala ya nchi yao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki alipokutana na wanahabari pamoja na wadau wa habari mkoani Kilimanjaro, ambapo alisema ufundishwaji wa historia ya nchi na Bara la Afrika utaweza kuwasaidia wanahabari kupata mtazamo chanya juu ya taifa lao.

"Ipo haja ya vyuo hivyo kufundisha historia ya nchi na ya Bara la Afrika, namna tulivyopata uhuru na ukombozi wake...lengo likiwa kuwasaidia kuwa walimu wa kuielimisha jamii na kiwa kuna ukosoaji wakosoe kwa njia ya kutaka maendeleo na sio kubomoa vitu vyema vilivyojengwa na waasisi wa taifa hili," alisema.

Aliwasisitiza wanahabari umuhimu wa kujiendeleza kitaaluma badala ya kuacha dhana kuwa serikali inaweza kuongeza muda wa utekelezaji wa sheria ya huduma ya habari 2016, ambato pamoja na mambo mengine inamtaka mwanahabari kuwa na elimu angalao ya stashahada ya taaluma hiyo.

"Wanahabari kila ninapopita katika ziara zangu za kuzungunza nanyi naendelea kusisitiza juu ya kujiongezea elimu kutokana na masilahi duni mnayolipwa... na mimi kama waziri mwenye dhamana sitakubali kuendelea kukubali mateso na manyanyaso hayo," alisema na kuendelea: ""Badala yake ni lazima nihakikishe haki zenu zinapatikana kama sekta nyingine duniani."

"Wengi wanaikosoa sheria hiyo hata kufikishwa mahakamani, lakini ukweli ni kwamba wanahabari mjitahidi katika kuhakikisha mnapata muda wa kuisoma na kuielewa katika kuleta mabadiliko katika taaluma hii, kwani utafiti unaonyesha kuwa wanahabari wengi hawajaipitia sheria hiyo badala yake hupewa propaganda kutoka kwa baadhi ya watu wasioipenda tasnia hii," alisema.

Awali akimkaribisha Waziri Mwakyembe katika majadiliano hayo Mkurugenzi TBC, Dk. Ayubu Rioba, aliwataka wanahabari kutumia muda mrefu kujisomea mambo mbalimbali ya nchi ili kuleta mabadiliko yao katika utendaji wao wa kazi na kwa nchi kwa ujumla.

Enos Masanja, mwanahabari kutoka Azam TV, aliiomba wizara kuwasaidia wanahabari kutafsiri sheria hiyo kwani wengi wao hushindwa kusoma na kutafsiri mambo yaliyomo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, aliwataka wanahabari kutumia muda uliobaki vyema kuelekea kwenye sheria mpya ya habari itakayoanza kutekelezwa mapema 2022.




Salome Kadio, mkazi wa Kata ya Ruvu, Wilaya ya Same, akieleza namna vitendo vya ukeketaji kwa watoto wa jamii ya wafugaji wa Kimaasai vinavyoongezeka kwenye kata hiyo, na kuathiri watoto wa kike kuendelea na elimu ya sekondari, katika mkutano uliofanyika wikiendi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mfuko wa maafa watakiwa katika jamii

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

JAMII imetakiwa kuwa na mfuko maalumu wa maafa ndani ya kata na kuwa na utaratibu wa kusaidiana pindi linapotokea janga au majanga kama ya kuunguliwa nyumba, mafuriko pamoja na magonjwa ya milipuko.

Ushauri huo umetolewa na Makamu Mwenyekiti wa Muungano wa Vyama vya Ushirika vya Uru Kaskazini, Felix Masao, wakati akikabidhi mabati 20 kwa Deogratias Urio, ambaye ni mwanachama wa chama cha ushirika Uru Kaskazini.

Masao alisema suala la majanga halina hodi badala yake hujitokeza ghafla pasipo na taarifa, hivyo ni vyema jamii ikawa na mfuko maalumu wa kusaidiana pindi linapotokea tatizo kama hilo.

Alisema endapo kutakuwa na mfuko maalumu na mfuko huo ukawa na bima maalumu ili pindi linapotokea tatizo iwe rahisi kutatuliwa itasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua mzigo kwa serikali ya kumsaidia mwananchi mmoja mmoja.

"Ndani ya serikali kuna mfuko wa maafa, ila nipende kutoa ushauri kwa jamii kuanzisha mfuko maalumu utakaokuwa ukisaidia pale linapotokea tatizo kama la Deogratias...sisi wana ushirika tumeguswa na tatizo hili na ndiyo maana nashauri jamii iwe na utaratibu wa aina hiyo," alisema Masao.

Mtendaji wa Kijiji cha Ongoma, Helena Kissae, alikiomba chama cha ushirika kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu katika kijiji hicho.

Aidha, alikishukuru chama hicho kupitia mradi wao wa muungano wa vyama vya ushirika kwa kutoa msaada wa mabati 20 kwa mhanga wa moto ambaye kwa mwezi amekosa mahali pa kuishi yeye na familia yake.

Mwathirika aliyeunguliwa na nyumba yake na kupoteza fedha taslimu zaidi ya shilingi milioni 20, alikishukuru chama cha hicho kupitia mradi wa pamoja kwa kumsaidia mabati 20.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 28, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 15

## Miaka 50 Shirika la Elimu Kibaha



Ukurasa 17

## Ujue wajibu wa kukusanya kodi



Ukurasa 19

## Aliyeongoza shule miaka 20, amiliki yake kwa staili mpya




# Kufunga vyuo vikuu kielelezo cha uwezo mdogo elimu ya juu

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# FFU kazini



Jeshi la Polisi, Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU), kikiwa kazini katika maeneo tofauti nchini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**






JIELIMISHE

# Corona yarefusha Siku ya Taifa China

**BEIJING,** China

CHINA jana ilirefusha siku kuu yake kubwa kabisa ya kitaifa, ili kuendelea kupata muda wa kupambana na mlipuko wa virusi vya Corona.

Hiyo inatokea huku kukiwapo idadi kubwa ya vifo inayoongezeka hadi watu 80. Kuna hatua sasa za ziada, kuna watu wanaozuiwa kwenye miji yao na hata hawaruhusiwi kusafiri.

Waziri Mkuu, Li Keqiang, alitembelea Mkoa wa Hubei ambao ndio chimbuko la kirusi hicho, ili kuongoza juhudi za kukabiliana na Corona mjini wa Wuhan, ambako kuna wakazi milioni 11. Kuwapo vifo 24 vilivyoripotiwa leo katika mkoa wa Hubei, huku idadi ya walioambukizwa ikipanda hadi 2,700 kote nchini humo ni ishara mbaya kimataifa.

Tayari kuna juhudu zingine za kimataifa, ugonjwa huo ukiripotiwa kusambaa katika nchi kadhaa, Mkuu wa Shirika la Afya Duaniani (WHO), Tedros Adhanom Ghebreyesus, ameelekea Beijing kukutana na maofisa wa serikali kujadili mzozo huo wa kiafya.

Matukio ya dalili za kusambaa ugonjwa huo sasa yanaripotiwa katika nchi za Ufaransa, Marekani na Canada, huku nchi nyingine za Asia zikigundua dalili za virusi hivyo.

Juzi Jumapili, nchi hiyo inayoathirika, ilitangaza kuongeza hatua zake za vizuizi vya kusafiri, ikiwa ni mbinu ya kujaribu kuudhibiti ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona, uliokwishawaua watu 56 na wengine 2,000 wameambukizwa.

Wakati huo huo Marekani, Ufaransa na Japan juzi zilisena zinajiandaa kuwaondoa raia wao katika mji huo, ulioko katika karantini ya chimbuko la virusi hivyo vya Wuhan. China imezuia watu ama kuingia au kutoka katika mji huo ulioathirika zaidi katika jimbo la Hubei, katikati ya nchi hiyo, ikiwa ni utekelezaji wa operesheni ya kunusuru mamilioni ya watu na kupunguza kasi ya ugonjwa huo kusambaa, Ni ugunjwa unaoathiri njia ya kupumua.

"Uwezo wa virusi hivyo kusambaa unaonekana kuwa imara zaidi , licha ya kuwa , si vyenye nguvu sana kama virusi vya SARS," maofisa waandamizi wa afya wa China, wamesema katika mkutano na waandishi habari.

Awali kulikuwapo virusi visivyojulikana vilivyosababisha wasiwasi mkubwa duniani kwa ukaribu wake kama virusi vya SARS, vilivyosababisha matatizo makubwa ya kupumua, ambavyo viliua mamia ya watu nchini China na Hong Kong katika mwaka 2002 hadi 2003.

Nje ya eneo ulipoanzia ugonjwa huo, miji minne, ikiwa ni pamoja Beijing na Shanghai na jimbo la Mashariki la Shandong, imetangaza marufuku kwa mabasi yanayosafirisha abiria masafa marefu kuingia ama kutoka katika mipaka yake, hatua ambayo itawaathiri mamilioni ya watu wanaosafiri kwa ajili ya sikukuu ya mwaka mpya.

China inajenga haraka hospitali itakayochukua wagonjwa 1,000 mjini Wuhan kwa azma ya kupambana na virusi vya Corona

**WAKAZI KUVAA VIZUWIZI USONI**

Jimbo maarufu la Mashariki la Guandong, Jiangxi katikati ya nchi hiyo, na miji mitatu imeweka ulazima kwa wakazi kuvaa vifunika uso wakiwa katika maeneo ya watu wengi. Ukianzia katika mji mkuu wa jimbo la Wuhan , Hubei, virusi hivyo vilisambaa nchini China na duniani,ambapo maambukizi yalithibitishwa katika karibu nchi 12 hadi Marekani.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani imesema Jumapili iliyopita, ilipanga kuwa na safari ya ndege kutoka Wuhan kwenda San Francisco kwa wafanyakazi wake wa ubalozi mdogo na Wamarekani wengine, mjini humo.

Katika taarifa ya barua pepe, siku ya Marekani imewaambia kwamba ina uwezo mdogo kuwachukua raia wake wa kawaida.

Wananchi mjini Beijing wakivaa vitambaa vya kufunika mdomo na pua kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona Serikali ya Ufaransa na kampuni ya Ufaransa ya kuunda magari ya PSA pia imesema wanatayarisha mipango kuwaondoa wafanyakazi na familia zao , ambao wanawekwa katika karantini katika mji uliopo katika jimbo jirani.

Japan inafanya uratibu na serikali ya China kuwaondoa haraka raia wake, waziri mkuu Shinzo Abe amesema. Ubalozi mdogo wa Korea kusini mjini Wuhan umesema unafanya taratibu za kuwahesabu raia wake kupitia mtandaoni ili kujua mahitaji ya ndege za kukodi zinazohitajika.



Ndivyo yalivyo matibabu na kujihami Corona. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Miaka 50 Shirika la Elimu Kibaha

- Sekondari, msingi mbili; wasichana, wavulana
- Hospitali Tumbi, shule mafunzo ya matabibu

SHIRIKA la Elimu Kibaha, mkoani Pwani, ni kati ya mashirika kongwe nchini linalotoa huduma za kijamii katika kutimiza lengo lake la kupigana na maadui watatu wakuu: Ujinga, maradhi na umasikini.

Mwaka 1963, serikali ya Tanganyika kwa kushirikiana na nchi za Kinordic (Norway, Sweden, Denmark na Finland) kwa pamoja zilianzisha mradi uliojulikana 'The Tanganyika Nordic Project.'

Madhumuni ya mradi yalikuwa ni kuleta maendeleo vijijini, ikiwa chombo cha mfano chenye kuleta maendeleo ya wananchi, kwa kutoa elimu inayowaandaa kupingania na madai ya matatu ya maendeleo kwa nchi huru: Ujinga, maradhi na umasikini.

Itakumbukwa ilikuwa ajenda mojawapo ya Mpango wa Maendeleo kwa Kwanza, mwaka 1964 hadi 1969 ibaeba hioja hizo .



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo, akikagua bidhaa za maonyesho, kwenye maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la Elimu Kibaha. **NA MPIGAPICHA WETU.**

### MRADI ULIPOANZA

Serikali ilikabidhiwa mradi huo wa Januari 10 mwaka 1970 na ndipo jina la mradi lilibadilika kuwa Shirika la Elimu Kibaha, wakati huo ukiwa ni katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, ulioendana na uundwaji mashirika mengi ya kimaendeleo katika zama hizo.

Ni aina ya mradi wa kimaendeleo ambao hatua za uanzishwaji wake unafanana na taasisi kama Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), ambalo ni la mwaka 1969, lakini mzizi wake unazama hadi myda mfupi tangu uhuru, huku mwaka 1973 kukabuniwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (Sido).

### SABABU UANZISHAJI

Madhumuni ya kuanzishwa Shirika hilo, ni kuendeleza wajibu wa utoaji elimu shuleni na inayohusu afya na kilimo, kutoa tiba na kinga kwa wananchi wanaozunguka eneo la Kibaha, huduma, zinazoendelea kupanuka hadi nje ya Kibaha.

Katika maadhimisho ya kuanzishwa Shirika la Elimu Kibaha, ambayo Januari 10 limetimiza miaka 50, Kaimu Mkurugenzi wake, Robert Shilingi, anaelezea namna linavyotekeleza majukumu yake.

Mbele ya mgeni rasmi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo, Sekondari ya Kibaha ilianzishwa mwaka 1965 ikiwa na wanafunzi 110.

Shilingi, anasema nia ni kuna na Shule ya Msingi Tumbi ambayo nayo iko chini ya shirika, ilianzishwa mwaka 1966 ikiwa na wanafunzi 30.

Mengine katika mradui huo kwa mujibu wa Shilingi, ni Kituo Cha Afya Tumbi, kilichoanzishwa mwaka 1967 na Chuo Cha Waganga Vijijini cha mwaka 1968.

Anasema, taasisi hizo zilianzishwa kwa lengo la kutoa elimu, na huduma kwa ajili ya kupambana na maradhi ya umma.

> "Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, ambayo ni ya kutwa, lengo ni kuiendeleza iwe ya bweni itakayochukua wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita.

Mbali ya Taasisi hizo, pia kilianzishwa Chuo Cha Wakulima mwaka 1964, kwa lengo la kutoa mafunzo ya kilimo na fani mbalimbali za ufundi kwa jamii ili kuondoa umasikini.

Shilingi anasema, shirika linaendelea kutoa huduma ya elimu ya msingi, sekondari na huduma za maktaba ili kuondoa ujinga.

"Mwaka 1970 shirika lilikuwa na shule moja ya msingi iliyokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 na shule moja ya sekondari iliyokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600, hadi kufikia Desemba mwaka 2019 tuna shule za sekondari tatu," anasema.

"Tuna Shule ya Sekondari Kibaha, hii ni ya bweni, inayopokea wanafunzi wenye vipaji maalumu kutoka sehemu mbalimbali za nchi, tuna sekondari ya Tumbi. Hii ni mchanganyiko iliyoanzishwa mwaka 1999, ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 640 wa kidato cha kwanza hadi cha nne.

"Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, ambayo ni ya kutwa, lengo ni kuiendeza iwe ya bweni itakayochukua wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita," anaeleza Shilingi.

### KITUO CHA AFYA

Kaimu Mkurugenzi huyo anasema, Kituo Cha Afya Tumbi kwa sasa ni Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani na Chuo Cha Waganga Wasaidizi Vijijini, kwa sasa ni Chuo Cha Afya na Sayansi Shirikishi.

Anaeleza kuwa chuo hicho, kwa sasa kimepiga hatua na kinatoa mafunzo katika fani za utabibu, uuguzi na Ukunga na afya ya jamii.

"Shirika la Elimu tumeendelea kutoa elimu dhidi ya kuondokana na Umasikini kupitia Chuo Cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha, ambacho awali kilijukikana Kama Chuo Cha Wakulima." anasema.

Katika kipindi Cha miaka 50 jumla ya wanachuo 11,912 walihitimu mafunzo ya fani mbalimbali na kwasasa kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 wa fani za muda mrefu" anaeleza.

Shilingi anasema kuwa, Taasisi zote zilizopo katika Shirika hilo, zimekuwa zikijitahidi kutoa huduma kwa ufanisi kwa kuzingatia malengo ya kuanzishwa kwake na hivyo kuwafikishia wakazi wa Mkoa wa Pwani na nje ya mkoa huo.

Anasema, mbali ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho Cha miaka 50, pia zipo changamoto zinazokabili shirika hilo, anaainisha changamoto hizo kuwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti ya kuendeshea taasisi Kibaha na uchakavu wa miundombinu.

Shilingi anasema, ili kupambana na changamoto hizo, shirika limejipanga kutumia ardhi ya shirika kama chanzo cha mapato, kuandaa maandiko ya miradi kwa wadau wa maendeleo, ili kutafutwa kuungwa mkono na mashirika yasiyo ya kiserikali.

### WAZIRI JAFFO

Akizungumza katika Maadhimisho hayo, Waziri Jafo anasema, changamoto za miundombinu tayari zimeanza kufanyiwa kazi, hususani upande wa Shule ya Sekondari ya Kibaha.

Jafo anasema, ukarabati wa shule hiyo ya sekondari umeenda sambamba na shule nyingine kongwe 63 ambazo serikali ilizitenga kiasi cha Sh. bilion 49.9.

Akizungumzia huduma ya dharura katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi, Jafo anasema, ombi hilo litashughulikiwa ili kuokoa vifo vya wagonjwa. Jafo anaahidi kushughulikia changamoto zilizoainishwa na Kaimu Mkurugenzi huyo wa Shirika la Elimu Kibaha, huku akimpatia jukumu la kuhakikisha anatengeneza timu nzuri, ambayo itafanya kazi kwa ushirikiano kutatua changamoto za wafanyakazi waliopo.

Anawataka, pia watumishi katika idara yake ya afya kufanya kazi kwa ufanisi na kuachana na lugha chafu kwa wagonjwa wanaofika kuhudumiwa hospitalini Tumbi.

Ni kauli ya Jafo, iliyotokana na hatua ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, kumueleza malalamiko ya baadhi ya watumishi hospitalini Tumbi, kuwa na lugha zisizo rafiki kwa wagonjwa, malalamiko yanayoongezeka kila siku.

Waziri huyo anasema, wizara yake itaendelea kushirikiana na Shirika la Elimu Kibaha, katika kukabiliana na changamoto zilizopo liendelee kutekeleza mipango yake iliyojipangia.

Shirika la Elimu Kibaha limekuwa limekuwa na historia kwa wakazi wa Pwani kutokana na huduma za kijamii zinazopatikana, lakini pia msaada kwa Vijana wanaosoma elimu ya Ufundi.

ELIMU

NA NIMI MWETA

# Kufunga vyuo vikuu kielelezo cha uwezo mdogo elimu ya juu nchini?

## • Huu hapa mbadala hai kwa watekelezaji mradi

HATUA iliyochukuliwa na serikali kupitia Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (TCU), yenye lengo la kuhakikisha kuwa viwango vinafuatwa kikamilifu katika taasisi tofauti za elimu ya juu ni kielelezo cha hali halisi katika sekta ya elimu kwa jumla na elimu ya juu kwa upande mwingine.

Tume hiyo imefungia vyuo vikuu sita na kampasi au vituo vitatu vya vyuo vikuu vingine ambavyo vinaendelea kutoa huduma katika vituo vyake vikuu, wakati vya ziada vimezidiwa nguvu, haviwezi kuendesha masomo ya elimu ya juu kwa ufanisi na kukidhi viwango stahiki.

Haikuwa ni hatua iliyochukuliwa haraka, kwani tume ilitoa tahadhari ya miaka minne kuangalia maendeleo ya taasisi hizo hasa katika eneo la rasilimali watu, wakufunzi wenye vyeti vinavyohitajiwa kwa ngazi ya uhadhiri, uandamizi wa uhadhiri, uprofesa wa fani kadhaa husika.

Yako pia maeneo mengine ambako taasisi hizo zilihitajiwa kuonyesha mabadiliko, lakini taarifa ya tume kwa kuchukua hatua hiyo ililenga zaidi tatizo la rasilimali watu, kwani uwezo wa kutoa mihadhara darasani, unaendana na kiwango cha anayetoa mihadhara hiyo.

Pia kiwango cha kutathmini nacho, kitaendana na kile cha ufundishaji, au kuandika tungo za kitaaluma kufikia ngazi za shahada za kwanza, pili au hata za tatu unaendana na viwango hivyo vya ubora wa wahadhiri na kina cha ufundishaji.

Ni maeneo ambayo hata waliofungiwa wanayafahamu, kwani wakuu hao wengi ni wahadhiri na maprofesa ambao kwa kiasi kikubwa wana historia ya pakongwe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ndani ya historia takriban miaka 50, tangu mwaka 1970 ilipotangazwa chuo kikuu kinachojitegemea.

Ni chimbuko linaloweza kufumbuliwa kwa kiasi fulani, kwa kushirikisha ndugu yake Chuo Kikuu cha Sokoine Morogoro (SUA), iliyojikita katika kilimo, kwani ilianza katika nafasi ya tawi la UDSM.

Ikiangalia safu ya wahadhiri waandamizi waliokuwa katika vyuo vikuu vipya, hata ungeongeza hivyo vilivyofungiwa, kitovu cha rasilimali watu wake ni waliochukuliwa kutoka safu ya wahadhiri na maprofesa kutoka UDSM.




Chuo Kikuu cha Tiba – IMTU, jijini Dar es Salaam.

> Hizo ni dhamana ambazo kwa kawaida zinaongezeka thamani, hivyo wenye hisa wanapata gawio na chuo kikuu husika kinafaidika.




Chuo Kikuu cha Josiah Kibira, Bukoba, tawi la Chuo Kikuu cha Makumira, Arusha. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### SWALI LINAPOANZA

Suala ni baada ya kuwapata wazoefu hao kuanzisha chuo kikuu kipya au kituo (kampasi) mpya ya chuo kikuu kimojawapo, kulikuwapo uwezo gani kifedha kuajiri wengine wenye hadhi ya uhadhiri kwa mpangilio wa UDSM, au kuwezesha wasome kufikia ngazi ya uzamivu (PhD) kukitumikia chuo kwa ufanisi?

Hapo ndipo kwenye dalili za matatizo. Kuna vianzio vya rasilimali fedha havikujengeka, kupanuka, au huenda vilidumaa, baada ya kupatikana michango ya kuanzisha chuo na kuweka msingi wa kitaaluma inayotakiwa.

Tafakari ya hali hiyo, inaibua mtazamo wa hoja, kwamba kuna utata katika uwepo wa mfumo tegemezi katika uanzishaji vyuo vikuu, huo unaonekana dhahiri katika taasisi kama vyuo, hali inayojitokeza sana hata katika mifumo mingine ya kibiashara,

Ndani ya vyuo vikuu mchango wa kwanza ni ada za masomo, lakini kwa vile ushindani ni mkubwa, uwezo wa soko haukui kwa kiwango kinachoridhisha, hali inayotoa uwezekano wa uwezo wa kulipa ada unapungua badala ya kuongezeka katika miaka kadhaa sasa.



Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Profesa Charles Kihampa.

Tathmini hiyo haihitaji takwimu za kina, kwani elimu ya juu kwa mtu binafsi ni hitaji la ziada, baada ya mahitaji ya msingi kama chakula, mavazi na makazi, pindi mtu anapokabiliwa na kupungua fedha za matumizi,

Mzazi kumsomesha mtoto chuo kikuu ni jambo muhimu, ila baada ya kukidhi mahitaji ya lazima, ambayo hayakwepeki, panapo uhai.

### PENGO LA UKUAJI

Mtu anapoangalia kwa upande wa kukua kwa elimu nchini, kufungwa vyuo vikuu sita na vituo vitatu vya vyuo vya aina hiyo, ni ishara isiyohitajika ya kudumaa ukuaji wa elimu ya juu nchini, ikizigantiwa idadi ya Watanzania inaongezeka, hisabati imeshavuka 50 ikisonga mbele.

Hiyo ni kwa mujibu wa makisio ya kitaaluma na kitaasisi yaliyopo sasa, baadhi wakienda mbali kwamba kila mkoa unapaswa kuwa na chuo kikuu kimoja.

Kwa mataifa yaliyopiga hatua, mfano hao nchini Marekani, katika mgawanyo kama huo (wa mikoa) unaokisiwa nchini Tanzania, wasomi na taasisi katika maeneo hayo yanakuwa na chuo kikuu kimoja cha taifa (cha serikali).

Ni mgawanyiko unaoenda mbali, katika maeneo hayo mbali na vyuo vikuu vya kitaifa, tena kuna walau kingine kimoja binafsi na taasisi zingine zenye vyuo vya elimu ya juu kwa fani tofauti.

Siyo rahisi kusema vyuo vikuu vilivyofungwa vitafufuliwa hivi karibuni kwa njia ya wadau ama kujituma zaidi au kupata misaada kwingineko, labda panapo majaliwa ya uhusiano mzuri kitaifa na kimataifa. Kigezo hapo kipo, kwamba msukumo wa TCU kuzitaka zibadilike zina miaka mingi.

Inawezekana vyuo nyingi kati ya vilizofungwa, vitadumu kwa miaka kadhaa kupata mazingira mapya ya kuziwezesha kuibuka upya. Hicho nacho ni kielelezo kingine, kuwa badala ya kusonga mbele kufungua vyuo vikuu vipya, nchi inarejea nyuma kunaimarisha vilivyopo.

Ni sura ambayo pasipo kubadilishwa, inaangukia dhana ya kuwapo vyuo vikuu vingi zaidi ndani ya udumavu, kwani katika hatua za maendeleo, mahitaji ya miaka mitano hayatakuwa ya leo na dira yake inaangukia kwenye makubwa zaidi.

### KUPATIKANA SOMO

Siyo rahisi kusema au kujua kama itafikia mahali wasomi nchini na hasa wadau katika sekta ya elimu kwa jumla, watakuwa katika mazingira ya kuangalia kwa kina nini kinachosibu sekta ya elimu ya juu? Hata hivyo, wanaweza kulenga katika suala moja tu, kati ya njia kuu tatu za kupata fedha na kuendeleza vyuo vikuu kutoka kwa waliofanikiwa.

Nchini Marekani kunaweza kuwa somo, ikizingatiwa, Ulaya kwa sehemu kubwa zaidi vyuo ni vya serikali au umma, kukiwapo njia moja tu ya kuingiza mapato kutoka ada kwa wanafunzi, hali inayotawala nchini.

Kimsingi, ushindani unapunguza uwezo wa ongezeko la kipato cha ada na rasilimali watu wakuu, wahadhiri na maprofesa wanalazimika kupandishwa mishahara.

> Kimsingi, ushindani unapunguza uwezo wa ongezeko la kipato cha ada na rasilimali watu wakuu.

Maeneo yaliyobaki ni kutokuwapo mfumo wa mali binafsi katika ardhi ambako chuo kimejengwa, kugeuzwa mali binafsi, kufikia mfumo uitwao ‘mutual funds’ kwa maana ya mkusanyiko wa dhamana zinazouzwa na kununuliwa kwa pamoja katika masoko ya hisa.

Hizo ni dhamana ambazo kwa kawaida zinaongezeka thamani, hivyo wenye hisa wanapata gawio na chuo kikuu husika kinafaidika.

Mfano mdogo, ni katika uwekezaji wa pesa Sh. milioni 100 kabla ya kuanza kupokea ada, halafu kuna watu waliosoma hapo waliofikia umri mkubwa hawawaachii vijana wao fedha waziharibu.

Anachokifanya, ni kwamba ananunua au kudhamini taasisi au masomo yaitwe kwa jina lake, hivyo aache sehemu kubwa ya mali zake au fedha benki kama amana ya muda maalum (fixed deposit) inayotoa faida ya riba kwa ajili ya chuo hicho.

Hatua, nyingine ni michango ya moja kwa moja kwa chuo. Katika baadhi ya nchi, michango hiyo inaondolewa kodi.

---

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Ujue wajibu wa kukusanya kodi



Maofisa Kodi wakikagua biashara. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KULIPA kodi hutajwa kuwa wajibu wa msingi kwa kila mtu aishiye katika serikali ya kisiasa.

Kodi inatajwa kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa serikali ya kisasa, ikigharamia mahitaji mbalimbali na kuendesha dola hiyo, kama vile gharama za mishahara na kutoa huduma muhimu, zinazotolewa na serikali hiyo.

Aidha, kuna aina mbalimbali za kodi: Kodi za moja kwa moja kutoka wananchi; mapato, kila mtu mwenye mapato hutozwa asilimia fulani kulingana anachokipata.

Pia, kuna kodi isiyo dhahiri kupitia bei za bidhaa au huduma, mfano kodi ya mauzo; na zinazotegemea mali ya watu, mfano nyumba au shamba.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inataja wajibu kadhaa wa kila mlipa kodi, anayestahili kusajiliwa kisheria.

• Uwasilishaji wa marejesho;Mlipakodi aliyesajiliwa ana wajibu kisheria kuwasilisha marejesho na kulipa kodi iliyokadiriwa kwa muda unaotakiwa.

• Usahihi wa marejesho na nyaraka za forodha na madai ya marejesho kutoka kwa mlipakodi

. Mlipakodi anatakiwa kulipa kwa wakati, kuepuka adhabu au, pia riba zilizoainishwa kisheria.

• Kutoa na kudai stakabadhi na ankara za kodi za kielektroniki, katika kila ununuzi utakaofanyika

• Ushirikiano na maofisa wa TRA; mlipakodi ana wajibika kuwapa ushirikiano kwa maofisa wa TRA kwa kutoa taarifa na nyaraka inayohitajika na sahihi, au taarifa nyinginezo anapotakiwa kufanya hivyo.

Inafafanuliwa zaidi kwamba, kila mtu ana wajibu wa kutoa ushirikiano kwa maofisa TRA na kuwapa kutimiza wajibu wao wa kisheria pasipo kuwaingilia kwa namna yoyote.



Shughuli za ulipaji kodi zikiendelea.

### MADHARA YA KUKWEPA

Mlipa kodi anayesindwa kulipa, huagukia katika sharia za kodi na nyinginezo kadhaa kama vile: Kushtakiwa mahakamani; malipo ya ziada; kulipa kwa kuuza mali yake anaposhindwa; na kuwekewa vikwazo vya kutoenda sehemu nyingine; na mali yake kuzuiwa

### UKUSANYAJI KODI

Malipo ya kodi ni wajibu wa wananchi hata kama watu wengi wanajaribu kuepukana nayo. Serikali inadai malipo ikitisha adhabu kwa watu wanaoficha mapato yao au wanaokataa malipo.

Serikali huwa na idara za kodi ambazo zimekabidhiwa jukumu la kutunza kumbukumbu ya malipo na kukusanya pesa zinazodaiwa.

Katika mazingira ya kisasa ni kampuni zinazopaswa kukusanya kodi za wafanyakazi kwa njia ya kukata kodi kwenye mshahara na kuzikabidhi kwa serikali.

Biashara zinatakiwa kutunza kumbukumbu za mapato kwa kodi isipokuwa mara nyingi biashara ndogondogo hutozwa kiasi fulani isiyobadilika bila kuchunguza mapato yenyewe.

***Kwa mujibu wa tovuti za TRA na Legal Aids Clinic, toleo la mwaka 2017.**

JE, WAJUA?

## NEW DELHI, INDIA

# Harusi ya mapacha wanne siku moja

• Kaka yao... abaki mpweke



Mapacha wanne wakiwa katika picha ya pamoja na wazazi wao, wawili kushoto na wawili kulia. **PICHA: MTANDAO**

CHEREKO aina yake, dada wanne kutoka jimbo la South Dandian, Kerala waliozaliwa siku moja, kuishi pamoja katika nyumba moja wanaolewa kwa mpigo, wakimuacha kaka aliyezaliwa nao anashangaa.

Kinadada hao, maisha yao yalitawaliwa na vazi la sare, shule na nyumbani, wanafunzi wa darasa hadi kufika miaka 15, sasa mbioni kuolewa kila mtu atasonga kwake.

Walijulikana 'wadada wanne' tangu wazaliwe na hata kwenye mitandao ya kijamii wanatumia hadi sasa 'akaunti' moja kabla ya kutawanyika.

Kwa majina hao ni Uthra, Uthraja, Uthara, Uthama, wazaliwa wa Novemba mwaka 1995 na wanapanga kufunga ndoa mwaka ujao, April 26.

"Mazungumzo yetu kwa sasa nyumbani ni kuhusu harusi yetu. Tunaangalia kitambaa gani tutanunua kwa ajili ya magauni yetu ya harusi. Lakini, tutanunua kitambaa cha aina mmoja na rangi moja na mshoto mmoja," Uthara.

Katika waoaji, mmoja ni mwanahabari, huku harusi hiyo inatarajiwa kuwa ya kiutamaduni zaidi, ikielezwa ni chimbuko la wachumba waliochaguliwa, badala ya wao kuchagua watu wa kuwaoa. Mama yao ndiye aliingia katika mtandao kuwachagulia wachumba na kwa mujibu wa mazingira ya India, ni aina ya uchumba na harusi inayohusisha watu wenye elimu au uchumi ulio na nafuu.

Hata hivyo, kuna vigezo vya kiutamaduni kama vile kuliganisha nyota za maharusi, pia historia za familia, huku ikizingatiwa ridhaa ya anayeoa na kuolewa.

Jambo moja linaloeleza hilo, ni kwamba harusi hiyo haiwafanyi mapacha waonane wako tofauti na watahakikishiwa harusi yao inafanana kila kitu.

Ni mapacha wanaoelezwa katika mfumo wa mapacha yao kila siku maisha yao hawajaacha kufanana na takriban kila kitu tangu wazaliwe, licha ya kwamba si mapacha waliofanana kwa kila kitu.

Mmoja wao, Uthraja alifukuzwa shule, Uthama alipenda muziki na alijifunza kupiga vyombo vyake aina ya ' violin', huku kaka yao Uthrajan alipenda kupiga vyombo vya muziki wa India.

Uthra, alienda kusomea ubunifu wa nguo naUthraja na Uthama, walikuwa mafundi mitambo hospitalini.

Hivyo walivyoanza kutafuta waume zao, Uthraja alianza kwa kutafuta mwenza kwa mwaka mmoja uliopita, lakini aliamua kutokuwa na haraka.

"Ni mama yetu ndiye alikuwa anatamani tuolewe siku moja. Hivyo, tuliamua kusubiri," Uthraja anatamka, huku akiongeza kwamba kupanga harusi ya Kihindi ni gharama sana na nyingi zinajumuisha wanafamilia wa karibu, kupunguza gharama hiyo.

Hivyo, dada hao wanne kupanga harusi ya pamoja, ni msaada kwaa mama huyo, huku maharusi wanafurahia.

"Huwa tunafanya kazi pamoja katika hospitali moja kabla hajaenda Kuwait. Tunafahamiana na familia yake ilifurahi kuja kwa mama yangu," anasema mume wa Uthraja, ambaye anatarajia kuhamia nchini Kuwait kikazi.

Bado kumbukumbu, wazazi walifurahi sana kuwakaribisha duniani mapacha hao watano na nyumba yao wakaipa jina la"Pancharatna" - ikiwa ina maana ya vito.

Watoto hao walikuwa na maendeleo mazuri shuleni ingawa afya ndio ilikuwa mgogoro.

"Walizaliwa wakiwa na uzito mdogo na walikuwa wakiugua kila mara," alikumbuka Rema Devi, mama yao.

Wazazi wao Prema Kumar na Rema Devi, wana simulizi ya kutaabika sana kuwalea watoto wao watano, huku kipato chao kikiwa kidogo sana. Kipaumbele chao kilikuwa elimu.

Utamaduni wa nchini India, mtoto wa kiume huwa anapewa kipaumbele zaidi kuliko mabinti. Lakini mapacha hao wanne wa kike wanasema kwao ilikuwa tofauti kupata kipaumbele cha kiume katika familia.

Vilevile wanasema wazazi wao waliwapa haki zao sawa, kwa kuwanunulia nguo zinazofanana, hata kufikia hatua wanavaliana nguo hizo.

"Tulikuwa hatugombani, tulikuwa hatukasirikiani tukivaliana nguo," anasimulia Uthara.

Baba yao alikuwa na duka la vifaa vya shule ndio lilikuwa chanzo cha kipato chao, wakati watoto hao wana miaka tisa, baba huyo alipata hasara kubwa katika biashara, akaamua kujiua mwaka 2004.

Jirani yao ambaye ni daktari, aliguswa na maisha yao hivyo aliamua kuwasaidia kwa kuwapa mahali pa kuishi na shuleni, watoto hao walihitimu kwa ufaulu wa juu, Uthara akisimulia: "Mama yetu anafuraha sana na anataka tuwe huru."

Hivi, sasa tukio la harusi yao itakayofanyika katika hekalu maarufu nchini India, imepata umaarufu wa pekee, ndugu wana karibu ndio watakaokaribishwa peke yake, waandishi wa habari nao hawatakosa.

"Harusi hii itakuwa ya aina yake na baraka kubwa kwetu," anasema Uthara na mitandao ya kijamii na vyombo vya habari imetawaliwa na habari namna kinadada hao waliozaliwa siku moja watafunga ndoa.

Sasa wako katika hatua ya kutafakari namna watakavyokumbukana, baada ya kutawanyika .

## RIPOTI

# Zimbabwe wawaka darasa rushwa kutoka Uganda

RAIA wa Zimbabwe wamekuja juu, baada ya Jaji Mkuu nchini humo kummualika Jaji wa Uganda, kutoa mafunzo kwa mahakimu wa Zimbabwe, kuhusu namna ya kukabiliana na ufisadi.

Kupitia mitandao ya kijamii, raia wa Zimbabwe wamechachamaa, kwamba Uganda sio nchi sahihi ya kujifunza kwa Jaji Mkuu wao.

"Tafadhali muache kuharibu rasilimali za wananchi. Je, tunahitaji usaidizi wa Uganda kukabiliana na ufisadi nchini Zimbabwe?" ni sehemu ya nukuu, huku mwingine akijenga hoja: "Uganda kukabiliana na ufisadi... kwanza tazama nchi ambayo mnaiomba ushauri na usaidizi."



Jaji Mkuu wa Uganda, Bart Katureebe. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Jaji mkuu wa Zimbabwe, Luke Malaba, aliwaambia wanahabari kwamba, Hakimu Justice Lawrence Gidudu, kiongozi wa jopo la kukabiliana na ufisadi Uganda, atatoa mafunzo ya wiki moja katika mji mkuu wa Zimbabwe, Harare.

Jaji Malaba anasema, Zimbabwe ina mengi ya kujifunza kutoka Uganda, ambayo imeshawashitaki na kuwafunga watu waliopatikana na makosa ya ufisadi kwa miaka mingi sasa.

Ni hatua inayochukuliwa kabla ya kuanzishwa kwa mahakama mpya za kukabiliana ufisadi. Katika hotuba yake ya mwaka wa sheria 2020, Jaji Mkuu Malaba anasema, mfumo wa mahakama unaimarisha juhudi za kukabiliana na ufisadi.

Uganda tayari ina mahakama maalum za kukabiliana na ufisadi kwa takriban miaka 10 imepita, iliorodheshwa kuwa bora zaidi na shirika la Transparency International mwaka jana.

Katika orodha hiyo, Uganda ilikuwa nafasi nzuri kuliko Zimbabwe ikiorodheshwa.

Hata hivyo, kuwa ikirejewa ripoti ya Transparency International, majirani wa Zimbabwe, nchi kama Botswana, Namibia na Afrika Kusini ziliorodheshwa katika nafasi nzuri zaidi ya Uganda, jambo ambalo walalamikaji wanahoji, kwanini darasa la vita ya ruswa lisichukuliwe huko?

**Kwa mujibu wa mtandao.**



Jaji Mkuu wa Zimbabwe, Luker Malaba.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Aliyeongoza shule miaka 20, amiliki yake kwa staili mpya

• Atamba kujua upungufu ulikojificha • Hakuna kumpunguza 'asiyejiweza' • Mbinu tatu za kuwainua wasomaji

MAFUNZO ya uongozi na usimamizi wa elimu ni moja ya njia inayotoa fursa kubwa kwa viongozi ngazi ya shule katika kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kuongoza na kusimamia shughuli za shule.


Ni mfumo unaotoa fursa kwa viongozi wa ngazi hizo kusimamia taaluma na kuleta matokeo chanya katika nyanja za uongozi na usimamizi wa majukumu.

Kumekuwapo wakala mbalimbali wa serikali nchini katika kufanikisha hilo, akiwamo Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), waliotoa mafunzo ya aina hiyo kwa wakuu wa shule za sekondari za serikali na binafsi, lengo ni kuwawezesha kubadilishana mawazo ya namna bora kuboresha utendaji shuleni.

Ni mkakati unaoenda sambamba na utoaji maelekezo ya utendaji wa kazi ya kutoa elimu bora.

Mmiliki wa Shule ya Sekondari Balili, iliyopo Mbagala Kuu jijini Dar es Salaam, Lucas Hassan, ambaye pia anafundisha masomo ya Baiolojia na Kemia, anasema uzoefu wake katika kuongoza shule mbalimbali nchini, umempa upeo wa kujifunza mengi ya uongozi wa shule.

Anasema, alishatumikia shule mbalimbali za sekondari katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa miaka 20, kabla ya kumiliki shule yake, akiwa na ufunuo wa kushiriki mafunzo mengi ya uongozi, pia upungufu unaowanyima fursa baadhi ya Watanzania haki yao kupata elimu.



Wanafunzi wakiwa ndani ya chumba cha mitihani. Namna bora ya kuwanoa kwa mitihani ndio njia inayofanywa katika Shule ya Balili. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU.**



Mkuu wa Shule ya Balili, Richard Mgonja.

**VIWANGO DUNI**

Mwalimu Hassan, anasema aligundua mapengo ya kielimu yanayowanyima fursa wanafunzi wenye uelewa mdogo, kupata haki ya msingi ya elimu, hasa kwa hatua ya baadhi ya shule zinazowaondoa wanaoshindwa kufikia viwango vilivyowekwa na shule.

Anasema katika kulikabili hilo, shule yake imekuja na mikakati ya kutambua umuhimu wa wanafunzi wote kuwa na haki sawa ya kupata elimu bora na kuwezesha wanafunzi wote kunufaika kielimu.

Hassan anaoanisha hilo na dhana ya kitaifa iliyopo sasa, ikinuia kufikia Uchumi wa Kati wenye Tanzania ya Viwanda, inayobuni mbinu mbalimbali za kuwainua kielimu.

**MKUU WA SHULE**

Mkuu wa Shule hiyo, Richard Mgonja, anarejea mikakati ya kitaaluma iliyowekwa na shule yake, kwamba haibagui wanafunzi kwa kuwachukua wote wanaofundishika, lengo ni kuwainua kitaaluma na kutimiza ndoto zao za elimu.

Inafanikishwaje? Mgonja anasema, shule yao imekuwa ikiandaa mitihani ya kila mara, kuwawezesha wanafunzi kujifunza mbinu mbalimbali za kujibu maswali, ikiwa namna ya kuwajenga.

Anataja mbinu nyingine, ni ya kuongea na mwanafunzi mmoja mmoja na kumjenga kisaikolojia, ili aendelee kumudu masomo yake na kufanya vizuri katika mitihani.

"Uongozi wa shule umeunda bodi ya shule inayoitwa Balili Examination Board (BEB), inayofanya kazi ya kutunga mitihani ya kila mwisho wa mwezi na kuwapatia walimu waweze kuwapa wanafunzi na wanafunzi waliofanya vizuri na wale walioonyesha juhudi kitaaluma, kwa kupanda hatua moja hupatiwa motisha mbalimbali zikiwapo fedha," anasema Mgonja.

Pia, shule hiyo imekuwa na utaratibu wa kualika wazazi kila mara kufuatilia maendeleo ya wanafunzi na kupata maoni yao, lengo ni namna ya kuboresha zaidi viwango vyao vya ufaulu.

> Katika mazingira hayo inalazimika tu ukubali kuumia. Huwezi kupandisha karo wakati hali ya uchumi ni mbaya.

"Tunawashukuru wazazi na walezi kwa ushirikiano wao wanaouonyesha kwetu, kwa kuitikia mwito pale wanapohitajika kufanya hivyo," anasema Mgonja, huku akiwaomba wazazi wasichoke kufuatilia watoto wao.

Mbali na mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, anataja kuwapo maabara nne kwa mazoezi kwa ya vitendo shuleni, akifafanua: "Shule yetu ina maabara ya jiografia, fizikia, kemia na baiolojia ."

Mgonja aneleza mbinu za ufundishaji walizonazo, kwamba wanafunzi wake kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita hawatenganishwi, kama inavyofanyika katika shule nyingi, imekuwa ikiwachanganya, kama mbinu ya kuwainua walio na uwezo mdogo darasani.

"Katika kuhakikisha hili linafanikiwa shule imekuwa ikiandaa mitihani ya mara kwa mara na kutoa motisha kwa wote wanaofanya vizuri. Wale wanaovuka hatua moja mbele kwa kufanya vizuri kwenye mitihani yao," anasema Mgonja.

Anasema wakati wana huduma ya tiba, kupitia kituo cha afya chenye wahudumu, shule hiyo hivi sasa inajipanga kuangalia namna ya kuwasaidia watoto wanaotoka kwenye familia zisizojiweza kupata ama punguzo la ada au kusoma bure.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

Baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwaka huu, katika mikoa mbalimbali, hawajaripoti shuleni tangu shule zifunguliwe mwanzoni mwa mwezi huu. Wadau wanasemaje?



**MIRIAM LUWANDA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MTINDO huu wa baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari kutoripoti shuleni, unataka kuwa kama jambo la kawaida.

Kila mwaka wa masomo unapoanza, huwa kuna taarifa za baadhi yao kutoripoti shuleni bila kuwapo sababu za msingi. Inawezakana wapo wale ambao wazazi wao wanawahamishia katika shule binafsi, lakini wa aina hiyo sidhani kwamba ni wengi sana.

Umefika wakati sasa mamlaka husika kuchukua hatua kali za kisheria kwa wale ambao kwa makusudi hawaendi shule. Wazazi wao wabanwe, kwani inawezekana wakawa wanachangia kuwapo kwa tatizo hilo.

Jambo la msingi ni kuhakikisha wale wote waliochaguliwa kuanza sekondari wanahudhuria masomo, na kusiwe na kisingizio cha ada, kwa sababu serikali ilishaiondoa ili watoto wote wakiwamo wa maskini waweze kusoma.

Sasa kinachosababisha wasiende shule ni nini? Kama kuna wazazi wanafanya njama za kuwaoza mabinti zao, washughulikiwe kwa mujibu wa sheria.

Inasikitishia kuona mtoto amefaulu kwenda sekondari, halafu haendi shule. Kuna nini nyuma yake? Hebu jiulize kuhusu tukio la Mtwara, ambalo limeripotiwa kuwa wanafunzi wa kidato cha kwanza zaidi ya 3,000 hawajaripoti shuleni!

Wako wapi na wanafanya nini? Inauma sana. Kama kuna wazazi wanachangia kuwapo kwa utoro huo, wasionewe huruma kabisa.



**SHABAN CHANDE (MKAZI WA MJINI MOROGORO)**

HII siyo hali ya kawaida na inaendelea kujitokeza kila mwaka. Nakumbuka mwaka 2013, vyombo vya habari viliripoti tatizo kama hilo kwa Mkoa wa Ruvuma kwamba, karibu nusu tu ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mkoani Ruvuma mwaka walikuwa hawajaripoti katika shule za sekondari.

Moja ya sababu zilizodaiwa na baadhi ya wazazi kwamba, zinachangia utoro huo ilikuwa ni michango iliyokithiri katika shule za sekondari za kata, ambayo baadhi ya shule ilifikia zaidi ya Sh. 300,000.

Kwamba wazazi na walezi walio wengi ni maskini wanashindwa kumudu michango hiyo na wakati huo ada ya mwaka kwa sekondari za kata ilikuwa ni Sh. 20,000, lakini michango ikawa ni kikwazo kwao, ambao baadhi yao walikuwa wanasomesha watoto hadi watatu, hivyo kushindwa kumudu kulipa gharama hali iliyosababisha watoto wasiende shule.

Hizo ndizo zilikuwa sababu za wazazi wa mkoa huo wakati ada na michango havijaondolewa. Kwa sasa tatizo ni lipi ambalo linasababisha wanafunzi waliochaguliwa kwenda sekondari wasiende shule?

Ada na michango ilishafutwa shuleni, lakini cha kushangaza, matukio ya baadhi ya wanafunzi kuendelea kubaki nyumbani, huku wakiwa wamefaulu kwenda sekondari bado yapo, katika mikoa mbalimbali nchini.

Kuna haja ya kufuatilia kwa undani kujua ni nini chanzo kwa jambo hilo, ambalo mwisho wake ni kukwamisha maendeleo ya kielimu ya watoto wetu, ambao wanatarajia kuwa viongozi wa taifa la kesho.



**RHOBI SAMWELLY (MKAZI WA SERENGETI)**

MIMI kama mdau wa elimu, ninaona kuna sababu nyingi zikianzia kwenye uchumi, kwani wapo baadhi ya wazazi na walezi hali zao za kiuchumi ni duni kabisa na wanashindwa kutoa michango shuleni ikiwamo ya madawati na kuwanunulia watoto wao sare na madaftari.

Ninao mfano wa mwanafunzi, ambaye kwa sasa yupo nyumba yetu salama ya Butiama. Alifaulu kuanza kidato cha kwanza mwaka huu, lakini wazazi wako hawana kitu na sasa amelazimika kuja kwetu ili kumsaidia kuendelea na masomo.

Vilevile uelewa mdogo wa wazazi kuhusu elimu, mila na desturi ambazo zinasababisha mtoto wa kike kuolewa ili wapate mali vinasababisha watoto wengi wa kike kutoripoti. Na wengine hufikia kuwaambia wasijaze vizuri majibu ya mitihani ili mwisho wa siku waolewe.

Pamoja na hayo kuna suala umbali wa shule ambao husababisha baadhi ya wazazi kuzuia watoto wao kwenda shule wakihofia vitendo vya ubakaji ambavyo matokeo yake ni kupata mimba. Hayo yote na mengine mengi yanachangia watoto wengi kutoripoti shuleni kwa wakati.

Labda nitoe wito kwa jamii kwamba iwe tayari kusaidia ujenzi wa mabweni na pia kwa maeneo yetu ya vijijini, watoto wa kike wanunuliwe baiskeli, lakini pia wazazi wasio na uwezo wafunguke, waende kwenye ofisi za serikali za vijiji na kata kuelezea ili wasaidiwe badala ya kukaa na watoto bila kwenda kusoma na pia viongozi wa kuanzia madiwani na wabunge wawe tayari kusaidia suala hili la elimu wasijikite kwenye siasa tu.



**SALIM MJUNGU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIKU hizi jambo likizoeleka sana, watu wanasema kuwa ni wimbo wa taifa. Hivyo na mimi kwa jambo hili la baadhi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kushindwa kuripoti, ninaweza kusema kuwa ni wimbo wa taifa, kwa sababu lipo kwa miaka mingi sasa na linaendelea kujitokeza kila mwaka na huenda wapo ambao wanaliona kama la kawaida, lakini si jema kwa mustakabali wa elimu kwa mwanafunzi.

Bahati mbaya ni kwamba badala ya tatizo hili kupungua, linazidi kubwa kila mwaka. Hebu fikiria wilaya moja tu unakuta wanafunzi 5,000 hawajaripoti shuleni, sasa hali kama hiyo itakuwa nchi nzima mbona ni wanafunzi wengi sana watakuwa hawasomi, iwapo hatua za makusudi za kumaliza tatizo hili hazitachukuliwa haraka.

Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Musoma mkoani Mara, Dk. Vincent Anney, alikaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa wanafunzi zaidi ya 5,000 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu wilayani mwaka walishindwa kuripoti shuleni ndani ya wiki moja tangu shule zifunguliwe.

Hali hiyo ilimfanya awatangazie vita wazazi, ambao watoto wao hawajaripoti shuleni licha ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wilayani humo. Hii inaonyesha kuwa kwa namna moja ama nyingine, wazazi wanahusika kukwamisha watoto wao kuanza masomo kwa wakati. Hivyo ipo haja ya kuwafuatilia wazazi wa aina hiyo na kuwachukulia hatua za kisheria.



**JACOB MWENGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA mtazamo wangu ninadhani kuna uzembe, katika kushughulikia wale wanaokwamisha wanafunzi kuendelea na masomo ya sekondari. Tatizo hili ni la miaka nenda rudi.

Kwani kila mwaka wanafunzi wanapochaguliwa kwenda sekondari, baadaye huja taarifa kuwa baadhi yao hawajaripoti shule, na unaweza kukuta wameripoti wachache tu na kundi kubwa likiwa bado liko nyumbani.

Ndiyo maana ninasema kwamba tatizo hili ni la miaka nenda rudi siyo la mwaka huu tu na kama unafuatilia, utakuwa unalijua kwa kina kwamba imekuwa ni kawaida kila mwaka kusikia kwenye vyombo vya habari kutoka mikoa mbalimbali kwamba, wanafunzi wa kidato cha kwanza hajawaripoti shuleni licha ya kuchaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari.

Kwa maoni yangu ni kwamba serikali isifanye uzembe kwenye jambo hilo, ifuatilie kwa kina na kujua hao wanafunzi huwa wanakwenda wapi, wamejificha wapi hadi wasiende shule?

Ukishagundua chanzo cha tatizo hilo, ichukue hatua za kuhakikisha halitajirudia tena, vinginevyo kila mwaka tutaendelea kusikia taarifa za baadhi ya wanafunzi kutokwenda sekondari na mwisho wa siku litaonekana ni jambo la kawaida na kumbe ni hatari kwa maisha ya baadaye ya mwanafunzi.

Inauma sana mwanafunzi kusota kwa miaka saba akiwa shule ya msingi halafu anachaguliwa kwenda sekondari, lakini haendi, kwa nini?



## HABARI MBEYA

# Maelfu ya wakulima kushiriki maonyesho

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

ZAIDI ya wakulima 5,000 kutoka katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wanatarajiwa kushiriki kwenye maonyesho ya kilimo biashara yaliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Kituo cha Uyole jijini Mbeya.

Maonyesho hayo yameshaanza na yanatarajiwa kufikia kilele Mei 9 mwaka huu, ambapo wakulima hao wanatarajiwa kufundishwa mbinu na teknolojia mbalimbali za kilimo cha kisasa.

Mratibu wa maonyesho ya kilimo Biashara kutoka Tari, Leonard Sabula, alisema taasisi mbalimbali zimeshaanza kuandaa mashamba darasa kwa ajili ya kuwafundisha wakulima watakaohudhuria maonyesho hayo.

Alisema maonyesho hayo yatafanyika katika mashamba ya taasisi hiyo yaliyopo katika eneo la Uyole pembezoni mwa Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) na hivyo ni rahisi kufikika na kila anayetaka kwenda kujifunza.

"Maonyesho haya kwa mara ya kwanza yalifanyika mwaka jana na yalileta mafanikio makubwa ambayo yameleta hamasa kwa taasisi nyingi zaidi kuja kuleta teknolojia zao hapa na ni matarajio yetu kuwa wakulima wengi watanufaika," alisema Sabula.

Alisema wanaendelea kusajiri wakulima na taasisi mbalimbali zitakazokuwa tayari kufanya maonyesho hayo ili kuhakikisha kuwa wakulima wanazalisha kwa tija.

Aliwataka wananchi wa mikoa hiyo ya Kanda ya Nyanda za Juu kusini kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kujifunza teknolojia zitakazokuwa zinaonyeshwa ili waongeze uzalishaji.

Kaimu Mkurugenzi wa Tari Uyole, Dk. Ndabhemeye Mlengera, alizitaka taasisi ambazo ni wadau wa kilimo ambazo zitashiriki maonyesho hayo kutangaza bidhaa zao kwa wakulima na kuhamasisha wananchi kunufaika na fursa zilizopo.

Alisema maonyesho hayo ni ya kimataifa kwa maelezo kuwa kuna baadhi ya taasisi zilizothibitisha kushiriki zinatoka nje ya nchi na hivyo akawataka wananchi kuhudhuria kuanzia hatua za awali mpaka wakati wa kilele ambapo vipando vilivyoandaliwa vitakuwa vinavunwa.

Alisema matarajio yao kwa sasa ni kuhakikisha hali ya mavuno kwenye mashamba ya wakulima inabadilika na kuwa bora kuliko ilivyo kwa sasa ambapo baadhi wanavuna chini ya kiwango.

Alisisitiza kuwa maonyesho hayo ni bure na hivyo wakulima wanatakiwa wasiogope kujitokeza wakidhani pengine watakuwa wanatozwa kiingilio kama inavyokuwa kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane.

# Mbarali yahimizwa kuboresha zahanati, vituo afya pembezoni

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, imetakiwa kuboresha zahanati na vituo vya afya vilivyopo pembezoni kwa lengo la kusogeza huduma za afya kwa wananchi na kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali mpya ya wilaya ambayo miundombinu yake haijakamilika.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapunduzi (CCM) mkoa wa Mbeya ambayo ilitembelea miradi kadhaa ya maendeleo wilayani humo kwa lengo la kukagua hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa ilani ya mwaka 2015 hadi 2020.

Akizungumza kwenye majumuisho ya ziara hiyo, Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Solomon Itunda, alisema kuwa ili kusogeza huduma za afya kwa wananchi, ni lazima zahanati na vituo vya afya vilivyo pembezoni viboreshwe kwa kuwekewa miundombinu mizuri pamoja na wahudumu wa afya wa kutosha.

"Kamati yetu inashauri boresheni zahanati na vituo vya afya hasa vilivyo pembezoni mwa wilaya kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma za afya, kwa sasa wananchi wanapata taabu ya kufuata mbali huduma hizo kutokana na mazingira duni yaliyopo kwenye zahanati na vituo vya afya vilivyo karibu na makazi yao," alisema Itunda.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa wanaofika katika Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya kupata huduma za afya ambazo zingeweza kutolewa kwenye vituo vya afya vilivyo kwenye maeneo yao.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Abbas Kitalima, alisema miundombinu ya hospitali ya wilaya hasa majengo bado haijakamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

Alisema Sh. milioni 487 zinahitajika ili kukamilisha majengo yote ya hospitali ya wilaya na kuweka miundombinu mingine muhimu inayohitajika wakati wa utoaji wa huduma za afya kwa wagonjwa.

Hata hivyo, alisema kuwa Serikali Kuu imeahidi kutoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo na kudai kuwa fedha hizo zitakapowasili majengo yote yatakamilishwa na huduma zitaanza kutolewa hospitalini hapo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliitaka halmashauri hiyo ya Mbarali kutenga maeneo ya kutosha kwenye zahanati na vituo vya afya kwa ajili ya maendeleo endelevu ya baadaye.

Alisema serikali inao mpango wa kuboresha sekta ya afya nchi nzima, hivyo suala la upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji kwenye sekta hiyo ni changamoto ambayo inaweza kujitokeza katika siku za usoni, hivyo akaitaka halmashauri hiyo kuanza maandalizi ya upatikanaji wa maeneo hayo kuanzia sasa.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliitaka serikali kukamilisha ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Mbarali haraka ili wananchi waanze kupata huduma kama ilivyokusudiwa.




Mafundi wakiendelea kuchora alama za kuvuka watembea kwa miguu maarufu kama Pundamilia katika Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia, eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wajasiriamali wachangamkia NSSF

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

JUMLA ya wanachama 3,493 wameunganishwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) mkoani Mbeya kati ya mwaka 2018-19 na kuwa na wanachama wengi ambao wajasiriamali hususan waendesha pikipiki, bajaji, daladala na mama lishe.

Meneja wa mfuko huo mkoa wa Mbeya, Nurdin Mruma, alisema jana kuwa mbali na jitihada hizo pia kumekuwa na ongezeko la wanachama wanaojisajili na mfuko huo na kuwa kati ya mwezi Julai, mwaka 2019 hadi Desemba 2019 kulikuwa na wanachama wapya waliojiunga mfuko huo wanaofikia 2,810.

Alisema wengi wa wanachama waliojiunga na mfuko huo ni wajasiriamali licha ya kuwapo kwa wafanyakazi wa serikali na kuongeza kuwa jitihada hizo zinatokana na mwamko wa wananchi walio katika sekta binafsi kutambua manufaa ya mfuko huo wa NSSF.

Mruma alisema malengo ya mfuko huo kwa mkoa wa Mbeya ifikapo Juni, unakusudia kusajili wanachama 5,640 ikiwa makusudio yao ni kuwasajili wajasiriamali ambao wataweza kunufaika na mfuko huo kutokana na huduma zinazotolewa.

Alisema mfuko huo unakusudia kuwawezesha wanachama wa sekta isiyo rasmi kupata mafao ya pensheni na pia kunufaika na huduma za muda mfupi zikiwamo za fao la uzazi, pamoja na fao la kupata matibabu.

Alibainisha kuwa sheria ya mfuko wa NSSF inataka wanachama kutoka sekta isiyo rasmi wapewe kipaumbele kama wanachama wanaochangia kwa hiari na kuwa jitihada zinaendelea kutekelezwa na mfuko huo kwa lengo la kuhakikisha wanachama wengi zaidi wanaendelea kujiunga.

Mruma alisema NSSF ni moja ya mifuko ya jamii ambayo inawanachama wengi ambao wamekuwa wakichangia katika mfuko huo wakiwamo watumishi wa taasisi ambao wamekuwa wakilipwa fedha baada ya muda mrefu (pensheni) na wanachama ambao ni wachangiaji wa hiari kutoka sekta binafsi.

"Wachangiaji wa muda mrefu wamekuwa wakinufaika kwa kupata pesheni ya uzeeni,ulemavu na urithi na pensheni hii imekuwa ni msaada mkubwa kwao katika kujikimu katika maisha yao ya kila siku baada ya kufika muda wa uzeeni," alisema.

Aliwataka wanachama kujenga utamaduni wa kuhakiki taarifa kila wakati ili kuboresha taarifa zao kwa lengo la kuepukana na usumbufu wakati wa kujipatia mafao mbalimbali ndani ya shirika hilo.





# Vikundi vyapata mkopo mil. 65/-

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa mikopo ya Sh. milioni 65.13 kwa vikundi 18 vilivyoko kata ya Kilimani ndani ya miaka minne ili kukuza miradi yao.

Diwani ya Kata hiyo, Neema Mwaluko, alisema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa kazi na shughuli za maendeleo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika mwisho mwa wiki.

Alisema hatua hiyo imewawezesha wananchi kiuchumi katika kipindi cha miaka mine, ambapo wamepata pia elimu ya namna bora ya kukuza ya biashara na kuziboresha.

Mwaluko alibainisha kuwa walitoa elimu ya kuunda vikundi kwa makundi mbalimbali ya eneo hilo na kufanikiwa kuundwa kwa vikundi 43 ambapo vimepata usajili.

Diwani huyo alisema kati ya vikundi hivyo, 18 ndivyo vilivyopatiwa mikopo.

Alivitaja baadhi ya vikundi hivyo vilivyopata mikopo hiyo kuwa ni Six Power, Domshine, Jecafa, Shaloom, Wachapakazi, Uwakido, Vicoba Police Line, Amka Fanyakazi, Jiamini, TMV, Kiviki, Uwawachi na Dom Care.

Pamoja na hayo, alisema wametatua migogoro mikubwa ya ardhi katika Mtaa wa Chinyoya iliyodumu kwa miaka 20 kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa.

"Kwa sasa upimaji na uboreshaji wa mtaa huo unaendelea vizuri na tumefanikiwa kutenga maeneo ya ujenzi wa huduma za jamii kama hospitali, shule na soko," alisema.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Semindu Michael, aliwataka viongozi wengine kutoa taarifa zao za utekelezaji kwa wananchi ili wajue mambo yaliyoahidiwa na kutekelezwa.

"Kuna wakati serikali tumekuwa tukilaumiwa kuwa hatufanyi kitu kumbe watu wamekalia taarifa nzuri za maendeleo yaliyofanyika katika maeneo yao. Nawaomba kila kiongozi kwenye eneo lake ahakikishe anaandaa taarifa yake ya utendaji ili wananchi wazijue," alisema.

Michael alisema utaratibu wa kutoa taarifa kwenye mikutano ya hadhara unasaidia wananchi kujua malengo ya maendeleo yanayotarajiwa katika eneo husika.

**"Kwa sasa upimaji na uboreshaji wa mtaa huo unaendelea vizuri na tumefanikiwa kutenga maeneo ya ujenzi wa huduma za jamii kama hospitali, shule na soko," alisema.**

# Jafo ataka ujenzi hospitali saa 24

Na Augusta Njoji, CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, ameliagiza Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (Suma JKT) kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Uhuru inayojengwa Chamwino, mkoani Dodoma.

Ujenzi huo unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 3.99 hadi kukamilika kwake.

Akizungumza jana alipokagua maendeleo ya ujenzi huo, Waziri Jafo alisema mkandarasi huyo anapaswa kufanya kazi ili akamilishe kwa muda uliopangwa.

"Ujenzi unatakiwa kukamilika Mei, mwaka huu, hivyo naagiza mfanye kazi usiku na mchana Suma JKT. Fungeni taa kubwa na mwongeze nguvu kazi ili ukamilike kwa wakati ujenzi," alisisitiza.

Alisema ujenzi wa hospitali hiyo utarahisisha upatikanaji huduma kwa wananchi wa Chamwino na wasafiri wanaotumika barabara ya Dodoma-Dar es Salaam kutokana na kujengwa karibu na barabara.

Alimtaka kuhakikisha anakamilisha mradi huo kwa viwango vinavyokubalika na serikali.

Kadhalika, Jafo aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuhakikisha unasimamia ujenzi huo kwa weledi, ili gharama zitakazotumika ziendane na majengo yanayojengwa.

"Mkuu wa Mkoa na viongozi wote wa halmashauri hakikisheni vifaa vinapatikana kwa wakati na mnasimamia kila wakati na kila hatua ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika," alisema.

Aidha, Jafo alitaka viongozi hao kuhakikisha vifaa vinapatikana kwa wakati ili mkandarasi asipate shida kukamilisha ujenzi kwa muda uliopangwa.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Dk. Eusebius Kessy, alisema ujenzi huo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa Novemba, 2018 na alitoa Sh. milioni 995.18 ambazo zilitengwa kwa ajili ya sherehe za uhuru mwaka 2018, na kuongeza kiasi cha Sh. bilioni 2.35 zilizotokana na gawio la hisa kwa kampuni ya simu ya Airtel.

Alisema awali ujenzi huo ulianza Oktoba 26, 2019 katika kitongoji cha Maduma, lakini baadaye walihamisha na kuanza kujenga upya katika eneo la Buigiri kutokana na maelekezo ya Rais.

"Katika eneo hili la Buigiri, ujenzi ulianza Novemba bila kuathiri taratibu za mkataba wa awali na ujenzi unatumia mfumo wa 'force account'. Mkandarasi wa ujenzi ni Suma JKT na mhandisi mshauri ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)," alisema.



Waziri Kivuli wa Elimu (Chadema), Susan Lyimo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, kuhusu ukosefu wa vyumba ya madarasa vya kujiunga kidato cha kwanza kwenye shule nyingi za serikali. Kushoto ni Waziri Kivuli wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, Ruth Mollel na Katibu Mkuu Bawacha, Grace Tendega. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Tanesco yawatoa hofu wananchi

Na Renatha Msungu, DODOMA

KUTOKANA na wakazi wa kijiji cha Chilungulu kulalamika mkandarasi kupitisha nguzo za umeme kwenye mashamba yao, Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) Wilaya ya Bahi, limesema liko tayari kuhamisha nguzo hizo endapo mkandarasi atakuwa ameziweka kinyume cha maelekezo.

Meneja wa Tanesco wilayani humo, Kitila Bryceson alisema hayo jana alipokuwa akijibu malalamiko ya wakazi hao ambao walidai kuwa baadhi ya nguzo zimewekwa kinyume cha makubaliano.

Meneja huyo alisema hakuna kitakachoshindikana na kwamba nguzo hizo zitaendelea kuwekwa kwa mpangilio sahihi kulingana na mita zilizowekwa bila ya kuwaathiri wananchi wa eneo husika.

"Nawaomba wananchi wa kijiji cha Chilugulu hakuna atakayeathiriwa na uwekaji wa nguzo hizo kwa ajili ya kuwapelekea wanakijiji umeme," alisema Bryceson.


Meneja huyo alisema lengo lao ni wananchi wote wapate umeme ili kuchochea maendeleo kwenye maeneo wanayoishi.

Hata hivyo, alisema tayari suala lao linaendelea kupatiwa ufumbuzi hivyo wakazi wa eneo hilo wasiwe na hofu na mkandarasi wa kampuni ya A&Z ambaye anahusika kuweka nguzo hizo kwa kuwa hatavuka mipaka iliyowekwa.

Naye Mwenyekiti wa kitongoji cha Chilungulu, Mambeja Meja, alisema mkandarasi huyo amekuwa akitoa lugha chafu kwa wananchi pale wanapouliza sababu za kuingiza nguzo zaidi ya mita 15 zilizopangwa kwenye mashamba yao.

"Tunaomba Tanesco endeleeni kumsimamia huyu mkandarasi ili anapokosea apewe maelekezo kulingana na bikoni zilizowekwa," alisema Meja.

Alisema wanakijiji wanahitaji maendeleo lakini sio kuchukua ardhi yote kuweka nguzo kiholela.



**HABARI ZANZIBAR**

# Waziri afagilia TCC kusaidia wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma N'hunga, amesema kupatiwa nyenzo za kufanyia kazi kwa watu wenye ulemavu kutawaweza kupata kipato ili kuondoa dhana potofu iliyopo kwenye jamii kwamba watu hao ni wa kuomba.

Akizungumza jana kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rias wakati wa ugawaji wa vifaa visaidizi kwa watu wenye ulemavu vilivyotolewa na Kampuni ya Sigara Tanzania, alisema serikali itaendelea kutoa fursa mbalimbali kwa watu wenye ulemavu zikiwamo za ajira na kutoa mafunzo kwa makundi hayo ili kuwasaidia bila ya kujali ulemavu wao.

Alisema kuwa serikali itaendelea kushirikiana na kampuni na wadau wa maendeleo wenye lengo la kuleta maendeleo hasa kwa kuhusisha makundi ya watu wenye ulemavu ili kuona wao ni sehemu ikiwamo kuwapatia nyezo za kufanyia kazi.

"Inatia moyo kuona bado kuna viongozi wa makampuni yenye mioyo ya kizalendo ambayo yanasaidia makundi haya bila ya kujali hali walizonazo kwani walemavu kwa kuamini wanauwezo wa kufanyakazi kama watapatiwa visaidizi," alisema.

Aliushukuru uongozi wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC) kwa kushirikiana na Idara ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar na Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu (SHIJIWAZA) kwa mchango wao waliotoa kutambua mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Aliwataka waliopatiwa vifaa hivyo, kuvitumia kama ilivyokusudiwa ili lengo lililokusudiwa lifikiwe hasa katika shughuli zitakazo waletea maendeleo.

Alieleza kuwa kuwasisitiza kuwa ulemavu sio umaskini, na kwamba ukiwa na kifaa cha kusaidia wanaweza kufanya kazi.

Naye Mkurugenzi wa Sheria wa kampuni ya TCC, Godson Killiza, alisema wamefarijika na mapokezi makubwa waliyoyapata kutoka kwa viongozi hao na kuahidi kuendelea kusaidia watu wenye ulemavu Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa TCC, Michal Bachan, alisema kuwa utoaji huo wa visaidizi unaingia katika awamu ya saba kwa upande wa Zanzibar ambapo awamu nyengine zilikuwa katika mikoa ya Pwani, Dar es Salam, Dodoma, Morogoro, Ruvuma na Geita ambapo jumla ya watu 1,800 walipatiwa visaidizi hivyo.

Alisema msaada huo ni miongoni mwa marejesho ya fedha zinazopatikana katika kampuni hiyo ambapo wamekuwa na lengo la kutoa misaada mbalimbali katika jamii.

Mwenyekiti wa SHIJUWAZA, Mwandawa Khamis Mohamed, aliomba serikali kuangalia sheria ya utoaji wa huduma zinazohusu kampuni kama hizo na kuzipitia upya sheria hizo hasa kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18.



Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu Zanzibar, Simai Mohamed Said, akizungumza katika mkutano wa wanachama na wananchi wa Wadi ya Bungi, Mkoa wa Kusini Unguja, akielezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika jimbo lake kwenye mkutano juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# SMZ yaahidi ushirikiano matibabu kwa wananchi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, amesema serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na nchi mbalimbali ili kuwapatia huduma za matibabu kwa wananchi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo juzi katika Shule ya Afya Mbweni wakati wa Mkutano wa Madaktari wa Cuba na Zanzibar walipowasilisha taarifa za utafiti wao za magonjwa mbalimbali waliyoyafanyia uchunguzi ambayo yameonekana kushamiri duniani na kupatiwa huduma za matibabu.

Alisema Tanzania ina ushirikiano makubwa na Serikali ya Cuba kwa muda mrefu kwa lengo la kuboresha huduma za tiba kwa maradhi sugu ambayo yanaikabili jamii.

Aisema kuwa utafiti unaonyesha ugunduzi wa tiba, ambazo zitasaidia wagonjwa kurudia katika hali zao za kawaida pamoja na kuepukana na ulemavu usiotarajiwa hasa kwa wale wagonjwa wa kisukari.

Alieleza kuongezeka kwa wataalamu nchini kutoka katika nchi tofauti kutasaidia ushirikiano wa kimatibabu na kuongeza ujuzi kwa madaktari wazalendo jambo ambalo litasaidia kuimarisha huduma za kimatibabu nchini.

Naye Mkuu wa Shule ya Afya Suza, Salum Seif Salum, akielezea utafiti kuhusu kudhibiti mazalia ya mbu, alisema kuwa ongezeko kubwa la mazalio ya mbu linatokana na uchafu wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya mji hasa katika baadhi ya mitaa ambayo hutuama maji na kusababisha mazalio ya mbu.

"Wizara ya Afya kwenye kitengo chetu cha kuondosha maradhi kinachukua juhudi za kuwaangamiza mbu hao, ambao husababisha maradhi ya malaria, homa ya manjano na pia homa ya kinyungu'nya, na kuhakikisha wanapotea kabisa," alisema Dk. Salum.

Msaidizi wa Shule ya Afya Mbweni, Amina Abdulkadir Ali, wakati akiwasilisha mada ya uuguzi na wakunga, alisema inapaswa wauguzi kuzingatia mambo matatu muhimu katika kutoa matibabu kwa wagonjwa.

Mambo hayo ni kichwa, mikono na moyo wa huruma na kutumia lugha nzuri wakati wa kuhudumia wagonjwa.

# Balozi Iddi aeleza dawa ajira vijana

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wizara inayosimamia masuala ya vijana inapaswa kuratibu na kusimamia vyema masuala ya maendeleo yao ili kubaini vilivyochangamoto za upatikanaji wa ajira unaozingatia zaidi ujuzi, vipaji pamoja na juhudi zao katika taaluma.

Alisema jukumu la Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni kuhakikisha mahitaji na matarajio ya vijana kisekta yanajitosheleza katika miongozo inayokwenda sambamba na utekelezaji wa agenda ya Maendeleo Endelevu ya Dunia kufikia mwaka 2030.

Akizindua programu ya ajira kwa vijana na ugawaji wa vifaa kwa vikundi vya kiuchumi vya vijana ngazi ya wilaya huko Kikwajuni Mjini Zanzibar.

Balozi Iddi alisema ili kijana aweze kuuzika hanabudi kujikita zaidi katika kutafuta elimu na ujuzi kulingana na soko la ajira liliyopo.

Balozi Iddi alisema serikali iko katika hatua ya kuandaa miongozo mipya ya maendeleo ngazi ya taifa ikiwamo dira ya mwaka 2025, mwelekeo wa sera ya kufikia mwaka 2030 na ilani ya uchaguzi ya kufikia mwaka 2025 lengo likiwa kuongeza uchumi wa Taifa kupitia nguvu kazi ya vijana.

Alisema utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana ni miongoni mwa jitihada za serikali kutimiza dhamira yake ya kukuza ujuzi kwa vijana wanaokadiriwa kufikia asilimia 36.2 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 ili kuchochea maendeleo na ujenzi wa uchumi wa viwanda kufikia uchumi wa kati.

Alisema serikali inaielewa vyema changamoto kubwa ya ufinyu wa ajira kwa vijana kupitia hali halisi inayoonekana wazi mitaani pamoja na utafiti mbalimbali uliofanywa na wataalamu wa takwimu kitaifa na kisekta ndani na nje ya nchi.

Akitoa taarifa ya kitaalamu juu ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana Katibu Mkuu Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Omar Hassan Omar (King), alisema programu hiyo ni mfumo wa jitihada za serikali za kuwajengea uwezo wa kujitegemea vijana nchini.

Omar alisema jumla ya vijana 3,051 katika visiwa vya Unguja na Pemba watafaidika na programu hiyo ya ajira kwa vijana katika maeneo ya miradi ya kilimo, viwanda vidogo na ujasiriamali ambapo serikali imeshatenge jumla ya Sh. bilioni 12 zitakazoratibiwa na Wizara ya Vijana.

# Waziri: Kibano cha mikutano vyama vya siasa kinaendelea

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amesema msimamo wa kuzuia mikutano yote ya siasa isiyofuata utaratibu upo pale pale.

Masauni aliyasema hayo jana na kusisitiza kuwa muda wa siasa ukifika watu wataruhusiwa kuendesha mikutano yenye lengo la kueleza kwa wananchi walichokifanya kwa muda waliopewa nafasi baada ya kuchaguliwa na kuteuliwa katika nafasi mbalimbali.

Alieleza hayo wakati akitoa taarifa ya usalama na uhalifu visiwani Zanzibar katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka jana wakati akihojiwa na kituo kimoja cha redio.

Masauni alizungumzia pia mauaji na kusema mwaka 2018 jumla ya matukio 40 ya mauaji yalitokea tofauti na mwaka jana ambapo matukio hayo yalipungua na kufikia 35, huku akisema kazi imefanyika kuyadhibiti hadi kufikia idadi hiyo.

Alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi na pande zote zinazohusika zimeanza harakati kuweza kudhibiti matukio hayo yanayosababishwa na sababu mbalimbali ikiwamo imani za kishirikina.

"Matukio ya udhalilishaji kwa mwaka 2019 yaliongezeka baada ya matukio 35 kuripotiwa tofauti na mwaka 2018 ambapo kulikuwa na matukio 15 na jitihada mbalimbali zinafanyika ikiwepo utolewaji elimu kupitia askari na Ofisi ya Polisi Jamii na wadau huku sababu mbalimbali ikiwamo imani za kishirikina.

Alitaja sababu zingine jamii kukosa elimu ya kutosha kuhusu madhara ya makosa hayo, watu kushindwa kuzuia matamanio, ukuaji wa matumizi ya mitandao, kutotolewa adhabu stahiki na kwa muda muafaka kwa wakosaji na kuwapo mmomonyoko wa maadili zikitajwa ndiyo sababu.

Kuhusu matukio ya wizi wa watoto wachanga, Masauni alisema mwaka 2018 yalitokea matukio mawili na mwaka jana hakukuwa na tukio.

"Jeshi liko makini katika kudhibiti mtandao wa biashara ya dawa za kulevya ambayo tumeona siku za nyuma vijana wengi ambao ni nguvu kazi ya taifa wakiaribika, kuna mpango maalumu uko katika utekelezaji na tayari umeanza kutoa matokeo chanya ambapo mwaka 2019 watuhumiwa 496 walikamatwa na tulikamata Cocaine gramu 960.65, Heroine kilogramu 10.2 na gramu 806.102 imekamatwa, bangi kilogramu 659.6 na gramu 649.775 ilikamatwa."

Alisema walikamata mirungi kilogramu 10.6 na gramu 096.648 pamoja na vidonge vya Valium gramu 10.30.

Kuhusu usalama barabarani, alisema mwaka 2018 makosa yaliyoripotiwa yalikuwa ni 31,524 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo makosa yalikuwa ni 23,166.

Alisema makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha, wizi wa magari, wizi wa mali za serikali kuu, wizi wa mifugo, ajali za moto, rushwa na wizi yameendelea kushuka.

"Makosa ya rushwa mwaka 2018 ni tukio moja tu liliripotiwa na mwaka 2019 hakukua na tukio likihusisha utoaji na upokeaji rushwa. Wizi wa magari pia mwaka 2018, magari matano yaliibiwa na mwaka 2019 yaliibiwa mawili," alisema.




Mkuu wa Masoko wa Tigo, William Mpinga, akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, katika uzinduzi wa kampeni mpya ya kampuni hiyo, ijulikanayo kama 'Ujanja Ni', yenye lengo la kuwapa wateja wake thamani ya pesa zao kila wanapotumia bidhaa za Tigo. Kulia ni Kaimu Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, David Umoh. **PICHA: JOHN BADI**

## Zungu ahamasisha Ilala kujiandikisha

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amewataka wakazi wa Jimbo la Ilala kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura.

Zungu aliyasema hayo jana katika Kata ya Upanga Mashariki wakati wa kikao kilichoitishwa na Diwani wa Kata hiyo, Sultan Salim, kilichokuwa kikisikiliza kero za wananchi.

"Kazi ya kuboresha daftari la kudumu la mpigakura katika mkoa wetu linatarajia kuanza hivi karibuni, nawaomba wananchi wangu wa Jimbo la Ilala wote mshiriki kujiandikisha kwa ajili ya kuchagua viongozi wenu katika uchaguzi ujao mwaka huu, kupiga kura ni haki ya kila mmoja na ili mpate haki hiyo ni lazima kujiandikisha, na ni haki yenu kidemokrasia," alisema Zungu.

Aliwata pia vijana ambao walikuwa hawajatimiza sifa ya kupiga kura ambao kwa sasa wana sifa hiyo kuitumia haki hiyo kwa kuhakikisha wanajiandikisha na kupiga kura mwaka huu.

"Nafahamu kuna vijana ambao walikuwa hawajajiandikisha kwa sababu ya kukosa sifa kutokana na umri wao, lakini kwa sasa wametimiza umri huo, wasiipoteze fursa hiyo, wajitokeze kwa wingi kujiandikisha ili siku ikifika wakapige kura, na wale waliopoteza vitambulisho vyao na wao wajiandikishe wakati ukifika," alisema Zungu.

Pia alizitaka kamati za mazingira na za ulinzi zinazotokana na serikali za mitaa, zilizopo katika jimbo hilo la Ilala kuwajibika na kufanya kazi kwa weledi katika kutatua changamoto zilizopo.

Diwani Salim akielezea changamoto yake kwa Zungu, alisema kilio kikubwa katika kata yake ni ukosefu wa madawati kwa baadhi ya shule.

**"Nafahamu kuna vijana ambao walikuwa hawajajiandikisha kwa sababu ya kukosa sifa kutokana na umri wao, lakini kwa sasa wametimiza umri huo, wasiipoteze fursa hiyo, wajitokeze kwa wingi kujiandikisha ili siku ikifika wakapige kura, na wale waliopoteza vitambulisho vyao na wao wajiandikishe wakati ukifika," alisema Zungu.**

# Sukari guru kuzalisha nishati pombe ya kupikia vyakula Dar

**Na Gaudensia Mngumi**

KAZI za kibunifu zinazofanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwamo Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), zinaanzisha mpango wa kutumia sukari guru kuzalisha nishati ya kupikia nyumbani.

Mradi huo unatarajiwa kuanzia Dar es Salaam ili kupunguza matumizi makubwa ya mkaa na kuni, unaotekeleza maelfu ya hekari za misitu nchini.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam wakati Ofisi za Umoja wa Mataifa (UN), Mtandao wa Ubunifu wa UN (UNIN) na Kituo cha Ubunifu cha Mpango wa Chakula wa Duniani (WFP), ulipoandaa usiku wa ubunifu wa mashirika ya UN nchini na kuonyesha kazi mbalimbali na jinsi ubunifu ulivyo mwarobaini wa kumaliza changamoto za jamii.

Victor Akim, kutoka UNIDO, akielezea ubunifu wa kuhamasisha kutumia sukari guru kutengeneza nishati mbadala ya kupikia nyumbani alisema mradi utatumia guru (molasesi) kutengeneza pombe ('bioethanol') na kwamba majaribio yanaanzia Tabata na Ilala kwa kusambaza majiko 110,000 kwa kaya za eneo hilo kwa majaribio.

"Ubunifu na teknolojia hii unalenga kushirikiana na sekta binafsi wazalishaji wa sukari kutumia molasesi kutengeneza bioethanol - nishati mbadala. Lakini siyo sukari guru pekee tunalenga pia kutumia mabibo ya korosho na mabaki ya katani," anaeleza Akim alipowasilisha wazo la ubunifu kutoka UNIDO.

Kaimu Mratibu, Mkazi wa UN na Mwakilishi wa WFP nchini, Michael Dunford, akizungumza kwenye usiku wa ubunifu alisema:

"Mazoea ya kutekeleza majukumu kwa njia zilizozoeleka hautatusaidia kufikisha kwenye malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) yatupasa kuwa wabunifu, kufikiria ufumbuzi wa changamoto za siku zijazo na kutoogopa kujaribu mambo mapya."

Dunford alihimiza utamaduni na kujenga mazingira wezeshi ya kuleta ubunifu na kufanya mambo mapya akisema ni muhimu katika kuibua njia mpya za utendaji katika UN. Ili kufanikisha azma hiyo mashirika mengi ya UN yameunda timu za kuhamasisha ubunifu kidunia na katika mataifa wanapofanyia kazi.

Alisema kwa UN Tanzania harakati za ubunifu zinaendeshwa na Kituo cha Ubunifu cha WFP na Mtandao wa Ubunifu wa UN -UNIN na kwamba kupitia safari ya ubunifu maofisa 30 kutoka mashirika 11 ya UN wamejifunza na kutumia njia mbalimbali za ubunifu zilizoainisha kikamilifu njia bora za kutatua matatizo kama vile , kuibua mbinu za kufanya mawasiliano yenye ufanisi zaidi na wadau na wahisani wa UN. Je, tutafanya nini ili kupata nishati endelevu kwa ajili ya watu wanaoishi katika kambi za wakimbizi?

## HABARI KIMATAIFA

# Ndege yaanguka barabara ya magari

**TAIRAN,** Iran

NDEGE ya abiria ya Iran imejikuta ikitua kwenye barabara ya magari baada ya kuteleza uwanja wa ndege ilipokuwa ikitua.

Abiria wawili kati ya 136 waliokuwa wakisubiri ndege hiyo walipata majeraha ya miguu kutokana na kisa hicho katika mji wa Mahshahr, kulingana na maofisa wa afya.

Ndege hiyo ya kampuni ya Caspian iliondoka mjini Tehran na matairi yake hayakujitokeza kabisa wakati ilipotarajiwa kutua.

**Ripota mmoja ambaye alikuwa ndani ya ndege hiyo alisema kwamba matairi ya nyuma yaliharibika hivyo iliteleza bila matairi yake.**

Picha za abiria waliokuwa wakitoka katika ndege hiyo zilichapishwa katika mitandao ya kijamii.

Runinga ya serikali ilinukuu maofisa wa usafiri wa angani wakisema kwamba rubani aliishusha ndege hiyo kwa kuchelewa hivyo akakosa barabara ya ndege.

Ripota mmoja ambaye alikuwa ndani ya ndege hiyo alisema kwamba matairi ya nyuma yaliharibika hivyo iliteleza bila matairi yake.

Msemaji wa Shirika la Udhibiti wa Safari za Angani, Reza Jafarzadeh, alikiambia chombo cha habari cha Isna News kwamba ndege hiyo iliteleza kutoka katika barabara yake siku ya Jumatatu alfajiri na kwamba uchunguzi unaendelea.

Iran ina rekodi mbaya ya safari za ndege, watu 66 walifariki katika ajali ya ndege mwezi Februari, mwaka jana huku makumi wakifariki wakati ndege ya IranAir ilipovunjika vipande vipande baada ya kuanguka mwaka 2011.

Muungano wa Ulaya umepiga marufuku kampuni mbili za ndege kutotumia anga yake kutokana na wasiwasi wa kiusalama.

Iran ilikuwa imepanga kuimarisha ndege zake zilizozeeka baada ya vikwazo vya miaka mingi kuondolewa ikiwa ni miongoni mwa makubaliano ya mkataba wa kinyuklia wa 2015 na mataifa yenye uwezo mkubwa.

Hata hivyo wizara ya fedha nchini Marekani ilifutilia mbali leseni ya kampuni kuuzia Iran ndege za abiria baada ya Rais Donald Trump kujiondoa katika makubaliano hayo 2018. **BBC**



Wazee wa Kiyahudi kutoka Israel, Marekani, Australia, Peru, Urusi na Slovania, wakiwa kambi ya mauti ya Auschwitz-Birkenau, eneo ambalo miaka 75 iliyopita lilikuwa alama ya dhuluma kubwa dhidi ya binadamu. **PICHA: REUTERS**

## Ufaransa kuwarejesha raia wake waishio Wuhan, China

**PARIS,** Ufaransa

SERIKALI ya Ufaransa kupitia Waziri wake wa Afya, Agnes Buzyn, imetangaza kuwa itawarudisha nyumbani raia wake waishio mji wa Wuhan, kitovu cha mlipuko wa ugonjwa Corona, nchini China, katikati ya wiki ijayo.

"Mchakato wa kuwarudisha nyumbani raia wetu waishio Wuhan, nchini China, utafanyika "katikati ya wiki" kwa "makubaliano na viongozi wa China," Waziri wa Afya wa Ufaransa alisema.

Alisema mchakato huo utafanyika chini ya usimamizi wa "timu maalumu ya matabibu". Watakapowasili, watu hao "watabaki kwenye eneo la mapokezi kwa muda wa siku 14", kipindi kinacholingana na kipindi cha kuonekana dalili za mtu aliyeambukizwa virusi vya ugonjwa mpya unaofahamika kama Corona. Waziri Buzyn amekadiria kuwa idadi ya watu wanaohusika katika mchakato huo inaweza "kuanzia zaidi ya kumi hadi zaidi ya mia moja". Maofisa kwenye balozi zetu nchini China "wameanza kuorodhesha"

Wale wanaotaka kurudi, wengine wanaweza kusita kwa sababu ya kipindi cha karantini ambacho kimewekwa kuzuia. "Kusambaa kwa virusi katika ardhi ya China", Waziri Buzyn alisema. **RFI**

# Wazimbabwe wapinga Jaji wa Uganda kutoa mafunzo

**HARARE,** Zimbabwe

RAIA wa Zimbabwe wameandamana baada ya Jaji Mkuu nchini humo kumualika Jaji wa Uganda kutoa mafunzo kwa mahakimu wa Zimbambwe kuhusu namna ya kukabiliana na ufisadi.

Taarifa hizo hazikupokelewa vizuri na raia wa Zimbabwe katika mitandao ya kijamii ambao walisema kwamba Uganda siyo nchi sahihi ya kujifunza.

"Tafadhali muache kuharibu rasilimali za wananchi. Je, tunahitaji usaidizi wa Uganda kukabiliana na ufisadi Zimbambwe" Leonard Koni ameandika.

"Uganda, kukabiliana na ufisadi... Mulifanikiwa vipi kuchanganya maneno hayo mawili NICK? Kwanza tazama nchi ambayo mnaiomba ushauri na usaidizi," TB Mandlazi ameandika.

"Uganda sio mfano mzuri kwa nchi zenye kukabiliana na ufisadi pengine Rwanda, Singapore, Netherlands, Malaysia na kadhalika wala siyo Museveni.

"Bado tuko mbali sana katika suala la kuanza kupiga vita ufisadi," Takudzwa Munangwa ameandika.

"Lakini kwa nini Uganda na wala sio Rwanda au Kenya ama Afrika Kusini," Nelson Tuwadya aliuliza.

"Mataifa ya Afrika ambayo kiwango chao cha ufisadi kiko chini ni Seychelles, Botswana, Cape Verde, Rwanda, Mauritius, Sao Tome and Principe, Namibia na Senegal. Kulingana na orodha ya makadirio ya kiwango cha ufisadi iliyotolewa na shirika la Transparency International," Tarrysnun ameandika.

Jaji Mkuu wa Zimbambwe, Luke Malaba, aliwaambia waandishi wa habari kuwa Hakimu Justice Gidudu, kiongozi wa jopo la kukabiliana na ufisadi Uganda, atatoa mafunzo ya wiki moja katika mji mkuu wa Zimbambwe, Harare.

Jaji Malaba alisema Zimbambwe ina mengi ya kujifunza kutoka kwa Uganda ambayo imewashtaki na kuwafunga watu jela waliopatikana na makosa ya ufisadi kwa miaka mingi tu.

Hatua hiyo imechukuliwa kabla ya kuanzishwa kwa mahakama mpya za kukabiliana ufisadi tu.

Katika hotuba yake ya mwaka wa sheria 2020, Jaji Mkuu Malaba alisema mfumo wa mahakama unaimarisha juhudi za kukabiliana na ufisadi ambako kumeorodheshwa kuwa adui namba moja na Rais Mnangagwa.

Uganda ambayo imekuwa na mahakama maalum za kukabiliana na ufisadi kwa karibia kipindi cha miaka 10 iliyopita, iliorodheshwa kuwa bora zaidi ya Zimbambwe katika orodha ya makadirio ya nchi fisadi na shirika la Transparency International mwaka 2019.

Katika orodha hiyo, Uganda ilikuwa namba 137 kati ya nchi 180 huku Zimbabwe ikiorodheshwa kuwa namba 158.

Lakini nchi jirani za Zimbambwe kama Botswana, Namibia na Afrika Kusini, ziliorodheshwa katika nafasi nzuri zaidi ya Uganda. **BBC**

# Waziri ataka wachimbaji wadogo kupata umeme

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amemtaka Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) wilayani Kahama, King Fokanya, kupeleka umeme kwa wachimbaji wadogo ili waondokane na gharama za uendeshaji katika migodi yao.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa uzinduzi wa nishati ya umeme katika kiwanda cha uchenjuaji wa dhahabu cha Kweji kilichoko kijiji cha Mwabomba wilayani Kahama, huku akibainisha kuwa mpaka sasa kiwanda hicho kimelipa ushuru wa Sh. milioni 37 kwa halmashauri.

Dk. Kalemani alimwagiza meneja huyo kuhakikisha anafanya operesheni sehemu zote zenye wachimbaji wadogo na kuwapelekea umeme kama ilivyo katika mkoa wa Geita ambako migodi midogo 36 imekwishapata huduma hiyo.

"Tunataka wachimbaji wadogo wote nchi nzima wasiendelee kuwa wadogo tena ili uchimbaji wao uwe na manufaa na tija kwenye taifa kama walivyo wachimbaji wengine wakubwa. Lazima tuhakikishe tunawafungia umeme," alisema.

"Hata wachimbaji wakubwa mnaowaona leo Barrick na Acacia nao walianza kuwa wachimbaji wadogo na matumaini ya serikali ni kuona wachimbaji wadogo nchini wanakuwa wawekezaji wakubwa kwa kuwapunguzia gharama za uendeshaji," aliongeza.

Naye Meneja wa Tanesco Mkoa wa Shinyanga, Narowil Sabaya, alisema kuwa Mkoa wa Shinyanga unavijiji 509 kati ya hivyo 171 vimepata umeme na vijiji 318 bado havijapata huduma hiyo.

Alisema Shinyanga ina kata 130 na kati ya hizo, 93 zimefikiwa na huduma ya umeme na 37 bado huku Wilaya ya Kahama ikiwa na vijiji 249 na 59 vimefikiwa hiyo.

Wilaya ya Kishapu, alisema ina kata 29 na vijiji 117, huku kata 22 zimefikiwa na umeme na kata saba zikiwa bado hazijafikiwa huku vijiji 56 vikiwa na nishati hiyo na 61 vikiwa bado.

Mmiliki wa kiwanda cha Kweji, Saidi Kweji, alisema kabla ya kufungiwa nishati ya umeme walikuwa wakitumia mafuta zaidi ya lita 40 kwa siku.



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Siku ya Sheria ambayo itafanyika jijini Dodoma Februari 6 mwaka huu. Kushoto ni Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi na Naibu Msajili wa Mahakama ya Rufani, Eddie Fussi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Lukuvi aja na mwarobaini ucheleweshaji hati ardhi

**Na Munir Shemweta, DODOMA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amekuja na mwarobani wa ucheleweshaji utoaji hati za ardhi.

Katika kulipatia ufumbuzi tatizo hilo, ameagiza karatasi na majalada ya kutunzia kumbukumbu za ardhi, sasa kuchapishwa Chuo cha Ardhi Tabora sambamba na idara za ardhi katika kila halmashauri kupatiwa vifaa vitakavyowezesha uandaliwaji hati za ardhi.

Lukuvi alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya utunzaji kumbukumbu na ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi kwa wataalamu wa sekta ya ardhi kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Singida, Dodoma na Morogoro jijini hapa.

Alisema pamoja na uchapishwaji karatasi na majalada ya utunzaji kumbukumbu za ardhi, kuanzia bajeti ijayo ya serikali, hataki kusikia ofisa ardhi kwenye halmashauri yoyote anatumia fedha zake za mfukoni kununua vifaa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

"Kuanzia sasa karatasi zote tutachapa wenyewe kwenye chuo chetu cha ardhi pale Tabora ili kuepuka ucheleweshaji uliokuwa ukijitokeza halafu nije kuona halmashauri inachelewesha hati kisa karatasi," alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, katika halmashauri kuna wananchi wamekamilisha taratibu zote za kupatiwa hati za ardhi lakini wamekuwa wakicheleweshewa jambo linalosababisha wananchi kukosa hati kwa wakati na kuikosesha serikali mapato kupitia kodi ya pango la ardhi.

"Tatizo maofisa ardhi badala ya kushughulikia majalada ya ardhi wanataka mpaka wawaone wamiliki wake. Usipomwona mpima au ofisa mipango miji basi unaweza kuambiwa eneo lako ni hatarishi au la makaburi, wanataka kula bila kunawa," alisema.

Lukuvi alisema serikali imejipanga vizuri kuhakikisha wananchi hawasumbuki tena kufuatilia hati na yule aliyekamilisha taratibu zote anatakiwa kuipata hati yake ndani ya mwezi mmoja bila gharama yoyote isipokuwa kodi zilizopangwa kwa mujibu wa sheria.

Alibainisha hivi karibuni wizara itaanzisha ofisi za ardhi za mikoa zitakazokuwa na wataalamu wa upimaji, mipango miji, wathamini na usajili na mwananchi hawatakwenda umbali mrefu kuchukua hati na hakuna huduma ya ardhi itakayotolewa kwa kuvuka mkoa mmoja.

Pia Lukuvi amewataka maafisa ardhi kwenye halmashauri nchini kuhakikisha wadaiwa wote wa kodi ya pango la ardhi wanalipa malimbikizo yao ya kodi ili kukusanya maduhuli ya serikali na kusisitiza utendaji kazi wa maofisa hao sasa utapimwa pia kupitia makusanyo ya kodi kwenye maeneo yao.

# Wadaiwa kuuza msitu wa kijiji

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

BAADHI ya viongozi wa kata ya Lugubu, Igunga mkoani Tabora akiwamo Diwani wa Kata hiyo, Magreth Kafumu (CCM), wanatuhumiwa kuuza eneo la msitu wa hifadhi wa Kijiji cha Mgazi.

Licha ya tuhuma hizo, viongozi hao wanadaiwa kuuza eneo hilo kwa Sh. milioni 25 kisha kugawana fedha hizo.

Tuhuma hizo zimetolewa na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Mgazi walipozungumza na waandishi wa habari waotembelea kata hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita kusikiliza malalamiko ya kuuzwa kwa msitu huo wa hifadhi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Charles Shisho, Idd Juma na Dala Amani, walisema walizuiwa kufanya shughuli zozote zile za kibinadamu katika msitu huo lakini cha kushangaza katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019, viongozi hao wamekuwa wakiuuza msitu huo kimya kimya. Kwa mujibu wa Shisho, licha ya wao kupeleka malalamiko yao kwa Diwani Kafumu, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na ndipo baadaye waligundua kwamba naye alikuwa akihusika na tuhuma hizo za kuuza eneo la hifadhi ya kijiji.

Majina ya viongozi wanaokabiliwa na tuhuma za kuuza eneo la msitu huo, kwa mujibu wa wananchi hao, mbali na Kafumu ni aliyekuwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Masaka Chupa, ambaye kwa sasa amehamishiwa katika kijiji cha Lugubu.

Wengine ni waliokuwa wajumbe wa serikali ya kijiji hicho pamoja na kamati ya ugawaji, Mwandu Busagala, Mbelele Mwanzalima, Samweli Stephano, Habi Jimoga, Emmanuel Charles na Busagala Saduka.

Wananchi hao walisema viongozi hao waliuza eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 6,000 na kwamba fedha hizo walishindwa kuzipeleka kwenye shughuli za ujenzi wa zahanati, hivyo kuwafanya wananchi hadi sasa kuendelea kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Sambamba na hilo, walifafanua kuwa hawako tayari kuona fedha zao zikiliwa na viongozi wenye uchu na tamaa badala ya kuzipeleka kwenye shughuli za maendeleo.

Walisema iwapo viongozi wa wilaya hawatakuwa tayari kuchukua hatua za kusimamia fedha hizo ili zirudishwe, watakwenda moja kwa moja kuonana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ili kudai haki yao.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Lugubu, Salimu Mpaki, alikiri kupokea malalamiko ya wananchi hao juu ya kuuzwa kwa hifadhi ya kijiji na kwamba tayari suala hilo alishaliripoti kwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga kwa hatua zaidi.

Kafumu alipotakiwa kuzungumzia tuhuma hizo zinazomkabili, alikiri kuuzwa kwa eneo hilo na kwamba fedha za mauzo yake zilitumika kuendeshea kesi ambayo mtu binafsi aliwashtaki viongozi katika Baraza la Ardhi la Mkoa.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


## KUPOTEA KWA CHETI



**ZAINABU G. JOHN** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S.1520/0046 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KISONDELA SEKONDARI mwaka 2014.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MAG/RB/40/2020.

115601402

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Mohammed enterprises ltd** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki Aina ya **BAJAJI BOXER** yenye namba ya usajili **MC 885 CGD.** Chasis no. **MD2A21BY1KWA95950** Engine no.**PFZWKA93120.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/600818/2019**

215601502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**
**SHAURI NA 309 LA 2019**
**MARY THADEO……..MDAI**
**DHIDI YA**

1. **JAMES KIZITO JOHN**
2. **DAVIDCHARLES MARWA…………WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: JAMES KIZITO JOHN**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yako katika baraza la ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 30.01.2020 katika chumba cha baraza, barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAA- ukijua kwamba kushindwa kufika, kutapelekea baraza kusikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya baraza leo tarehe 16/01/2020

215601102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;19/2020**

**Ombi la AYUBU SIKWEJALA MWASUMBI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi rehemu JACOB MWASUMBI MWAKAJILA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/01/2020.

Tarehe 22/1/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115602502

**JAMUHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Mahakama**
**Usimamizi wa mirathi form II**
**(S.M.M 1984 Nyongeza ya 5 kanuni 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo Dodoma Mjini
Usimamizi wa mirathi 09/2020
Ombi la **HONORATHA HENRY MSUYA** kuteuliwa

Msimamizi wa Mirathi ya Joseph Henry MSUYA
Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe.... Kabla ya mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 21/1/2020.

115601002

**The United Republic of Tanzania**
**Judiciary**
**In The District Court Of Dodoma At Dodoma**
**Execution 20 Of 2019**
**Yahya Bakari Itara……………. Plaintiff(s)**
**Yusufu Swalehe Said.. ……….Defendant (s)**
**Notice to show cause why execution should not issues**
**(O.XXI, r.20(1) of the civil procedure code)**

**To YUSUPH SWALEHE SAID**
Whereas the plaintiff has made application to this court for execution of decree in the above suit on the allegation that the said decree has transferred to him by assignment or without assignment) this is to give you a notice that you are to appear before this court on the 19/02/2020 to show cause why execution should not be granted.

Given under my hand and the seal of the court, this 15th Jan 2010.

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA REGION

215602002

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**MUHAMMAD KASHIF SERAJ** anatangaza KUPOTELEWA na kadi ya GARI aina ya **TOYOTA IPSUM** yenye namba za usajili **T601BUH.** Chesis no. **ACM265012072** Egine **no.2AZ0982370.** Yeyote ataeona atoe taarifa kituo Cha polisi. **DOD/DOD/RB/57650/2020**

115601602


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SARRI ACHEKELEA NAPOLI KUIFUNGA JUVENTUS

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri amesema alikuwa na furaha kwa Napoli baada ya timu yake hiyo ya zamani kuifanya Juventus kupokea kipigo cha pili msimu huu kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na kuwazui kuongoza ligi kwa tofauti ya poiti sita dhidi ya Inter.

Ingawa Cristiano Ronaldo alifunga kwenye mchezo wake wa nane mfululizo, haikutosha kwa mabingwa hao watetezi kuondoka na ushindi baada ya mabao ya Piotr Zielinski na Lorenzo Insigne kuwafanya Napoli kupata ushindi wa 2-1, juzi Jumapili.

Kulikuwa na mabango ya kumbeza Sarri kwenye uwanja huo wa San Paolo, lakini kocha huyo alionyesha furaha kuwaona Napoli wakipata ushindi huo.

"Nina furaha kwa hawa jamaa, mara zote nimekuwa nyuma yao," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Kama ni kupoteza mchezo, nafikiri ni afadhali hapa Napoli ili wamalize matatizo yao. Angalau sasa wameanza kushinda na pengine hata mchezo wao ujao watashinda."

Napoli huo ulikuwa mchezo wake wa kwanza wa ligi kushinda nyumbani tangu Oktoba baada ya katikati ya wiki kushinda kwenye mchezo wa Coppa Italia dhidi ya Lazio.

# Klopp athibitisha kutokaa benchi Liver

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amethibitisha hataiongoza timu yake hiyo kwenye mchezo wa marudiano wa Kombe la FA raundi ya nne dhidi ya Shrewsbury Town, na Neil Critchley atachukua majukumu ya kukiongoza kikosi hicho.

Mchezaji Jason Cummings alitokea benchi na kuifunga mara mbili Liverpool, Jumapili na kuwawezesha kupata sare ya 2-2 na timu hiyo ya daraja la kwanza Shrewsbury na sasa timu hizo zitarudiana kwenye Uwanja wa Anfield mwanzoni mwa mwezi ujao.

Mchezo huo utaangukia wakati wa mapumziko mafupi ya Ligi Kuu, huku Klopp akiamua kuwapumzisha nyota wake katika mchezo huo wa marudiano.

Kocha msaidizi, Critchley ambaye ni kocha wa kikosi cha Liverpool chini ya umri wa miaka 23, alitolewa kwenye Kombe la EFL na Aston Villa mwanzoni mwa msimu huu wakati timu ya wakubwa ilipokuwa kwenye michuano ya Klabu Bingwa ya Dunia nchini Qatar.

"Nitakuwapo benchi na wachezaji wakubwa watapumzika, maana wiki inayokuja itakuwa ngumu kwa upande wetu," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.





# *Valladolid yamwamsha Zidane Real Madrid*

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane ametaka kuimarika zaidi kwa Real Madrid baada ya kikosi hicho kuhitaji bao la dakika za mwisho kupata ushindi wa 1-0 dhidi ya Real Valladolid kwenye Uwanja wa Jose Zorrilla, Jumapili.

Nacho alitumia vizuri pasi ya Toni Kroos kuwapa ushindi huo Madrid dakika ya 78 kwenye mchezo ambao ulionekana kuwa mgumu kwako na vijana hao wa Zidane wakamaliza kwa kupata pointi tatu za kupanda kileleni mwa msimamo wa LaLiga.

Zidane alisifia safu ya ulinzi yake baada ya Valladolid kushindwa kupenya na kupata bao.


"Ulinzi ni safu inayofanya vizuri, tunafanya vizuri. Ni imara kwa upande wetu," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulijilinda vizuri na tulipoteza mpira tuliupata kwa haraka, na kama tukiendelea hivyo tutakuwa na nafasi nzuri ya kufunga.

"Nacho alifunga na hiyo ni sehemu ya soka. Tunajua kwamba tunaweza kuimarika kwa kiasi fulani.

"Nacho ni mchezaji wa aina yake. Wakati anapotakiwa kumalizia, anafanya vizuri. Nimefurahishwa na bao lake; mara zote anawafunga, lakini kwa muda unavyokwenda, anaweza pia kutengeneza nafasi kwa walinzi."

## HABARI MICHEZO



# KOBE BRYANT
## Umeondoka mapema kaka

**CALIFORNIA,** Marekani

KOBE Bryant alikuwa "mmoja wa wachezaji wa kuvutia zaidi" katika historia ya mchezo wa kikapu "ambaye aliwahamasisha watu wengi duniani" kucheza mchezo huo.

Amefariki akiwa na umri wa miaka 41, kwa ajali ya helikopta mjini California Jumapili akiwa na binti yake, Gianna mwenye umri wa miaka 13.

Bryant, ambaye alistaafu kucheza mpira wa kikapu mwaka 2016 baada ya miaka 20 kwenye mchezo huo akiwa na timu ya Lakers, alikuwa mshindi mara tano wa taji la NBA na alitajwa kwenye timu ya nyota wote wa NBA mara 18.

"Familia ya NBA imepatwa na mshtuko mkubwa kwa kifo cha Kobe Bryant na binti yake Gianna," amesema Kamishna wa NBA, Adam Silver.

"Kwa misimu 20, Kobe alituonyesha sisi nini kinachowezekana wakati unapokuwa na kipaji kikubwa. Alikuwa mmoja wa wachezaji wa kuvutia kwenye historia ya mchezo wetu na amemaliza akiwa gwiji.

"Lakini tutamkumbuka zaidi kwa kuwahamasisha watu duniani kuamua kucheza mpira wa kikapu na kushindana kwenye ubora wa juu kabisa."

Shaquille O'Neal, ambaye alishinda mataji matatu ya NBA akiwa na Bryant pale LA Lakers, amesema: "Hakuna maneno ya kuelezea maumivu niliyonayo, naumia mno kumpoteza yeye pamoja na binti yake. Patina wangu wa ushindi.

"Nakupenda na nitakumisi sana. Rambirambi zangu zinakwenda kwa familia ya Bryant na familia ya abiria wengine waliokuwa kwenye helikopta. Mimi ni mgonjwa kwa sasa."

Mfungaji wa wakati wote wa nyota wote wa NBA, Kareem Abdul-Jabbar, ambaye aliichezea Lakers kuanzia mwaka 1975 hadi 1989, amesema: "Ni vigumu kwa upande wangu kuzungumza maneno namna ninavyojihisi. Kobe alikuwa mtu wa familia, alimpenda mke wake na binti zake, alikuwa mwanamichezo wa aina yake, alihamasisha kizazi chote. Kifo chake ni ngumu mno kukikubali."

Rais wa zamani wa LA Lakers, Magic Johnson, bingwa mara tano wa NBA miaka ya 1980, aliandika kwenye twitter yake: "Kobe alikuwa kiongozi wa mchezo wetu, mwalimu wa wachezaji wa kike na kiume. Maneno hayawezi kutosha kuelezea kile alichoufanyia mchezo wa kikapu."

Mshindi mara sita wa NBA, Michael Jordan amesema: "Nilimpenda Kobe - alikuwa kama mdogo wangu. Tulikuwa tunazungumza mara kwa mara, na nitamisi sana ile mijadala yetu."

LeBron James ambaye alimpiku Bryant na kushika nafasi ya tatu kwa kuwa mfungaji wa wakati wote wa NBA Jumamosi, amesema: "Nina furaha kuwa kwenye daraja moja na Kobe Bryant.

"Mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote kuwahi kucheza mpira wa kikapu niliyemshuhudia, mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote wa Lakers."

Bryant alimaliza kipindi chake cha kuichezea Lakers akiongoza kwa pointi za kufunga, na sasa anashika nafasi ya nne kwa kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa NBA akiwa na pointi 33,643.

Katika mchezo wake wa mwisho na Lakers Aprili 2016, alifunga pointi 60 kwa mara ya sita.

Lakers walistaafisha jezi namba 24 aliyokuwa anaivaa Bryant Septemba mwaka 2017.

### RONALDO, MESSI, TYSON NA WOODS NAO WAMLILIA

Gwiji wa mchezo wa golf, Tiger Woods na mshindi mara 15, amesema alisikia habari hizo wakati akicheza raundi ya mwisho katika mashindano ya Farmers Insurance Open mjini California.

"(Caddie) Joey La Cava aliniambia toka nje. Sikuelewa kwa nini umati wa mashabiki ulikuwa ukiimba 'Mamba mzuri', sasa najua," amesema.

"Hakika inaumiza sana, kwa sababu alikuwa mtu wa watu na mwenye historia ya aina yake kwenye kikapu."

Bingwa wa zamani wa masumbwi wa uzito wa juu, Mike Tyson aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Nailia duniani. Tumempoteza gwiji. Sina maneno. Nimehuzunika mno. RIP Kobe Bryant, Gianna na abiria wengine."

Nahodha na mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Sina maneno... mapenzi yangu yote kwa familia ya Kobe na marafiki. Lilikuwa jambo zuri zaidi kwangu kukutana na wewe na kutumia muda tukiwa pamoja. Ulikuwa na kipaji cha ukweli kama watu wengine wachache."

Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo amesema "amevunjika moyo", akiongeza, Bryant alikuwa "gwiji wa ukweli na aliyewahamasisha wengi", huku kiungo wa Manchester United, Paul Pogba akisema: "Mashujaa wanakuja na kwenda, magwiji wanabaki moyoni milele."

Bingwa mara sita wa mbio za magari za Formula 1, Lewis Hamilton amesema: "Nina huzuni kubwa kusikia kwamba tumempoteza mmoja wa magwiji wetu. Bryant ni mmoja wa mwanamichezo bora wa wakati wote aliyewahamasisha wengine nikiwemo na mimi."

Nyota wa Brazil na Paris St-Germain, Neymar ambaye aliifungia timu yake mabao mawili dhidi ya Lille Jumapili, alilitoa bao la pili kwa Bryant.

Neymar alishikilia vidole viwili vya mkono mmoja na vinne vya mkono mwingine vingine akiwa na maana ya kuonyesha namba 24 jezi aliyokuwa akivaa Kobe wakati akichezea Los Angeles Lakers.

Baada ya mchezo huo, Neymar - ambaye ni shabiki mkubwa wa mpira wa kikabu, alimsifia Bryant akisema kwamba, kifo chake ni huzuni kwa dunia yote ya michezo."

Mchezaji namba moja wa tenis duniani, Rafael Nadal aliandika kwenye twitter yake: "Nimeamka asubuhi hii na habari za kutisha kwa kifo cha Kobe Bryant, binti yake Gianna na abiria wengine. Rambirambi zangu kwa mkewe na familia yake yote."

Mshambuliaji wa Manchester United na timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford naye aliandika kwenye Twitter yake: "Mtu aliyehamasisha wengi kwenye michezo. RIP gwiji." Na nyota wa Manchester City, Raheem Sterling akaongeza: "Pumzika kwa urahisi gwiji."

Bryant ambaye alimuoa Vanessa aliyejaliwa naye kupata mabinti wanne, hadi anafariki alikuwa shabiki mkubwa wa soka wa timu za Barcelona, AC Milan na Manchester City.

Na hadi anafariki alikuwa hazungumzi na wazazi wake (baba na mama yake) ambao walimkataza asioe mwanamke mzungu, huku pia yeye akiwatuhumu wazazi wake hao kuuza picha zake za utotoni kwa mamilioni ya dola bila kumhusisha.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES AZIDI KUIVURUGA UTD

Cha juu chazua utata mpya, Jorge Mendes amfuata Ed Woodward Old Trafford, wateta...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United bado haijafikia thamani Sporting Lisbon inayoitaka kwa kiungo wake, Bruno Fernandes, wakati huu mazungumzo yakiendelea kati ya klabu hizo mbili.

**Alhamisi klabu hizo mbili zilitofautiana thamani ya pauni milioni 10 wakati United ilikuwa tayari kulipa pauni milioni 42 na awali wakiwa wamekubaliana kukamilisha mpango huo kwa pauni milioni 55.**

Wakati zikiwa zimebaki siku nne kabla ya dirisha dogo la Januari kufungwa, Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer anataka kuongeza nguvu katika safu ya ushambuliaji, hasa kwa kuzingatia Marcus Rashford ni majeruhi.

Hata hivyo, mazungumzo bado yanaendelea, na United sasa ipo tayari kulipwa zaidi pauni milioni 46.

Wiki iliyopita, Sporting walitumai kufikia muafaka na United wa kununua kiungo huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 25.

Wakala maarufu Jorge Mendes alikwea pipa hadi Manchester akiwa na Rais wa Sporting, Frederico Varandas, pamoja na Mkurugenzi wa Soka, Hugo Viana, kwenda kukamilisha dili hilo na Makamu Mwenyekiti wa United, Ed Woodward.

Kama mazungumzo yalibadilika na United walibadilisha msimamo wao, na Mendes ambaye amekuwa akishauri Sporting kuhusu masuala ya usajili tangu majira ya joto yaliyopita, alipendekeza katika mazungumzo yake na Sky Sports News kuwa United ina hatari ya kumkosa kama ingesubiri dili hilo kwa muda mrefu.

Dili hilo limeendelea kuchanganya zaidi bado kukiwa na madai kwamba mkataba wa Fernandes unajumuisha kipengele ambacho wakala wake, Miguel Pinho, atapaswa kulipwa asilimia 10 ama pauni milioni nne, kama Sporting itapokea ofa ya pauni milioni 42 kwa mchezaji wake huyo, hata kama mpango huo hautafanikiwa.

Fernandes anataka kujiunga na United, lakini kadri ilivyo simama kwa sasa, anabaki kuwa mchezaji wa Sporting na anaendelea kucheza.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KWA RODRIGUEZ

ARSENAL inajiandaa kuingia vitani na Everton kuiwania saini ya kiungo wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez, 28. ***(AS, via Mail)***

### EMRE CAN BADO LULU UTD

MANCHESTER United bado inatumai kukamilisha dili la kiungo wa Juventus na Ujerumani Emre Can, 26, aliyewahi kuitumikia Liverpool. ***(Express)***

### SPURS YAMKARIBIA BERGWIJN

TOTTENHAM inakaribia kukamilisha dili la kuinasa saini ya mshambuliaji wa PSV Eindhoven, Mholanzi Steven Bergwijn, 22. ***(Mirror)***

### BEN YEDDER KUMRITHI SUAREZ

BARCELONA imetoa ofa ya pauni milioni 67 kwa mshambuliaji wa Monaco, Wissam Ben Yedder. Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29, ataziba pengo la majeruhi Luis Suarez. ***(Foot Mercato)***

### KUINUFAISHA SPURS

TOTTENHAM itastahili kupata pauni milioni 10 kama fidia endapo kocha wao wa zamani Mauricio Pochettino atapata kazi ya kuinoa timu nyingine kabla ya mwishoni mwa msimu. ***(Mirror)***

### GENK YAZUIA BERGE EPL

SHEFFIELD United ilitoa ofa kwa kiungo Mnorway Sander Berge ikakataliwa na klabu yake ya Genk, huku pia West Ham ikivutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### ARTETA AMTULIZA MUSTAFI

BEKI wa Arsenal, Shkodran Mustafi, 27, alihusishwa na kuondoka London majira ya joto, lakini Kocha Mikel Arteta anaamini anaweza kumbadili nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani. ***(Telegraph)***

### SPURS YAMRUDIA PIATEK

TOTTENHAM imefungua tena meza ya mazungumzo na AC Milan kuhusu uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Poland, Krzysztof Piatek, 24. ***(Sky Italia, via Mail)***

### 'CHRIS HANA HATI PUNGUZO'

MANCHESTER United imekataa kushusha dau la pauni milioni 25 inalotaka kwa Chris Smalling licha ya ombi hilo kutoka kwa Roma, sehemu ambayo beki huyo wa England anacheza kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Sun)***

### SUSO ANUKIA KUTUA SEVILLA

KIUNGO wa zamani wa Liverpool anayeichezea AC Milan kwa sasa, Mhispania Suso, 26, anatarajiwa kujiunga na Sevilla. ***(Calciomercato)***

### LEEDS YAMTAKA AUGUSTIN

LEEDS United inajiandaa kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig, Jean-Kevin Augustin, 22, kwa mkopo kwa kipindi kilichobaki msimu huu. Mfaransa huyo amekuwa akicheza kwa mkopo kwa kipindi cha nusu msimu wa kwanza. ***(Star)***

HABARI MICHEZO

## Shime hesabu Uganda U-17

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17, sasa itakutana na mahasimu wao Uganda katika hatua ya pili ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia la Vijana zinazotarajiwa kufanyika Juni, mwaka huu nchini India, imefahamika.

Tanzania imesonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuwafunga Burundi jumla ya mabao 6-1, ikishinda 5-1 nyumbani na kupata ushindi wa ugenini wa bao 1-0.

Uganda yenyewe imesonga mbele katika mashindano hayo baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ethiopia katika mechi ya kwanza iliyochezwa Januari 11, mwaka huu jijini Kampala na juzi jioni ilipata ushindi wa 3-1 ikiwa ugenini jijini Addis Ababa.

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi baada ya kutua nchini wakitokea Burundi, Kocha Mkuu wa Tanzania, Bakari Shime, alisema wamerejea nchini na mapema wataanza maandalizi kwa ajili ya mchezo huo unaofuata.

Shime alisema anaifahamu vema Uganda baada ya kukutana nao katika mashindano mbalimbali na anaamini wakijipanga vema, watawatoa na kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Ni jambo zuri kumjua mpinzani wao, Uganda si wageni kwetu, tumecheza nao mara kadhaa, naamini ni kujipanga vizuri ili kuhakikisha tunafanya vizuri na kusonga mbele," alisema Shime.

Timu hizo za vijana zilikutana katika mashindano ya Kombe la Chalenji Afrika Mashariki na Kati na baada ya dakika 90, mchezo huo ulimalizika kwa sare ya bao 1-1, Tanzania ikitangulia kuziona nyavu.

## Tanga yajipanga kuibeba Sahare

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Tanga (TRFA), kimesema kitashirikiana na wadau mbalimbali jijini humo ili kuisaidia Sahare All Stars iweze kufanya vizuri katika mashindano ya Kombe la FA ambayo yanaendelea hapa nchini.

Sahare All Stars imetinga hatua ya 16-bora ya mashindano hayo baada ya kuwatoa Mtibwa Sugar kwa penalti 3-2, kufuatia dakika 90 za kawaida kumalizika wakiwa na sare ya bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa TRFA, Beatrice Mgaya, alisema wamefurahi kuona timu hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza imefika hatua hiyo na sasa zinahitajika nguvu za pamoja ili iendelee kufanya vema kwenye michuano hiyo.

Mgaya alisema katika soka hakuna lisilowezekana na wanaamini wakiiandaa vizuri, inaweza kufika fainali na hatimaye kubeba kikombe cha mashindano hayo.

# LEO USIKU WA SAMATTA

**Na Mwandishi Wetu**

MBWANA Samatta leo anatarajiwa kuwachelewesha usingizi Watanzania wakati atakaposhuka dimbani majira ya saa 4:45 usiku kuichezea timu yake mpya ya Aston Villa kwa mara ya kwanza, kwenye mechi ya Kombe la Ligi dhidi ya Leicester City katika Uwanja wa Villa Park.


**Samatta alianza kujifua na wachezaji wenzake kwa mara ya kwanza Ijumaa iliyopita na Kocha wa Aston Villa, Dean Smith, alisema anaweza kuwa tayari kwa mchezo wa nusu fainali ya pili ya Kombe la Ligi (Carabao Cup) dhidi ya Leicester City leo.**

Hata hivyo, mashabiki wa Aston Villa wametakiwa kuwa watulivu kwa Samatta kwa kuwa haitakuwa rahisi kwake kuzoea 'ligi hiyo ngumu zaidi duniani'.

"Amefunga mabao mengi, lakini hajathibitisha katika Ligi Kuu England," beki wa pembeni wa zamani wa Aston Villa , Alan Hutton alisema. "Ni ligi ngumu duniani."

Samatta, 27, ambaye alikamilisha uhamisho wake kutoka KRC Genk ya Ubelgiji kwenda Villa wiki iliyopita kwa takriban pauni milioni 8.5 hadi anaondoka alishacheka na nyavu mara 10 kwenye mashindano yote huku msimu uliopita akiifungia timu hiyo ya jumla ya mabao 42.

Tangu ametua Aston Villa, Watanzania wengi wamekuwa nyuma yake wakitangaza kuishabikia timu hiyo, na kuanzia wiki iliyopita habari ya mjini imekuwa mechi dhidi ya Leicester kabla ya Jumamosi kusubiria tena kumuona akicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu England wakati Aston Villa itakapokuwa ugenini dhidi ya Bournemouth.







Winga wa Yanga, Mghana Bernard Morrison akishangilia na mchezaji mwenzake, David Molinga baada ya kuifungia timu yake bao la kwanza kwa penalti kwenye mechi ya Kombe la FA dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Taifa juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mtibwa yajipanga kuisambaratisha Azam*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kutolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema kikosi chake kinaelekeza nguvu katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na wanaamini watatimiza malengo waliyonayo.

Mtibwa Sugar inatarajia kukutana na Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema wachezaji wake wameshaanza maandalizi ya kuwavaa Azam na wamejiandaa kukutana na ushindani katika mchezo huo.

Katwila alisema anahitaji kuona kasi waliyokuwa nayo kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi inahamia Ligi Kuu ambayo sasa imeingia katika mzunguko wa lala salama.

"Tumeshaanza mazoezi kwa ajili ya mechi za ligi, sijapumzisha wachezaji, lengo ni kuhakikisha tunaondoka na pointi tatu katika mchezo huo, tunawajua vema Azam, ninashukuru mpaka sasa hatuna majeruhi katika kikosi chetu," alisema Katwila.Aliongeza kuwa bado anaendelea kurekebisha makosa yaliyojitokeza katika mchezo uliopita dhidi ya Sahare All Stars na anaamini wachezaji wake wataingia na kasi tofauti.

"Naomba mashabiki wetu wasikate tamaa na matokeo yaliyopita, tumejipanga kuwafuta machozi, tunawataka waendelee kutuamini na kutuunga mkono, tumeweka nguvu zote katika Ligi Kuu, hatutawaangusha," alisema Katwila.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Mtibwa Sugar iko katika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 22 baada ya kucheza michezo 16, huku Azam FC yenye ina pointi 35 na imeshuka dimbani mara 16 iko katika nafasi ya pili nyuma ya vinara, Simba wenye pointi 41.

# Michezo

Jumanne Januari 28, 2020

Nipashe






Leo ni usiku wa Samatta HABARI UK.31





Gianna na Bryant

# Kobe Bryant, Gianna walivyoacha majonzi

- Rais Trump, Obama, Messi, Ronaldo wamlilia
- Hadi anafariki alikuwa hazungumzi na wazazi wake
- Ni shabiki kindakindaki wa Barca, Man City na Milan

**CALIFORNIA,** Marekani

SI ulimwengu wa michezo tu, bali dunia nzima imezizima na kujawa na majonzi makubwa kufuatia ajali ya helikopta iliyokatisha maisha ya gwiji wa mpira wa kikapu, Kobe Bryant na mwanawe kipenzi, Gianna.

**Bryant, aliyefariki dunia Jumapili usiku akiwa na umri wa miaka 41 na mwanawe mwenye umri wa miaka 13, ni "mmoja wa wachezaji wa kuvutia zaidi" katika historia ya mchezo wa kikapu duniani.**

Katika ajali hiyo, walifariki jumla watu tisa akiwamo Bryant, Gianna na wachezaji wenzake wa mpira wa kikapu.

Ajali hiyo iliwakuta wakiwa wanaelekea Thousand Oaks, California, kwa mchezo wa mpira wa kikapu (basketball) chanzo kikitajwa kuwa ni kutokana na



wingu zito, ambao Gianna alitarajiwa kucheza na Bryant akitarajiwa kumnoa katika mchezo huo.

Bryant, alidumu katika mchezo huo kwa kiwango cha juu kwa takriban miaka 20 kabla kustaafu mwaka 2016 akiwa na timu ya LA Lakers, wakati huo akiwa mshindi mara tano wa taji la NBA na alitajwa kwenye timu ya nyota wote wa NBA mara 18.

Mastaa wengi, wanasiasa pamoja na watu maarufu duniani wamemlilia nyota huyo ambaye ameacha alama kubwa katika mchezo wa kikapu duniani.

Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Kobe alikuwa gwiji. Kumpoteza yeye na Gianna ni maumivu makali mno moyoni hasa kwa sisi wazazi. Michelle na mimi tumetuma salamu za sala kwa Vanessa na familia yote ya Bryant juu ya siku hii isiyofikirika."

Rais wa Marekani, Donald Trump amesema: "Kobe Bryant, licha ya kuwa mchezaji bora zaidi wa wakati wote wa mchezo wa kikapu, ndio kwanza alikuwa akianza maisha. Aliipenda sana familia yake, na alikuwa na hamasa kubwa na majaliwa yake ya baadaye. Kupomteza binti yake mzuri Gianna, kunaufanya wakati huu kuwa mgumu zaidi."

HABARI ZAIDI UK. 29

# Morrison, Niyonzima gari limewaka kikosini Yanga

**Na Somoe Ng'itu**

MBALI na kupata ushindi katika mechi zake mbili zilizopita dhidi ya Singida United na Tanzania Prisons, habari ya mjini si matokeo ya michezo hiyo, bali ni mbwembwe na kiwango cha winga mpya wa Yanga Mghana, Bernard Morrison na namna walivyotengeneza muunganiko mzuri na Haruna Niyonzima.

Kwa muda mfupi tangu atue Yanga, winga huyo ambaye ameichezea timu yake mpya mechi mbili, amefunga bao moja na kutengeneza nafasi mbili za kufunga, tayari amekuwa 'gumzo' na kipenzi cha mashabiki na wanachama wa klabu hiyo na kurejesha imani iliyopotea klabuni hapo tangu kutimuliwa kwa Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera.

Winga huyo amekuwa kivutio hasa baada ya kuonyesha makeke yake kwenye mchezo wake wa kwanza mbele ya Singida United ambapo alicheza na mpira kwa kutembea juu na kupiga pasi na alifanya hivyo tena juzi dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Lakini pia utamu umeongezeka kutokana na kuelewana vema na Niyonzima aliyerejea Yanga baada ya kuondoka kwa misimu miwili, kwani amekuwa akiongeza 'udambwidambwi' katika kikosi kuku akifunga bao la kwanza msimu huu kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Singida United, lakini pia akitengeneza nafasi za kufunga kwa Yikpe Ghislain katika mchezo wa Kombe la FA juzi.

"Hii ndiyo Yanga, sasa kila atakayekuja lazima akae, hii ndiyo Yanga yetu tuliyokuwa tunaitaka na kuifahamu," alisema shabiki mmoja wa timu hiyo aliyejitambulisha kwa jina la Abdallah Msuka.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael amesema hafurahishwi na 'mbwembwe' na mitindo ya nyota huyo ambaye sasa yuko kwenye 'midomo' ya Wanayanga.

"Nilimzuia aache kuchezea mpira ila nimeona amerudia tena, hili jambo nitazungumza naye tena kwa mara nyingine kwani hanifurahishi mimi na ataigharimu timu, kuna wakati mwingine timu inakuwa haijafunga, sipendi kuona anafanya hivyo, Mohamed Salah anafanya hivyo, Sadio Mane anafanya hivyo, najua Afrika mnapenda, lakini si vizuri, nitamweleza, si vizuri kumdhihaki mpinzani wao," Eymael aliongeza.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >